# TATHMINI YA MWINGILIANOMATINI KATIKA UTUNZI WA EMMANUEL MBOGO: UTAFITI LINGANISHI WA TAMTHILIYA YA *NGOMA YA NG'WANAMALUNDI* NA *FUMO LIONGO*

**REHEMA ADAM MNINGO**

**TASINIFU HII IMEWASILISHWA KUKIDHI MASHARTI YA KUPATIWA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI KATIKA KITIVO CHA FANI NA SAYANSI JAMII - CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2015**

## ITHIBATI

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma Tasnifu hii iitwayo:

**Tathmini ya mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo*:* Utafiti Linganishi wa Tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo,*** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

..............................................................................

Dkt. Hadija Jilala

(**Msimamizi**)

**Tarehe**: .....................................................

## TAMKO

Mimi **Rehema Adam Mningo,** nathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya masharti ya kupata shahada yoyote.

**Saini** ................................................................................

**Tarehe** ............................................

## HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe kazi nzima au sehemu ya kazi hii bila kibali cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma za Uzamili na Uzamivu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa niaba ya mwandishi, isipokuwa kwa shughuli halali, kama vile kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma.

## IKIRARI

Tasnifu hii ni nakala halisi ambayo imehifadhiwa na hairuhusiwi kwa mtu yeyote kunakili au kuiga kazi hii, isipokuwa wale wanaofanya utafiti, kujisomea au kufanya mapitio ya maandishi, bila idhini ya mwandishi wa tasnifu hii, au na Mkurugenzi wa masomo ya Uzamili na Uzamivu, kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

## TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa wazazi wangu, Bw. Adam Mningo na Bibi Amina Mningo kwa kunizaa, kunilea, kunisomesha, na kunipa moyo katika kipindi chote cha masomo yangu, tangu darasa la kwanza mpaka sasa ninapokamilisha masomo yangu ya shahada ya uzamili. Mawazo yenu na busara zenu katika elimu nitazikumbuka daima na kuwa chachu ya kujiendeleza zaidi.

Vilevile ninamtabarukia mume wangu kipenzi Juma Ahmed Kabelwa, kwa ushawishi, uvumilivu, huruma na kunitia moyo pale nilipokata tamaa katika masomo yangu. Pia kwa msaada wa hali na mali katika kukamilisha masomo yangu, ikiwa ni pamoja na gharama za masomo na kuwa msimamizi na nguzo imara katika kuhakikisha sikati tamaa ila ninamaliza masomo yangu, tangu stashahada mpaka sasa shahada ya uzamili.

Ninawatabarukia pia wanangu Amina Kabelwa, Ahmed Kabelwa na Shabani Kabelwa, pia mkwe wangu Salmini Shekalaghe na wajukuu zangu Farhiya Salmini na Farhad Salmini, kwa uvumilivu wao katika kipindi chote cha masomo yangu. Ni matumaini yangu kuwa wataweza kutambua umuhimu wa elimu katika maisha ya mwanandamu ili iwe ni changamoto kwao.

## SHUKRANI

Kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa kila kitu, kwa kunijaalia afya njema, nguvu, uwezo, akili, busara, maarifa, utulivu na uvumilivu katika kipindi chote cha masomo yangu ya uzamili. Nashukuru tena kwa unyenyekevu kwa kusema, Alhamdulillah Rabbilaalamina.

Pili, napenda kumshukuru kwa dhati Msimamizi wangu Dkt. Hadija Jilala kwa kuniongoza vyema katika kila hatua ya utafiti huu. Hakusita wala hakuchoka kunishauri na kuirekebisha kazi hii katika hatua zote mpaka ilipokamilika. Amenilea kitaaluma na kunipa misingi ya nadharia za fasihi, fasihi linganishi na mbinu za utafiti ambazo zimezaa kazi hii. Namuomba Mwenyezi Mungu ambariki na ampe afya njema na amzidishie kila la kheri, Amin.

Tatu, napenda kuishukuru familia yangu kwa uvumilivu waliouonyesha kwa kuelewa kuwa nilikuwa masomoni, kwani kwa baadhi ya nyakati waliukosa upendo wa mama.

Nne, napenda kuwashukuru walimu wangu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa kunilea kitaaluma na kunikuza kinadharia na vitendo. Walimu hao ni Profesa E. Mbogo, Profesa T.Y. Sengo, Profesa S. Mdee, Dkt. P. Lipembe na Bwana M. Omary.

Tano, napenda kumshukuru Bi. Tatu Mfaume Katala, kwa kusaidia kuichapa kazi hii ya tasnifu na kuiwezesha kutoka kwa wakati. Mwenyezi Mungu atakulipa kila kheri.

## IKISIRI

Utafiti huu unahusu Tathmini ya mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo: Utafiti linganishi wa tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kufanya tathmini ya mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo, kwa kulinganisha tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988) na *Fumo Liongo* (2009), ili kubaini jinsi mtunzi huyo anavyofumbata mbinu ya mwingilianomatini katika kazi zake za fasihi, na namna mbinu hiyo inavyotumika kuibua dhamira za tamthiliya hizo.

Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalum, wakati ambapo data zilikusanywa kwa kutumia mbinu tatu, ambazo ni mapitio ya maandiko, usaili na majadiliano ya vikundi. Uchambuzi wa data ulifanyika kwa kutumia mbinu ya uchambuzi maudhui. Aidha nadharia ya mwingilianomatini ilitumika kukusanya, kuchambua na kujadili data za utafiti huu.

Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa, mtunzi ameendelea kufumbata mbinu ya mwingilianomatini katika utunzi wake, pamoja na kuwa kazi hizo zina mpishano wa takribani muongo mmoja katika kutungwa kwake. Aidha, tamthiliya zote mbili ni matokeo ya athari za mapokeo simulizi ya Kiafrika, ambapo mtunzi ameathiriwa na mapokeo simulizi ya ngano za kabila la Wasukuma kama dafina ya utunzi wa tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na mapokeo simulizi ya utendi wa "Fumo Liongo" kama dafina ya utunzi wa tamthiliya ya *Fumo Liongo.*

# YALIYOMO

**ITHIBATI** ……………………………………………..…………………………....i

**TAMKO...........** ............................................................................................................ ii

**HAKIMILIKI**.............................................................................................................. iii

**IKIRARI………..** ......................................................................................................... iv

**TABARUKU**.................................................................................................................v

**SHUKRANI**................................................................................................................. vi

**IKISIRI…….** ................................................................................................................ vii

**SURA YA KWANZA** ...................................................................................................1

**1.0 UTANGULIZI WA JUMLA**...............................................................................1

1.1 Utangulizi ..........................................................................................................1

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti .....................................................................................1

1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti ....................................................................................4

1.4 Malengo ya Utafiti...............................................................................................4

1.4.1 Lengo Kuu.........................................................................................................5

1.4.2 Madhumuni mahsusi ..........................................................................................5

1.5 Maswali ya Utafiti ...............................................................................................5

1.6 Umuhimu wa Utafiti.............................................................................................6

1.7 Mipaka ya Utafiti..................................................................................................6

1.8 Uzingativu wa masuala ya Kiitikeli (Kimaadili) ..................................................7

1.9 Muundo wa Tasnifu.............................................................................................10

1.10 Hitimisho ............................................................................................................10

**SURA YA PILI**..............................................................................................................11

**2.0 MAPITIO YA MAANDIKO TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA**..........11

2.1 Utangulizi ............................................................................................................11

2.2 Dhana ya Fasihi Linganishi .................................................................................11

2.3 Dhana ya Mwingilianomatini katika tamthiliya ya Kiswahili ....16
2.4 Utafiti linganishi katika Tamthiliya ya Kiswahili ....19
2.5 Pengo la Maarifa ....21
2.6 Kiunzi cha Nadharia ....22
2.6.1 Nadharia ya Mwingilianomatini ....22
2.6.2 Jinsi Nadharia ya Mwingilianomatini Ilivyotumika katika Utafiti ....25
2.7 Hitimisho ....25
**SURA YA TATU** ....27
**3.0 MBINU ZA UTAFITI** ....27
3.1 Utangulizi ....27
3.2 Eneo la Utafiti ....27
3.3 Kundi lengwa ....28
3.4 Usampulishaji na Mbinu za usampulishaji ....29
3.4.1 Mbinu ya Uteuzi wa Madhumuni Maalum ....30
3.4.2 Mbinu ya Uteuzi Rahisi ....31
3.5 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ....32
3.5.1 Mbinu ya Mapitio ya Maandiko ....32
3.5.2 Mbinu ya Usaili ....34
3.5.3 Mbinu ya Majadiliano ya Vikundi ....35
3.6 Zana za Utafiti ....36
3.6.1 Shajara ....36
3.6.2 Kompyuta ....36
3.6.3 Simu ya Mkononi ....37
3.7 Uchambuzi wa Data ....37
3.8 Hitimisho ....38

**SURA YA NNE** ....................................................................................................40

**4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI**..............................40

4.1 Utangulizi ..........................................................................................................40

4.1.1 Emmanuel Mbogo ni Nani?...............................................................................40

4.1.2 Muhtasari wa Tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ................................43

4.1.3 Muhtasari wa Tamthiliya ya *Fumo Liongo* .......................................................46

4.2 Matumizi ya Mwingilianomatini katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo* 47

*Liongo*...................................................................................................................47

4.2.1 Mwingilianomatini katika utunzi wa *Ngoma ya Ng'wanamalundi*...................48

4.2.1.1 Matumizi ya Hadithi.......................................................................................50

4.2.1.2 Matumizi ya ngoma.........................................................................................54

4.2.1.3 Matumizi ya Nyimbo.......................................................................................59

4.2.1.4 Matumizi ya Majigambo .................................................................................60

4.2.1.5 Matumzi ya wahusika wa fasihi simulizi .........................................................62

4.2.1.6 Matumizi ya Ushairi.........................................................................................63

4.2.1.7 Matumizi ya Nguvu za Sihiri ...........................................................................64

4.2.2 Hitimisho ...........................................................................................................65

4.2.3 Mwingilianomatini katika utunzi wa *Fumo Liongo* .........................................66

4.2.3.1 Matumizi ya Utendi.........................................................................................67

4.2.3.2 Wahusika ........................................................................................................69

4.2.3.3 Kisa.................................................................................................................69

4.2.3.4 Uchu wa Madaraka..........................................................................................71

4.2.3.5 Usaliti .............................................................................................................72

4.2.3.6 Matumizi ya Ngoma.........................................................................................74

4.2.3.7 Matumizi ya Nyimbo.......................................................................................76

4.2.3.8 Matumizi ya Majigambo .................................................................................79

4.2.3.9 Matumizi ushairi....80

4.2.3.10 Matumizi ya Sihiri....81

4.3 Hitimisho....83

4.4 Ulinganishaji wa Matumizi ya Mwingilianomatini Baina ya tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*....84

4.4.1 Kufanana kwa Matumizi ya mwingilianomatini katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*....85

4.4.2 Kutofautiana kwa Mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*....86

4.5 Hitimisho....88

4.6 Dhamira zinazowasilishwa na mbinu ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*....89

4.6.1 Dhamira zinazojitokeza katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*....89

4.6.1.1 Ukombozi....90

4.6.1.2 Ukandamizaji....91

4.6.1.3 Elimu....92

4.6.1.3.1 Elimu Chanya....92

4.6.1.3.2 Elimu Hasi....93

4.6.1.4 Mvutano wa Kitabaka....94

4.6.1.5 Usawiri wa Mwanamke....94

4.6.1.5.1 Mwanamke kama jasiri, shujaa na mwanamapinduzi....95

4.6.1.5.2 Mwanamke kama mwenye kuthamini utu wake na mwenye kujiheshimu. ....96

4.6.1.5.3 Mwanamke kama Chombo cha Starehe cha Mwanaume....96

4.6.1.5.4 Mwanamke kama chombo cha Uzalishaji mali....97

4.6.2 Dhamira zinazojitokeza katika tamthilia ya *Fumo Liongo*....98

4.6.2.1 Uongozi Mbaya....99

4.6.2.2 Rushwa na Usaliti ....100

4.6.2.3 Harakati za Ukombozi ....101

4.6.2.4 Dhamira ya Mapinduzi ....101

4.6.2.5 Usawiri wa Mwanamke ....102

4.6.2.5.1 Mwanamke kama Jasiri ....102

4.6.2.5.2 Mwanamke kama Mwaminifu ....102

4.6.2.6 Ushujaa ....103

4.7 Hitimisho ....104

**SURA YA TANO** ....106

**50. MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ....106

5.1 Utangulizi ....106

5.2 Muhtasari ....106

5.3 Hitimisho ....112

5.4 Mapendekezo ....113

**MAREJEO** ....114

**KIAMBATISHO Na. 1** ....118

**KIAMBATISHO Na. 2** ....119

**KIAMBATANISHO Na. 3** ....120

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 4.1 Matini zilizotumika katika utunzi wa *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ....... 49

Jedwali 4.2 Matini zilizotumika katika utunzi wa *Fumo Liongo*............................... 66

Jedwali 4.3 Matini zinazojitokeza katika Ngoma ya *Ngw'anamalundi* na *Fumo Liongo* ........................................................................................... 85

Jedwali 4.4 Mwingilianomatini na Uibuaji wa Dhamira katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ........................................................................ 90

Jedwali 4.5 Mwingilianomatini na Uibuaji wa dhamira katika *Fumo Liongo*........... 98

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI WA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

Sura hii ni sura tangulizi ambayo kwa ujumla wake inatoa mwongozo wa utafiti huu. Katika sura hii vipengele mbalimbali vinajadiliwa ili kuibua tatizo la utafiti huu. Vipengele vinavyojadiliwa ni usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, uzingativu wa kimaadili, muundo wa tasnifu na hitimisho.

### 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Dhana ya mwingilianomatini imejadiliwa na wataalam mbalimbali wa ndani na nje ya Tanzania. Baadhi ya wataalam wa nje waliojadili dhana hii ni pamoja Kristeva (1980), Allen (2000), na Lemaster (2012). Kristeva (1980) anaeleza kuwa mwingilianomatini ni kuathiriana, kuhusiana na kutegemeana kwa kazi za fasihi, ambapo matini za kifasihi huingiliana na kuchangizana ili kukamilishana. Anaendelea kufafanua kuwa, si rahisi kuzungumzia uasili au upekee wa kazi ya fasihi, kwani kwa vyovyote vile itakuwa imetokana na kazi za fasihi zilizotangulia au zilizopo. Hivyo kuamini kuwa matini ya kifasihi inajitegemea ni kupotoka.

Allen (2000) anafasili mwingilianomatini kuwa ni kuhusiana na kutegemeana kwa kazi za fasihi. Lemaster (2012) anaeleza kuwa, mwingilianomatini katika fasihi, ni pale ambapo kitabu kimoja kinarejelea kitabu kingine katika jina la kitabu, visa na matukio, wahusika na usimuliaji. Vilevile mwingilianomatini ni pale ambapo matini mbalimbali zinatumiwa ndani ya matini ya kifasihi kama vile, matumizi ya matini za

kijamii, wimbo, hadithi za kitamaduni, filamu, maonyesho ya televisheni, na matini za vyombo vya habari.

Kwa upande wa wanafasihi ya Kiswahili dhana ya mwingilianomatini inajadiliwa na wataalam mbalimbali, baadhi yao ni Wamitila (2003), Wamitila (2008), Senkoro (2011), Herman (2011) na Macha (2013). Wamitila (2008) anaeleza mwingilianomatini kuwa ni kule kuhusiana kwa kazi moja ya fasihi na nyingine zilizotangulia. Anabainisha kuwa, mwingilianomatini huo huweza kuwa katika dhamira, wahusika au mtindo.

Senkoro (2011), anasema kuwa, mwingilianomatini ni kule kutumiwa kwa utanzu mmoja wa fasihi katika kutolea au kuwasilishia utanzu mwingine, mfano wimbo ndani ya ngano au hadithi. Halikadhalika yaweza pia kuwa ni uwepo wa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi fulani ya fasihi, mfano matumizi ya nyimbo, barua, ngoma, masimulizi ya hadithi, misemo na nahau. Akiunga mkono hoja hii Macha (2013), anaeleza kuwa, mwingilianomatini ni ule uwepo wa sifa mbalimbali za matini moja katika kazi fulani ya fasihi, kama vile matumizi ya nyimbo, barua, ngoma, masimulizi ya dhati ndani ya hadithi, misemo, nahau, majibizano, vicheko na picha.

Kutokana na fasili ya mwingilianomatini iliyotolewa na wataalam hao tunabaini aina mbili za mwingilianomatini. Aina ya kwanza ya mwingilianomatini ni kule kuathiriana kwa waandishi kupitia kazi zao za fasihi katika vipengele mbalimbali kama vile jina la kitabu, wahusika, visa na matukio, muundo, usimulizi, mtindo na matumizi ya lugha. Aina ya pili ni kule kuhusiana, kuathiriana, kuingiliana na

kujengana kwa matini mbalimbali za kifasihi katika kazi moja ya fasihi. Mwingilianomatini katika aina hii huweza kujibainisha katika matumizi ya vipengele vya kisanii kama vile nyimbo, ngoma, semi, hadithi, ndoto, methali, nahau na hotuba katika kazi moja ya fasihi.

Kutokana na mjadala huo wa dhana ya mwingilianomatini, mtafiti aliona kuna haja ya kufanya utafiti ili kuona ni namna gani mwandishi mmoja anaweza kuweka uwiano wa ubunifu wake katika kazi zake za fasihi. Swali ambalo tulijiuliza ni je, msanii huyu anabadilikaje kulingana na wakati na muktadha katika uteuzi wa vipengele vya kimtindo? Je kuna ushikamani wa matini moja na nyingine katika kuibua dhamira zake? Je fani aliyoitumia muongo mmoja uliopita bado anaitumia hadi sasa? Maswali haya yalileta hamasa ya kutaka kuufanya utafiti huu. Maswali hayo ndiyo yalikuwa chachu ya utafiti huu ili kulinganisha kazi za Emmanuel Mbogo kwa lengo la kubaini namna mwingilianomatini unavyojitokeza katika kazi zake za fasihi kama mbinu ya utunzi.

Kwa hiyo, utafiti huu unachunguza matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988), na *Fumo Liongo* (2009), Emmanuel Mbogo ambazo zimeandikwa kwa vipindi tofauti vinavyopishana kwa takriban muongo mmoja, ili kuona ni jinsi gani msanii huyo anafumbata mbinu ya mwingilianomatini katika kazi zake za sanaa. Kwa kufanya hivi tutaweza kubaini upekee wake katika mtindo wa kisanii na kuweza kusema huyu ndiye Mbogo katika fasihi ya Kiswahili.

## 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Wataalam na watafiti wengi wameshughulika na utafiti wa vipengele vya fani na maudhui katika tamthiliya za Kiswahili. Aidha, wapo watafiti ambao wamefanya tafiti zao kwa lengo la kulinganisha fani na maudhui katika tamthiliya mbili. Baadhi yao ni Saleem (2013), Fadhili (2014) na Mkuwili (2014). Kwa maana hiyo utafiti linganishi ni eneo ambalo si geni. Hata hivyo, kutokana na uelewa wangu, hakuna utafiti ambao umejikita katika kuchunguza na kulinganisha kipengele cha mwingilianomatini katika kazi za mtunzi mmoja. Kwa hiyo, tatizo la utafiti huu ni kuchunguza mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo ili kuona ni jinsi gani msanii huyu anaifumbata mbinu ya mwingilianomatini katika kazi zake za fasihi. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kuibua kufanana na kutofautiana kwa matumizi ya mwingilianomatini katika kazi za msanii mmoja baada ya muongo mmoja, ili kubaini endapo kuna mabadiliko yoyote ya kiubunifu na mtindo wake kisanaa. Kwa hiyo, utafiti huu umelinganisha tamthiliya mbili za mtunzi Emmanuel Mbogo, zilizotungwa katika vipindi tofauti na kupishana takribani muongo mmoja, ambazo ni: *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988), na *Fumo Liongo* (2009), ili kubaini jinsi msanii huyo anavyofumbata mbinu ya mwingilianomatini na jinsi mbinu hiyo ilivyotumika kuibua dhamira.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu umejengwa na lengo kuu na malengo mahsusi matatu kama inavyojibainisha katika sehemu zifuatazo.

### 1.4.1 Lengo Kuu

Lengo la utafiti huu ni kufanya tathmini ya mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo kwa kulinganisha tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988) na *Fumo Liongo* (2009), za Emmanuel Mbogo ili kubaini jinsi mtunzi huyo anavyofumbata mbinu ya mwingilianomatini katika kazi zake za fasihi na namna mbinu hiyo inavyotumika kuibua dhamira za tamthiliya hizo.

### 1.4.2 Madhumuni mahsusi

Utafiti huu ulikuwa na madhumuni mahsusi matatu kama ifuatavyo:-

(a) Kubainisha mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo.*

(b) Kulinganisha na kulinganua matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*.

(c) Kubainisha dhamira zinazojidhihirisha kutokana na matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo.*

## 1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kujibu maswali yafuatayo.

(a) Mwingilianomatini unajitokeza vipi katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*?

(b) Je, kuna kufanana ama kutofautiana kwa matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*?

(c) Ni dhamira zipi zinazojidhihirisha kutokana na matumizi ya mwingiliano matini katika tamthiliya za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo?*

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una umuhimu mkubwa katika taaluma ya Fasihi Linganishi. Kwa hiyo, matokeo ya utafiti huu yatachangia katika maarifa ya nadharia ya Fasihi Linganishi ya Kiswahili. Kwa mfano, kwa kutumia nadharia za Fasihi Linganishi, utafiti huu utachangia katika ulinganishi wa kazi za msanii mmoja zinazopishana kwa takribani muongo mmoja, ili kuona ni jinsi gani zinafanana na kutofautiana katika matumizi ya mbinu za kisanii ili kuibua upekee wa mtindo wa mtunzi huyo kisanii. Utafiti huu utasaidia kuona ulinganisho wa mbinu ya mwingilianomatini jinsi ilivyotumika katika tamthiliya mbili za mwandishi mmoja zilizoandikwa katika nyakati tofauti, na kupishana kwa karibu muongo mmoja, zinavyofanana na kutofautiana na jinsi matumizi ya mbinu hiyo yalivyofanikisha kubainika na kueleweka kwa dhamira za tamthiliya hizo teule.

Vilevile utafiti huu utaweza kutumika kama rejeleo na chachu ya tafiti nyingine katika fasihi na Lugha. Aidha, mapendekezo ya tafiti zijazo katika maeneo ambayo utafiti huu haukuweza kuyagusa kutokana na malengo mahsusi ya utafiti huu, yatasaidia kuwapa mwongozo watafiti wengine ili kuzalisha tafiti nyingi zaidi katika lugha na Fasihi.

## 1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza matumizi ya mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo, lengo likiwa ni kulinganisha tamthiliya ambazo zimeandikwa

katika vipindi tofauti. Emmanuel Mbogo ametunga tamthiliya nyingi, baadhi yake ni *Giza Limeingia,* (1980), *Tone la Mwisho* (1981), *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988), *Morani* (1993), *Fumo Liongo* (2009) na *Sundiata* (2011). Kulingana na malengo ya utafiti huu, tuliamua kulinganisha tamthiliya mbili tu, yaani *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988) na *Fumo Liongo* (2009). Sababu ya kuteua tamthiliya hizo ni kwamba tulilenga kulinganisha tamthiliya za mwandishi huyu katika vipindi tofauti hususani tamthiliya zinazopishana muongo mmoja. Kwa hiyo, tamthiliya hizi zilionekana kuwa na sifa hiyo na zilionekana zinaweza kutufikisha kwenye lengo la utafiti huu. Kwa maana hiyo, utafiti huu umelinganisha tamthiliya mbili tu za Emmanuel Mbogo, tamthiliya zingine za mtunzi huyu hazikutumika katika utafiti huu ingawa zinaweza kutumika hapa na pale kwa lengo la kiulinganishi na kukuza mjadala.

Mkabala ulioongoza utafiti huu kuhusu mwingilianomatini ni ule wa Kristeva (1960). Utafiti huu haukujihusisha na vipengele vingine vya fani na maudhui, kama vile mandhari, wahusika, muundo, migogoro na falsafa, ila vipengele hivyo vimeweza kugusiwa pale tu ilipoonekana ni muhimu kufanya hivyo, hasa katika kuelezea jinsi mwingilianomatini unavyojitokeza katika tamthiliya teule. Hii ni kutokana na sababu kwamba, halikuwa lengo la utafiti huu kujishughulisha na wala kufanya uchambuzi wa vipengele vya fani na maudhui katika tamthiliya hizo.

## 1.8 Uzingativu wa masuala ya Kiitikeli (Kimaadili)

Hiki ni kipengele kinachohusika na masuala ya kimaadili katika utafiti na namna mtafiti alivyoweza kuyazingatia kabla ya utafiti, wakati na baada ya kukusanya data.

Padgett (2002), anafafanua masuala ya kimaadili ambayo huweza kuibuka na yanayopaswa kuzingatiwa katika aina zote za utafiti. Masuala hayo ni pamoja na kuomba idhini na ruhusa ya kufanya utafiti katika maeneo ya utafiti, usiri, uwazi, ushiriki wa hiari kwa wahojiwa, utiifu na uvumilivu.

Utafiti huu ulihusisha watu kutoka asasi mbalimbali. Kwa vile kila asasi ina sheria, taratibu, kanuni na utamaduni wake, kabla ya kufanya utafiti, mtafiti alipata kibali cha kufanya utafiti kutoka Chuo Kikuu Huria. Kibali hicho kilimsaidia mtafiti kuingia katika maeneo ya utafiti. Kabla ya kuwaona watafitiwa, mtafiti aliwaona viongozi au watu wenye mamlaka katika maeneo husika, ili kujitambulisha na kuhalalisha uwepo wake na kubainisha shughuli alizokusudia kuzifanya akiwa katika eneo hilo husika.

Schutt (2006), anaeleza kuwa ni muhimu sana washiriki wa utafiti wakashiriki kwa kujitolea bila kulazimishwa. Katika utafiti huu, mtafiti aliwaomba washiriki wake kushiriki kwa hiari na kwa kujitolea katika kutoa data za utafiti huu. Wahojiwa walioshiriki katika kutoa data za utafiti huu, walitoa data hizo kwa hiari na kwa uamuzi wao bila kushinikizwa na mtafiti. Wakati wa utafiti, mtafiti aliwaeleza watafitiwa lengo la utafiti na kwa nini anahitaji kupata data hizo, na kisha kuwaomba washiriki kikamilifu katika usaili na kujibu maswali yaliyopo kwa hiari. Hata hivyo, mtafiti alijadiliana kwanza na wahojiwa kuhusu lengo kuu la utafiti huu na matarajio yake ili kupata mawazo, maoni na mtazamo wao. Wahojiwa waliweza kutoa mawazo yao, maoni na mtazamo wao kwa kile wanachokifahamu kuhusiana na lengo kuu la utafiti huu kwa uhuru zaidi. Hii ilisaidia kurahisisha zoezi zima la utafiti na shughuli ya ukusanyaji wa data za utafiti huu.

Utafiti huu ulihusisha zana mbalimbali za kukusanyia data kama vile; simu ambayo ilitumika katika mawasiliano na wahojiwa, kurekodi mazungumzo kati ya mtafiti na wahojiwa na kupiga picha za kumbukumbu na mtunzi wa tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Kwa hiyo, kabla ya kutumia zana hiyo, mtafiti aliomba na kuheshimu ridhaa ya washiriki. Mtafiti aliwaeleza wahojiwa sababu na umuhimu wa kutumia zana hizi na kuwaomba ridhaa ya kuzitumia. Wahojiwa walikubali na kuwa tayari kusailiwa kwa kutumia simu na kurekodiwa katika kinasa sauti cha simu hiyo. Ufafanuzi na uwazi huu ulisaidia katika kukusanya data na kufanya zoezi hilo kuwa rahisi. Data za usaili za utafiti huu zilihifadhiwa katika kinasasauti na kurejelewa pale mtafiti anapohitaji. Speziale na Carpenter (2006), wanaeleza kuwa data za utafiti za usaili zinaweza kuhifadhiwa katika vitu mbalimbali kama vile kinasasauti, maandishi, tepurekoda, picha za video, na picha. Hivyo, vitu vyote vyenye uwezo wa kumtambulisha mhojiwa lazima vihifadhiwe kwa uangalifu wakati wa ukusanyaji wa data mpaka mwishoni mwa utafiti.

Usiri ni jambo lingine la kimaadili ambalo mtafiti alilizingatia wakati wa kukusanya data. Speziale na Ronet, kama walivyonukuliwa na Malangwa (2010), wanasema kwamba washiriki hawanabudi kuhakikishiwa na watafiti kuwa usiri wa data wanazozitoa utazingatiwa. Hii ni pamoja na kuwahakikishia kuwa, data hizo hazitatumika vinginevyo zaidi ya kutimiza malengo ya utafiti huu na bila kubainisha chanzo cha data hizo.

Mtafiti alizingatia pia suala la usiri kwa kuwaahidi na kuwahakikishia washiriki wa utafiti huu, ambao walishiriki katika usaili kuwa, data walizozitoa zitakuwa ni siri ya

mtafiti na mhojiwa na zitatumika kwa ajili ya malengo ya utafiti huu. Kwa kuwathibitishia hayo, wahojiwa hawakutakiwa kutaja majina yao, ili kulinda siri ya mtoa data. Vilevile katika mjadala wa matokeo haya, hakuna urejelezi wa jina uliofanywa katika uchambuzi, uwasilishaji na mjadala wa data. Kulingana na ahadi ambayo mtafiti aliitoa kwa wahojiwa wake, data zote alizokusanya kutokana na usaili kwa kinasasauti zimehifadhiwa kwa usiri mkubwa. Hii ni kwamba, mtafiti alichukua tahadhari kubwa katika kuzingatia vipengele vyote vya maadili katika utafiti.

## 1.9 Muundo wa Tasnifu

Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza ni sura tangulizi ambayo inatoa utangulizi wa jumla wa utafiti na kuibua tatizo la utafiti. Sura ya pili inachambua na kujadili mapitio ya maandiko yanayohusiana na utafiti huu na hatimaye kuibua pengo la kimaarifa ambalo ndilo lililohamasisha nia ya kufanya utafiti huu. Aidha, katika sura hii kiunzi cha nadharia kilichoongoza uchunguzi, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti huu kinajadiliwa. Sura ya tatu inafafanua na kujadili mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Sura ya nne ndiyo kiini cha utafiti huu ambapo uchambuzi, uwasilishaji na mjadala wa data na matokeo ya utafiti huu umefanyika kwa kina. Sura ya tano inatoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu.

## 1.10 Hitimisho

Sura hii imetoa utangulizi kwa kubainisha mambo mbalimbali yanayohusiana na utafiti uliofanyika. Mambo hayo ni pamoja na usuli wa tatizo, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, uzingativu wa maswala ya kiitikeli na mpangilio wa tasnifu.

# SURA YA PILI

## 2.0 MAPITIO YA MAANDIKO TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

### 2.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mapitio ya maandiko tangulizi yanayohusiana na mada ya utafiti. Sura hii ina sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza inahusu maandiko tangulizi na sehemu ya pili inahusu kiunzi cha nadharia. Katika sehemu ya kwanza mjadala umejikita katika vipengele vya dhana ya Fasihi Linganishi, dhana ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya Kiswahili, tafiti kuhusu Fasihi Linganishi ya Kiswahili na pengo la kimaarifa. Sehemu ya pili imeelezea kiunzi cha nadharia ya utafiti iliyoongoza utafiti huu.

### 2.2 Dhana ya Fasihi Linganishi

Utafiti huu ni utafiti linganishi, hivyo mjadala wa dhana ya Fasihi Linganishi ulionekana kuwa na umuhimu mkubwa sana ili kutoa uelewa wa dhana hiyo kwa ujumla. Dhana ya kulinganisha fasihi za jamii mbalimbali au mataifa mbalimbali ilianza zama za kale zaidi. (Ponera 2014) anaeleza kuwa, katika wakati huo jamii hizo za kale zilikuwa zinaongozwa na misingi ya vionjo mbalimbali katika kulinganisha utendekaji wa fasihi zao na za jamii nyingine. Vionjo hivyo vilitokana na jamii zilizokuwa na nguvu ya kihadhi. Tukitolea mfano zama za mwanafalsafa wa Kiyunani Aristotle, zilishuhudia kuwapo kwa ulinganishaji na ulinganuzi wa kazi mbalimbali za tamthiliya kwa lengo la kuchuja na kupata kazi bora zilizoafikiwa kupelekwa kwa hadhira. Halikadhalika zama za baada ya Kristo zilijihusisha na ulinganuzi wa matini za kidini (Biblia), wakati ambapo wasanii wa Kiarabu enzi za kati walijihusisha na ulinganishaji na ulinganuzi wa kazi za sanaa.

Akiendelea kueleza, Ponera (2014) anasema kuwa, katika umbo la sasa la kitaaluma, dhana ya Fasihi Linganishi ilianza huko Ufaransa mwishoni mwa karne ya 19 na kupata mashiko mwanzoni mwa karne ya ishirini (20), ikijikita zaidi katika utanzu wa tamthiliya kwa sababu utanzu wa riwaya ulikuwa bado mchanga. Maarifa ya awali ya taaluma hii yalijikita katika kulinganisha maudhui ya sanaa na kaida za maisha ya kila siku ya mwanadamu na mambo yamzungukayo kama vile dini, siasa na matabaka. Wadau wakubwa wa Fasihi Linganishi kwa wakati huo walikuwa ni watu binafsi waliofanya kazi kipwekepweke. Watu hao kwa uchache, kwa mujibu wa Ponera (2014), ni pamoja na Paul Van Tieghen ambae aliandaa makongamano huko Sarbonne kati ya mwaka 1827-1840, yeye aliandika makala na vipeperushi kuhusu dhana ya fasihi linganishi na kuvisambaza sehemu mbalimbali huko Ulaya. Wengine ni Dostoevsky na Marius Franco (Ponera, 2014).

Wataalamu mbalimbali wametoa fasili kuhusu dhana ya Fasihi Linganishi. Miongoni mwao ni Totosy de Zepetnek (1996), anasema kuwa, Fasihi Linganishi ni taaluma inayojihusisha na uteuzi na uchambuzi wa vipengele mbalimbali vya kazi za fasihi, kama vile kanuni, mafundisho na tamaduni ambavyo vinapatikana katika kazi za fasihi za jamii mbalimbali. Akiendelea kuelezea kuhusu taaluma ya Fasihi Linganishi, Totosy de Zepetnek (1998), anaelezea kuwa, Fasihi Linganishi ni taaluma ya ulinganishi wa tamaduni na asili za jamii mbalimbali, pia ulinganishi wa taaluma za sayansi na taaluma nyinginezo zinazohusu tamaduni, filamu, fasihi, habari na mawasiliano. Mtaalam mwingine aliyefasili dhana ya Fasihi Linganishi ni Bassnett (1993), anayeeleza kuwa Fasihi Linganishi ni taaluma ya usomaji matini za taaluma tofauti ili kubaini mazingira zinapokutana na zinapoachana. Wamitila

(2003), naye ameizungumzia dhana hii kwa kusema kuwa ni mbinu ya kuchunguza, kuchambua na kueleza sifa za mfanano zilizopo katika matini ya fasihi na kwamba, dhana yenyewe huenda sambamba na dhana ya ulinganuzi, ambapo ulinganuzi ni mbinu ya kuchunguza, kuchambua na kuonyesha sifa zinazotofautisha baina ya matini zaidi ya moja za kifasihi.

Kutokana na fasili hizo za wataalamu kuhusu dhana ya Fasihi Linganishi, tunaona kuwa mawazo yao hayatofautiani katika mtazamo na mwelekeo juu ya dhana hii. Kwa ujumla, tunakubaliana na mawazo yao kuwa, Fasihi Linganishi ni taaluma inayojishughulisha na ulinganishaji wa kazi za fasihi, ili kubainisha kutofautiana na kufanana kwa fasihi ya makundi mawili au zaidi ya kiisimu, kiutamaduni, kihistoria, kiitikadi, kiuchumi, kijamii na kimataifa.

Kutokana na mbinu zake, Fasihi Linganishi huweza pia ikatumika kulinganisha kazi za fasihi za lugha tofauti, mfano fasihi ya Kiingereza, Kijapani, Kijerumani, Kichina, Kiswahili na nyinginezo, lakini huweza pia ikajishughulisha na fasihi ya lugha moja ikiwa kazi hizo asili yake ni nchi tofauti au utamaduni tofauti ndani ya lugha hiyo. Mfano tunaweza kulinganisha kazi za fasihi za Emmanuel Mbogo na kazi za fasihi za Ebrahim Hussein zilizoandikwa kwa lugha ya Kiswahili.

Halikadhalika kazi za fasihi za mwandishi mmoja zilizoandikwa katika kipindi kimoja ama katika vipindi tofauti vya kihistoria zinaweza kulinganishwa kwa kutumia Fasihi Linganishi. Kwa kuegemea katika dhana hiyo, utafiti huu ulilenga kulinganisha kazi za fasihi za msanii mmoja, ili kuona kufanana na kutofautiana kwa

matumizi ya mwingilianomatini katika kazi za msanii huyo baada ya muongo mmoja, na kubaini endapo kuna mabadiliko yoyote ya kiubunifu. Kama ilivyokwisha elezwa tangu awali, utafiti huu ulilinganisha tamthiliya mbili za mtunzi Emmanuel Mbogo, zilizotungwa katika vipindi tofauti kwa mpishano wa karibu muongo mmoja, ambazo ni; *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988), na *Fumo Liongo* (2009). Lengo lilikuwa ni kubaini jinsi msanii huyo anavyofumbata mbinu ya mwingilianomatini na kuona upekee wake kimtindo katika ufumbataji wa mwingilianomatini katika kazi zake za sanaa, na jinsi mwingilinomatini ulivyotumika katika kuibua dhamira za tamthiliya hizo.

Vilevile kazi za fasihi za kipindi fulani cha kihistoria huweza kulinganishwa na kazi za kipindi kingine cha kihistoria. Katika kila kipindi cha kihistoria huwa na kazi zake za fasihi ambazo huwa na lugha, mandhari, mtindo, muundo na maudhui tofauti kulingana na mahitaji ya jamii kwa wakati husika. Ulinganisho huo husaidia kubaini tofauti na mfanano wa fani na maudhui katika vipindi vya kihistoria ambavyo jamii inakuwa imepitia, kwa mfano, tunaweza kulinganisha kazi za fasihi za kipindi cha mfumo wa chama kimoja na kipindi cha mfumo wa vyama vingi. Hivyo basi, mwelekeo huu ulitusaidia kubaini endapo kazi za msanii mmoja zinabadilika kulingana na vipindi tofauti vya kihistoria. Vilevile mwelekeo huo ulitusaidia kubaini sababu za kufanana ama kutofautiana kwa kazi teule za E. Mbogo. Pia kubaini endapo kuna athari za kihistoria ama za kisanaa za kipindi fulani. Mjadala wa matokeo haya utajadiliwa katika sura ya nne.

Shughuli za taaluma ya Fasihi Linganishi huangalia mambo anuai yanayotakiwa kufanyiwa ulinganisho wa vipengele vya kisanaa. Shughuli zote hizo hufanywa katika nyanja kuu tatu. Ponera (2014), anazitaja nyanja hizo kuwa ni nyanja ya uhakiki linganishi, nyanja ya uhusishaji wa kazi za fasihi na uasili na uhalisi na nyanja ya uhusishaji wa fasihi na sanaa nyinginezo. Kwa kutumia maeneo au nyanja hizo vigezo vya ulinganisho hufanyiwa ulinganisho. Vigezo hivyo vya ulinganisho ni pamoja na kigezo cha maana, uwakati, uigaji na uathiriano, upokezi, unusura, ukanda, fani, maudhui, motifu na utamaduni.

Katika utafiti huu matumizi ya mbinu ya mwingilianomatini katika tamthiliya teule, yalihakikiwa kwa kutumia nyanja ya uhakiki linganishi kwa kuhusisha ulinganisho wa kigezo cha fani. Matini mbalimbali zilizotumika katika utunzi wa tamthiliya teule zimebainishwa kupitia kipengele cha fani ya tamthiliya teule kwa kuhusisha kipengele cha mtindo uliotumika katika utunzi wa tamthiliya hizo, ambazo ni za mtunzi mmoja lakini zilizotungwa katika vipindi tofauti. Sababu za kuchagua nyanja hiyo ya uhakiki linganishi na kigezo hicho cha fani katika utafiti wetu, ni kutokana na kuona kuwa ndiyo nyanja na kigezo kilichoweza kujibu maswali ya utafiti na kutimiza malengo yetu ya utafiti, kwa kulinganisha na kulinganua matumizi ya mbinu ya mwingilianomatini katika tamthiliya za *Ngoma ya Ng’wanamalundi (1988),* na *Fumo Liongo (2009),* ambazo zimeshughulikiwa na utafiti huu. Kupitia utafiti huu linganishi tumeweza kubainisha mfanano na utofauti wa tamthiliya za Emmanuel Mbogo katika matumizi ya mwingilianomatini na jinsi matumizi ya mbinu hiyo yalivyowezesha kujengeka kwa dhamira katika tamthiliya hizo.

Maelezo hayo kuhusu dhana ya Fasihi Linganishi yametusaidia kuelewa fasili ya dhana ya Fasihi Linganishi, nyanja na vigezo vya ulinganisho. Hii ilituwezesha kuelewa kigezo cha ulinganisho katika utafiti wetu, ambapo kilitumiwa kulinganisha na kulinganua matumizi ya mbinu ya mwingilianomatini katika tamthiliya teule ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo* zote za Emmanuel Mbogo.

## 2.3 Dhana ya Mwingilianomatini katika tamthiliya ya Kiswahili

Dhana ya mwingilianomatini katika fasihi ya Kiswahili, imejadiliwa na wataalam mbalimbali, miongoni mwao ni Wamitila (2002), Wamitila (2008), Senkoro (2011), Herman (2011) na Adam (2014). Wamitila (2008) anaiangalia dhana ya mwingilianomatini kwamba ni kuhusiana na kutegemeana kwa matini au kazi za kifasihi na matini au kazi za kifasihi zilizotangulia. Uhusiano huo huweza kutazamwa katika vipengele vya fani na maudhui.

Senkoro (2011) anaielezea mbinu ya mwingilianomatini kuwa, ni kule kutumiwa kwa utanzu mmoja wa fasihi katika kutolea au kuwasilishia utanzu mwingine, mfano wimbo ndani ya ngano au hadithi. Anaongezea hoja yake kwa kusema kuwa, pia ni ule uwepo wa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi fulani ya fasihi, mfano matumizi ya nyimbo, barua, ngoma, masimulizi ya hadithi, misemo na nahau.

Mtaalamu mwingine ni Herman (2011), ambaye anaielezea mbinu ya mwingilianomatini kama mtindo wa kuchanganya vipengele mbalimbali vya kisanaa katika kazi moja ya fasihi. Akifafanua zaidi anaeleza kuwa, mwandishi wa kazi ya fasihi hujikuta amechanganya matini za nyimbo, semi, hadithi, hadithi ndani ya

hadithi, maigizo na matumizi ya ishara katika kazi yake ya fasihi. Mtindo huo wa kuchanganya vipengele tofauti katika kazi moja ya fasihi ni kitu kilichozoeleka sana miongoni mwa wanafasihi.

Hoja hiyo inaungwa mkono na mtunzi mahiri wa tamthiliya, Profesa Emmanuel Mbogo, ambaye anaamini kuwa uchanganyaji wa matini mbalimbali katika kazi ya fasihi huleta uhai katika kazi husika. Haya yanathibitishwa na Adam (2014:168), anaporejelea mahojiano yake na Mbogo. Katika mahojiano hayo Mbogo anaeleza kuwa:

> "Tanzu za fasihi kwa hakika ni kitu kimoja ambacho hakitenganishiki kwa uhalisia, bali hufanyika hivyo kwa nia ya kujifunza tu. Haiwezekani mtunzi wa kazi fulani ya fasihi akatunga kazi yake bila kuchanganya tanzu mbalimbali katika huo utunzi wake. Ni nadra kukutana na kazi ya riwaya, hadithi, tamthiliya au ushairi ambayo itakuwa haina matumizi ya misemo na methali za aina mbalimbali na bado kazi hiyo ikaendelea kuitwa kuwa ni kazi ya kifasihi. Hii ndio huifanya kazi ya fasihi kuwa na uhai na ikikosa vitu hivi basi itakuwa mfu. Hivyo basi, uainishaji wa tanzu tunaoufanya sisi wanataaluma ni nyenzo ya kujifunzia tu lakini katika muktadha halisi mambo hayako hivyo kwa kuwa tanzu za fasihi zimechangamana sana".

Maelezo hayo yanaunga mkono mawazo ya wataalam waliojadili kuhusu dhana ya mbinu ya mwingilianomatini hapo juu na yanaendelea kutoa ufafanuzi kuhusu dhana hiyo katika utunzi wa kazi ya fasihi ya Kiswahili, ambapo tumeona kuwa msingi wake mkuu ni kuchanganywa kwa tanzu au matini mbalimbali katika kazi moja ya fasihi. Matini hizo ni pamoja na tamathali za semi, nyimbo, misemo, methali, nahau, ngoma, hotuba na ndoto, majigambo na mafumbo.

Kwa upande mwingine, tunapozungumzia utunzi wa mwandishi fulani mara nyingi tunarejelea dhana ya mtindo ambayo inahusika na upekee wa mwandishi. Senkoro (1982), anaelezea kuhusu mtindo katika kazi ya fasihi kuwa, ni ile namna ambayo

msanii hutunga kazi yake na kuipa sura ambayo kifani na kimaudhui huainisha kanuni au kaida zilizofuatwa kama ni zilizopo au ni za kipekee. Hii ina maana kuwa, ni jinsi mtunzi anavyokuwa na uwezo wa kuisana kazi yake na kuipa muonekano fulani kifani na kimaudhui ambao utamtofautisha na mtunzi mwingine. Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa, mtindo, ni jinsi msanii anavyotumia ufundi, umahiri na hisia zake katika kutenda au kueleza jambo fulani. Pia mtindo huweza kuhusisha matumizi ya barua, hotuba, nyimbo, shairi, usimulizi na matumizi ya nafsi, lugha ya kitaswira na ishara, methali, misemo, tamathali za semi na nahau. Hivyo waandishi wanapotumia mtindo au mbinu mbalimbali husababisha kuwe na utofauti kati ya kazi ya fasihi ya mtunzi mmoja na mwingine na vilevile kati ya kazi moja ya fasihi na nyingine hata kama zote zitakuwa ni za mtunzi huyohuyo mmoja.

Utafiti huu ulihusu kubainisha kufanana na kutofautiana kwa matumizi ya mbinu ya mwingilianomatini katika tamthiliya teule za mwandishi mmoja, zilizotungwa katika vipindi tofauti ili kuona mtunzi anavyofumbata matumizi ya mwingilianomatini katika kazi zake za fasihi, na jinsi matumizi ya mbinu hiyo yalivyosaidia katika uibuaji wa dhamira za tamthiliya hizo na kuwezesha uelewekaji wake kwa hadhira iliyokusudiwa. Tamthiliya zilizohusishwa katika utafiti huu ni *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo* zote za Emmanuel Mbogo.

Maelezo kuhusu dhana ya mbinu ya mwingilianomatini yamesaidia kuelewa utafiti huu umelenga kuchambua matini zipi zilizoingiliana katika tamthiliya teule na hivyo kuweza kuzibaini na kuelezea zilivyotumika na kuwezesha uibuaji wa dhamira za tamthiliya husika.

## 2.4 Utafiti linganishi katika Tamthiliya ya Kiswahili

Watafiti kadhaa wamefanya utafiti linganishi kuhusu tamthiliya ya Kiswahili. Baadhi ya tafiti hizo zimejikita katika kulinganisha na kulinganua vipengele vya fani na maudhui katika tamthiliya moja na nyingine au baadhi zimechambua dhima ya mtindo katika tamthiliya kwa kufanya utafiti linganishi. Kazi zilizojihusisha na ulinganishaji na ulinganuzi wa vipengele vya fani na maudhui katika tamthiliya ni pamoja na kazi ya Saleem (2013), na Mkuwili (2014), na kazi zilizojihusisha na ulinganishaji na ulinganuzi wa dhima ya mtindo katika tamthiliya ni pamoja na kazi ya Fadhili, (2014).

Saleem (2013), alifanya utafiti linganishi wa tamthiliya ya *Mashetani* na *Kivuli kinaishi*. Lengo la utafiti wake lilikuwa ni kulinganisha na kulinganua vipengele vya fani na maudhui katika tamthiliya hizo na hatimaye kubainisha sababu za mfanano na utofauti katika vipengele hivyo. Matokeo ya utafiti huo yalidhihirisha kuwa kufanana na kutofautiana kwa tamthiliya hizo kumetokana na tofauti katika mbinu za kimtindo walizozitumia waandishi katika kujenga kazi zao. Aidha, tofauti na utafiti wa Saleem ambaye alishughulikia ulinganishaji wa kazi za waandishi wawili tofauti, utafiti huu ulijikita katika kuchunguza na kulinganisha matini za msanii mmoja. Aidha, utafiti huu haukujikita katika kuchunguza fani na maudhui bali umechunguza matumizi ya mwingilianomatini katika kazi za fasihi za mtunzi mmoja jambo ambalo Saleem hakulishuhulikia kwa sababu halikuwa lengo la utafiti wake. Hata hivyo, utafiti huo ulikuwa na mchango mkubwa katika utafiti wetu kwa sababu umejadili pia kipengele cha mtindo ambacho kimegusia mbinu ya uchanganyaji wa matini na tanzu mbalimbali za fasihi katika tamthiliya, kipengele ambacho utafiti huu

haukuweza kukiepuka katika kubainisha mwingilianomatini katika tamtiliya za Emmanuel Mbogo. Hivyo utafiti huo ulisaidia na kuupa tafiti huu msingi wa kinadharia na vitendo katika utafiti linganishi wa matini za kifasihi. Hata hivyo utafiti wetu ni tofauti na utafiti huo kwa kuwa utafiti huu lengo lake ni kuchunguza mbinu ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo* ambazo ni za mwandishi mmoja zilizoandikwa katika vipindi tofauti.

Mkuwili (2014), alifanya utafiti linganishi kuhusu fani na maudhui katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Kivuli Kinaishi.* Lengo la utafiti wake lilikuwa ni kuchunguza jinsi waandishi wanaotoka katika maeneo tofauti ya kijiografia yaani pwani na bara wanavyofanana na kutofautiana kifani na kimaudhui. Kwa kuwa utafiti huo ni utafiti linganishi, ulitusaidia kubaini mbinu na nadharia ya fasihi linganishi katika kulinganisha kazi za fasihi. Hata hivyo, utafiti huo ni tofauti na utafiti huu katika malengo yake na sababu za utafiti wake, ambapo ulilenga kuchunguza kazi za wasanii wanaotoka katika mazingira tofauti ya kijiografia na kiutamaduni, wakati utafiti wetu unachunguza kazi za msanii mmoja, ambaye ana utamaduni na uzoefu wake katika historia ya maisha ya kisanii. Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kubaini jinsi msanii huyu anavyofumbata matumizi ya mbinu ya mwingilianomatini na endapo anabadilika katika utunzi wake ndani ya muongo mmoja ambao vitabu vinavyofanyiwa utafiti vimetofautiana.

Fadhili (2014), amefanya utafiti linganishi kuhusu dhima ya mtindo katika tamthiliya za kihistoria za *Morani (1993)* na *Kinjeketile (1969).* Katika utafiti wake amechunguza dhima ya vipengele vya kimtindo katika tamthiliya hizo ili kuona ni

jinsi gani wasanii wa tamthiliya hizo wanafanana na kutofautiana katika uteuzi wa vipengele vya kimtindo wanapowasilisha suala la kihistoria. Utafiti huo umegusia vipengele vya lugha ambavyo pia ni matini zilizoshughulikiwa na utafiti huu, hivyo utafiti huo ulikuwa ni wenye manufaa kwetu kwa kubaini matini mbalimbali za lugha zinavyotumika katika kazi za fasihi. Hata hivyo utafiti wetu ni tofauti na utafiti huo kwa kuwa utafiti wake haukujikita katika kuchunguza mwingilianomatini kwa sababu hayakuwa malengo ya utafiti wake. Kwa maana hiyo tafiti hizi ni tafiti mbili tofauti zenye malengo tofauti.

## 2.5 Pengo la Maarifa

Kama tulivyoona katika mjadala hapo juu, tafiti linganishi mbalimbali zimefanyika kuhusu vipengele vya fani na maudhui katika kazi mbalimbali za tamthiliya. Hata hivyo kwa upeo wa mtafiti wa utafiti huu, bado hatujapata uthibitisho wa kazi ya utafiti ambayo imechunguza kwa kutumia utafiti linganishi, mwingilianomatini katika utunzi wa tamthiliya za mwandishi mmoja zilizotungwa katika vipindi tofauti, ili kuona ni jinsi gani msanii huyo anaifumbata mbinu ya mwingilianomatini katika kazi zake za fasihi, na kubaini endapo kuna mabadiliko yoyote ya kiubunifu na jinsi mbinu hiyo ilivyotumika kuibua dhamira.

Hivyo basi, utafiti huu umejaribu kuziba pengo hilo kwa kutathmini mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo ili kuona ni jinsi gani msanii huyu anaifumbata mbinu ya mwingilianomatini katika kazi zake za fasihi. Kwa kufanya hivyo tutaweza kuibua kufanana na kutofautiana kwa matumizi ya mbinu ya mwingilianomatini katika kazi za msanii mmoja baada ya kipindi cha takribani

muongo mmoja. Vile vile tutaweza kubaini endapo kuna mabadiliko yoyote ya kiubunifu yanayojidhihirisha katika tamthiliya hizo. Kwa hiyo, utafiti huu ulifanya tathmini ya mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo, kwa kulinganisha na kulinganua tamthiliya za; *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988) na *Fumo Liongo* (2009

## 2.6 Kiunzi cha Nadharia

Dhana ya nadharia imeelezewa na watalaam kadhaa akiwemo Wamitila (2002), anayesema kuwa, nadharia ni kauli ya kaida za kiujumla zinazotegemezwa kwenye uwazaji fulani. Kauli au kaida hizi huweza kutumiwa kuelezea hali au halia fulani. Kutokana na maelezo ya wataalam hao inaonyesha kuwa, nadharia ndiyo msingi mkuu wa kuweza kuelezea jambo fulani ili liweze kukubalika, kuaminika na kufanyiwa kazi na watu wa jamii husika. Kutokana na uelewa huo wa nadharia, zipo nadharia mbalimbali za fasihi linganishi zinazoweza kutumika katika kuchunguza na kuchambua data za utafiti wa kazi za fasihi. Baadhi ya nadharia hizo ni Upokezi, Athari na Uigaji, Usambamba na mwingilianomatini. Hata hivyo, kufaa au kutofaa kwa nadharia moja hutegemea malengo ya utafiti. Katika sehemu ifuatayo tutajadili baadhi ya nadharia zinazohusiana na malengo ya utafiti wetu ili kuona ni nadharia ipi ni bora zaidi kulingana na malengo ya utafiti huu.

### 2.6.1 Nadharia ya Mwingilianomatini

Mwingilianomatini ni moja ya nadharia za fasihi ambayo hutumika katika kuchunguza na kuchambua data za utafiti linganishi wa kazi za fasihi. Kristeva (1980), Wamitila (2002), Njogu na Wafula (2007) na Ndumbaro (2013), wameelezea

kuhusu nadharia hii iliyoasisiwa na Mwanasemiotiki wa Kifaransa, Julia Kristeva (1960). Kristeva aliizua nadharia hii ya Mwingilianomatini kutokana na mawazo yaliyotokana na nadharia ya Usemezano ya Mrusi Mikhail Bakhtin (1895 – 1975). Bakhtin katika nadharia hiyo ya Usemezano, anaamini kuwa kazi ya fasihi ina sauti mbalimbali zinazoingiliana na kupiga mwangwi katika kazi nyingine zilizotangulia, zilizopo au zitakazokuja baadaye. Hii ina maana kuwa, athari ya kazi moja huweza kuonekana katika kazi nyingine zilizotangulia, zilizopo na hata zijazo.

Hivyo Kristeva aliyaendeleza na kuyatanua mawazo hayo ya Bakhtin na kuibua nadharia yake ya mwingilianomatini mnamo mwaka 1960. Mhimili mmojawapo wa nadharia hii ni kwamba, hakuna matini yoyote inayoweza kuangaliwa peke yake, kwa upekee wake na kwa kujitegemea, isipokuwa lazima kutakuwa na matini nyingine iliyotangulia ambayo inahusiana na matini hiyo mpya. Hii ina maana kuwa, kunauhusiano na kutegemeana kwa kazi za fasihi, na kwa maana hiyo, si rahisi kuzungumzia uasili au upekee wa kazi ya fasihi, kwani kwa vyovyote vile itakuwa inatokana na kazi za fasihi zilizotangulia au zilizopo.

Mhimili mwingine wa nadharia ya mwingilianomatini ni kuwa, matini zinaingiliana na kuchangizana, hivyo kuamini kuwa matini ya kifasihi inajitegemea ni kupotoka. Pamoja na hayo mwingilianomatini huhusisha pia mitindo fulani ya kiusemi na misimbo fulani ambayo imesaidia katika uashiriaji wa kazi za baadaye. Hivyo mwingilianomatini sio urejelezi wa kazi fulani katika kazi nyingine tu, bali pia ni ule uingiliano wa mitindo ya kiuashiriaji.

Kwa ujumla, Kristeva anaitazama dhana ya mwingilianomatini kama jumla ya maarifa na mbinu zinazoifanya matini kuwa na maana, ambapo maana ya matini huangaliwa kama inayoitegemea matini nyingine katika kile kinachoitwa "mwanda wa ki – mwingilianomatini". Kwa hiyo, kwa mujibu wa Kristeva, matini yoyote ile huchukua au kufaidi kutokana na matini nyingine pamoja na kuziumbua katika mwanda huo wa kimwingilianomatini.

Kwa kutalii nadharia ya mwingilianomatini na hata mhimili wa mawazo makuu ya nadharia hiyo tuliona kuwa inahusiana sana na malengo ya utafiti huu. Kama ambavyo malengo ya utafiti huu yamejadiliwa katika sura ya kwanza kipengele cha 1.3, nadharia hii ilionekana inafaa kukidhi malengo hayo na inaweza kutusaidia katika kuchunguza, kuchambua na kujadili data za matokeo ya utafiti huu na hata kufikia hitimisho la matokeo ya utafiti huu.

Kulingana na malengo ya utafiti huu tuliona kwamba nadharia inayotufaa zaidi ni nadharia ya Mwingilianomatini. Katika utafiti huu tuliamua kutumia nadharia ya Mwingilianomatini ili kuchunguza na kubainisha matumizi ya mbinu ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Sababu ya kuchagua nadharia hii tofauti na nadharia zingine tulizozijadili, ni kutokana na kuona kuwa misingi yake inahusiana sana na malengo ya utafiti wetu. Vilevile tuliona kuwa, misingi ya nadharia hii itatuongoza katika kubaini na kuchambua mbinu ya mwingilianomatini katika tamthiliya teule na kutusaidia katika ulinganishaji na ulinganuzi wa tamthiliya hizo katika utumizi wa mbinu ya mwingilianomatini.

### 2.6.2 Jinsi Nadharia ya Mwingilianomatini Ilivyotumika katika Utafiti

Kama tulivyobainisha hapo juu kuwa nadharia iliyotumika kuchunguza, kuchambua na kujadili data za utafiti huu ni nadharia ya mwingilianomatini. Utafiti huu uliitumia nadharia hii katika kukidhi lengo namba moja na kujibu swali la kwanza la utafiti huu kwa kubainisha matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Kwa kutumia nadharia hii, tuliweza kubainisha mbinu mbalimbali ambazo ni matokeo ya mwingilianomatini kama vile; ngoma, nyimbo, majigambo, utendi, ushairi, hadithi, nguvu za sihiri na wahusika wa fasihi simulizi. Vilevile mawazo ya nadharia hii yalituongoza katika kulinganisha na kulinganua matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya teule za utafiti huu. Kwa kufanya hivi tuliweza kuonesha ni namna gani mwingilianomatini unajitokeza katika kazi moja na kazi nyingine na hata kuonyesha kuhusiana kwa kazi hizo na matini zilizotangulia kama vile mapokeo simulizi ya Kiafrika. Nadharia hii pia ilitusaidia kubaini maana na dhamira zilizojiegemeza katika mbinu za mwingilianomatini, zilizobainishwa katika matini hizo. Mhimili mkuu wa nadharia ya mwingilianomatini ulituongoza katika kutoa majumuisho ya mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo na kutoa hitimisho la usanii wake.

## 2.7 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili kuhusu mapitio ya maandiko mbalimbali kuhusu Fasihi Linganishi, mwingilianomatini na tafiti mbalimbali zilizofanywa kuhusu ulinganishaji wa kazi za tamthiliya na mwingilianomatini. Aidha katika mijadala hiyo, tumeweza kubaini pengo la kimaarifa na kuonyesha hitaji lililopelekea umuhimu wa kufanyika kwa utafiti huu. Vile vile sura hii imejadili kiunzi cha

nadharia kwa kutalii nadharia ambazo zilionekana zinaweza kuongoza utafiti huu. Katika mjadala wa kiunzi cha nadharia, utafiti huu umejadili mihimili ya nadharia hizo, ubora na upungufu wake katika kuchunguza, kuchambua na kujadili data za utafiti huu. Aidha, kwa kufanya hivyo utafiti huu uliweza kuchagua nadharia ya mwingilianomatini na kuonyesha uthabiti wa nadharia hiyo, sababu za kuichagua na namna ilivyotumika katika utafiti huu. Sura inayofuata itajadili kuhusu mbinu za utafiti zilizotumika katika kufikia malengo ya utafiti huu.

# SURA YA TATU

## 3.0 MBINU ZA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi

Sura hii inajadili mikabala, mbinu na vifaa vilivyotumika katika utafiti huu. Kwa ujumla utafiti huu umetumia mkabala usio wa kitakwimu katika kukusanya, kuzichambua, kuziwasilisha na kuzijadili data za utafiti huu. Jilala (2014: 89) akimnukuu Spicer (2012) anasema utafiti wa kitakwimu na usio wa kitakwimu hujazilizana na kukamilishana (taz. pia Creswel, 2009; Silverman, 2010). Kwa hiyo, utafiti huu ulihusisha nduni za utafiti usio wa kitakwimu katika misingi ya ukamilishano na ujazilizano. Kwa ujumla, sura hii inajadili yafuatayo: eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, mbinu za ukusanyaji data, uchambuzi wa data na hitimisho

.

### 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika jiji la Dar es Salaam. Utafiti huu ulikuwa ni utafiti wa maktabani na uwandani ambapo ulifanyika katika maktaba mbalimbali jijini Dar es Salaam ikiwemo maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (East Africana), maktaba ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) na maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Sababu ya kuchagua maeneo hayo ni kwamba utafiti huu ulilenga kupata na kusoma maandiko mbalimbali yaliyohusiana na utafiti, hivyo katika maktaba hizo ndiko kulikopatikana machapisho mbalimbali ambayo yalitupatia data za msingi na data za upili za utafiti huu. Katika maktaba hizo, mtafiti alisoma kazi tangulizi mbalimbali kama vile majarida, makala, tasnifu na vitabu vinavyohusiana na mada ya utafiti huu. Pamoja na kupata machapisho kutoka katika

maktaba hizo mtafiti alipitia pia tovuti mbalimbali zenye machapisho yanayohusiana na mada ya utafiti. Hivyo chaguo la eneo la utafiti huu lilitokana na upatikanaji wa nyaraka mbalimbali zilizomwezesha mtafiti kufikia malengo ya utafiti wake. Vilevile kwa kutumia maktaba na utulivu wa mazingira ya maktaba, mtafiti alipata nafasi ya kusoma matini za tamthiliya teule ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo,*

Aidha, sababu nyingine ya kuchagua Dar es salaam ni kwamba, ndilo eneo analoishi msanii Emmanuel Mbogo ambaye ndiye mtunzi wa tamthiliya lengwa za utafiti huu. Kwa vile utafiti huu ulikusudia kufanya usaili na msanii huyo kuhusu utunzi wake, eneo hili lilionekana ni muhimu katika utafiti huu. Kwa hiyo, ilikuwa rahisi kupata data zinazohusiana na mwingilianomatini katika usanii wa mtunzi huyo kwa kufanya nae usaili kuhusu utunzi wake na mwingilianomatini (tazama maswali ya mwongozo wa usaili). Vilevile Dar es salaam ni eneo ambalo kuna vyuo vikuu vinavyofundisha kozi za fasihi, Fasihi Linganishi na tamthiliya ya Kiswahili. Kwa hiyo, ilikuwa rahisi kuwapata wanafunzi wa chuo kikuu wanaosoma fasihi ya Kiswahili hususani tamthiliya. Hawa walilengwa wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam, wanaosomea shahada ya umahiri katika Kiswahili (BA.Kiswahili). Kundi hili lilihusishwa katika majadiliano ya vikundi ili kupata data zinazokidhi malengo ya utafiti huu.

### 3.3 Kundi lengwa

Kwa mujibu wa Spata (2003), na Komba na Tromp (2006), sampuli ni jumla ya wanachama wote, mtu mmoja, kikundi au elementi wakiwemo wanyama, vitu na matukio ambayo mtafiti amekusudia kuyahusisha katika kukusanya data za utafiti

wake. Vilevile kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao mtafiti amewakusudia na ambao kutoka kwao atapata taarifa anazozihitaji katika utafiti wake (Kombo na Tromp 2006; Enon 1998). Kwa hiyo, walengwa wa utafiti walikuwa ni; mtunzi wa tamthiliya ya *Ng'wanamalundi (1988)* na *Fumo Liongo* (2009) Emmanuel. Mbogo, huyu aliteuliwa kwa sababu ndiye mtunzi wa tamthiliya hizo. Uteuzi wa msanii huyu ulifanyika kwa kuamini kuwa kwa kumtumia mtunzi wa tamthiliya hizo tunaweza kupata data za kutosha kuhusu mwingilianomatini katika kazi zake na ni kazi zipi za sanaa ambazo zimemuathiri katika utunzi huo. Kwa hiyo, tulitegemea kupata data na usuli wa utunzi wake. Walengwa wengine ni kundi la wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanaosoma programu ya Fasihi ya Kiswahili (BA.Kiswahili). Kundi hili liliteuliwa kwa sababu tuliamini kuwa, ni kundi ambalo linasoma kozi ya tamthiliya ya Kiswahili na kwa maana hiyo wamesoma na kufanya uchambuzi wa tamthiliya za Emmanuel Mbogo, zikiwemo tamthiliya teule za utafiti huu. Kwa hiyo, tuliamini kuwa kundi hili lina msingi wa nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi na kwa kutumia kundi hili tungeweza kupata data za kutosha.

### 3.4 Usampulishaji na Mbinu za usampulishaji

Enon (1998), Spata (2003), Bryman (2004) na Walliman (2011), wanaeleza kuwa usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu kutoka kundi lengwa ili litumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa kwa kuwa sio rahisi kutafiti kundi lengwa zima. Zipo mbinu mbalimbali ambazo hutumiwa katika uteuzi wa sampuli, lakini sampuli ya utafifi huu imetumia mbinu mbili ambazo ni mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalum na mbinu ya uteuzi rahisi.

### 3.4.1 Mbinu ya Uteuzi wa Madhumuni Maalum

Uteuzi wa sampuli kwa kutumia kigezo cha madhumuni maalumu ni uteuzi wa sampuli kwa kuzingatia sababu mahususi. Katika mbinu hii ya uteuzi wenye madhumuni maalum, sampuli huteuliwa kwa kuzingatia vigezo maalum ambavyo vitakuwa na uhusiano na maswali ya utafiti ili yaweze kujibiwa kwa urahisi na ukamilifu (Powell na Conway, 2004). Kombo na Tromp (2006), wanasema, ni uteuzi ambao mtafiti kwa makusudi hulenga kuteua kundi la watu ambao anaamini kuwa ni raslimali anayoitegemea katika utafiti wake. Mbinu hii humpa mtafiti uhuru katika kuteua sampuli itakayowezesha kujibu maswali ya utafiti (Neuman, 2006).

Mbinu ya uteuzi wenye madhumuni maalumu ilitumika kuteua tamthiliya za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo* miongoni mwa tamthiliya nyingi zilizotungwa na Emmanuel Mbogo. Tamthiliya hizo teule ziliteuliwa hasa kutokana na uelewa wa awali wa mtafiti kwamba, ni tamthiliya zilizotungwa kwa muachano wa takriban muongo mmoja, hivyo kutokana na malengo ya utafiti huu, zilionekana kukidhi mahitaji na kuwa na sifa ya kuteuliwa. Kimsingi tamthiliya hizo zimesaidia kujibu maswali ya utafiti na hivyo kutimiza malengo ya utafiti huu.

Halikadhalika, mbinu hii ilitumika kumteua mtafitiwa wa utafiti huu, Profesa Emmanuel Mbogo. Lengo lilikuwa kupata data kuhusu matumizi ya mwingiliano matini. Kwa hiyo mtunzi wa tamthiliya hizo alikuwa na umuhimu katika utafiti huu kwa maana hiyo mbinu hii ilitumika kumteua kwa kuzingatia kigezo kuwa yeye ndiye mtunzi wa kazi hizo. Sababu za kutumia mbinu hii ni malengo ya utafiti na uelewa wa awali alionao mtafiti kuhusu mtunzi wa tamthiliya hizo.

Sababu nyingine ambayo ilimfanya mtafiti kutumia mbinu hii ni kwamba, mtafiti alikuwa na taarifa juu ya kuwepo kwa makundi yenye ujuzi, maarifa na uzoefu katika uhakiki na uchambuzi wa Fasihi ya Kiswahili hususani tamthiliya ya Kiswahili. Makundi haya ndiyo yaliyoonekana kuwa raslimali ya data za utafiti huu. Kwa hiyo, kwa kuzingatia ufahamu huo, mbinu hii ilitumika kuwateua wanafunzi wa chuo kikuu cha Dar es salaam wanaosoma program ya Fasihi ya Kiswahili. Uteuzi huu pia ulitegemea taarifa za awali alizozipata mtafiti kuwa kozi ya nadharia ya uchambuzi na uhakiki wa kazi za fasihi inafundishwa kwa wanachuo hao, wanachuo hao, walichaguliwa kwa kigezo kwamba tayari walikuwa wamesoma nadharia za uchambuzi na uhakiki wa kazi za fasihi hususani tamthiliya ya Kiswahili. Kwa kutumia kundi hili, utafiti huu uliweza kupata data za kutosha wakati wa majadiliano ya vikundi na wanachuo hao.

Kwa ujumla mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalumu ilimsaidia mtafiti kupata sampuli ya watu wenye uzoefu, stadi na maarifa katika nadharia na uhakiki wa fasihi na tamthiliya ya Kiswahili. Mbinu hii pia ilisaidia kupata data ambazo zimekuwa ni mhimili wa utafiti huu. Vile vile data zilizopatikana kwa makundi hayo zilimsaidia mtafiti kupata na kufanya majumuisho mahususi kulingana na malengo ya utafiti.

### 3.4.2 Mbinu ya Uteuzi Rahisi

Kothari (2013) anaelezea mbinu ya uteuzi rahisi kuwa, ni mbinu inayotumika kuteua sampuli ya wahojiwa miongoni mwa kundi kubwa la wahojiwa wenye sifa sawa. Sampuli katika mbinu hii, huteuliwa kuwakilisha kundi kubwa bila kujali sifa ya mteuliwa kwani kila mmoja katika kundi hilo huwa na sifa sawa na mwingine.

Kutokana na walengwa wote kuwa na sifa sawa au zinazofanana, yaani kuwa ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanaosoma Fasihi ya Kiswahili, mtafiti aliamua kuteua sampuli kwa kuchukua orodha ya majina ya wanafunzi hao. Kwa kutumia orodha hiyo, mtafiti aliteua sampuli yake kwa kutumia nafasi kila baada ya mtu wa pili, mtafiti aliteua jina la mtu ambaye alilengwa kushiriki kama sampuli yake. Alifanya hivi kwa majina ya kike na ya kiume na hivyo kuwa na idadi ya wahojiwa ishirini; kumi wanawake na kumi wanaume. Uteuzi wa kundi hili ulizingatia jinsia kwa sababu utafiti huu uliamini kuwa watu wa jinsi tofauti wanaweza kutoa maoni na mtazamo tofauti hususani pale panapokuwa na data za ujinsia. Kundi hili litasaidia kubainisha mbinu ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo* na kubaini kufanana na kutofautiana kwa tamthiliya hizo.

### 3.5 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Ukusanyaji wa data katika utafiti huu ulifanywa kwa kutumia mbinu tatu ambazo ni mbinu ya Mapitio ya Maandiko, Usaili, na Majadiliano ya Vikundi.

#### 3.5.1 Mbinu ya Mapitio ya Maandiko

Jilala (2014) anasema mbinu hii huhusisha uchambuzi wa maudhui yaliyomo katika nyaraka kama vile vitabu, magazeti na maudhui ya maneno ambayo yanaweza kuwa ya maandishi au mazungumzo. Mbinu hii iliambatana na usomaji na uchambuzi wa matini za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Mchakato huu ulifanyika ili kupata data zinazohusiana na mwingilianomatini. Vilevile, mbinu hii ilihusisha

usomaji, uchambuzi na uchunguzi wa data katika vitabu na majarida yanayohusiana na mada ya utafiti huu, kama vipeperushi, taarifa za kwenye mtandao na makavazi.

Hivyo mtafiti aliweza kupitia maandiko na kukusanya data za msingi kutoka katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo* zote za Emmanuel Mbogo. Mtafiti alipata data za mbinu ya mwingilianomatini kwa kusoma tamthiliya zote kwa umakini mkubwa, huku akiwa na hadidu za rejea zilizomuongoza kujua vipengele anavyopaswa kuvimakinikia wakati wa usomaji wake. Data kuhusu mbinu ya mwingilianomatini zilinukuliwa katika shajara kwa ajili ya kuchambuliwa kulingana na maswali ya utafiti ili kutimiza malengo ya utafiti huu.

Halikadhalika, data za upili za utafiti huu zilipatikana kwa mtafiti kupitia maandiko yanayohusiana na utafiti huu, kutoka katika maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, maktaba ya East Africana ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na maktaba ya Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili (TATAKI) na makavazi yake na pia katika tovuti na wavuti mbalimbali. Data hizi zilikusanywa kwa lengo la kukamilisha data za msingi ili ziweze kujibu maswali ya utafiti na kukamilisha malengo ya utafiti huu.

Kwa ujumla mbinu hii ilitusaidia kupata data za kutosha kuhusu mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo. Pamoja na kuwa tuliweza kukusanya data kwa kutumia mbinu hii lakini baadhi ya vipengele katika data hizo vilihitaji ufafanuzi na maelezo ya ziada. Kwa hiyo ilionekana kwamba, kwa kutumia mbinu hii peke yake hatuwezi kufikia malengo ya utafiti huu. Hivyo basi, ili kutimiza malengo ya utafiti huu tuliona kuna hitaji la kutumia mbinu nyingine itakayotusaidia kupata maelezo ya

ziada ili kujaziliza data tulizozipata wakati wa uchambuzi wa matini husika. Mbinu ambayo itatusaidia kuibua maoni, uzoefu, maarifa, mawazo na mtazamo wa mtunzi wa tamthiliya hizo. Kwa hiyo, utafiti huu uliamua kutumia mbinu ya usaili ili kujibu maswali ambayo msanii alijiuliza katika ukusanyaji wa data kwenye matini. Sehemu inayofuata inajadili kwa kina zaidi kuhusu mbinu ya usaili na namna ilivyotumika katika utafiti huu.

### 3.5.2 Mbinu ya Usaili

Usaili ni mbinu ya kukusanyia data ambayo huhusisha mahojiano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na mtafitiwa (Kothari, (2013). Katika utafiti huu, mbinu hii ilitumika kumhoji mtunzi wa tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo* Profesa Emmanuel Mbogo ili kuweza kupata data zaidi zilizowezesha maswali ya utafiti kujibiwa na hivyo kukamilisha malengo ya utafiti huu. Mtafiti aliandaa maswali kadhaa ambayo yalimwongoza katika kufanya usaili. Uteuzi wa kutumia mbinu hii katika utafiti huu ulitokana na sababu kwamba, ni mbinu ambayo itatusaidia kupata maelezo ya ziada na ufafanuzi wa ziada kuhusu matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya teule. Hii ilitokana na ukweli kuwa, mbinu hii inatoa uhuru kwa mtafitiwa kujieleza kwa mapana zaidi na vilevile inaruhusu kufafanua yale yasiyoeleweka vema kwa watafitiwa na kuweza kurekebisha majibu kwa kadri ya uhitaji wa mtafiti. Kupitia mbinu hii tulipata kubaini baadhi ya matini zilizotumika katika tamthiliya za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo,* sababu za kutumika kwa mbinu ya mwingilianomatini na baadhi ya matini zilizotumika katika tamthiliya hizo na msingi wa utunzi wa tamthiliya hizo.

Hata hivyo, pamoja na kuwa mbinu hii ilitumika kujaziliza data zilizopatikana katika mbinu ya usomaji wa machapisho tuliona kuwa bado tulihitaji kupata data zaidi kwa kuwahusisha wasomaji na wachambuzi wa matini za tamthiliya za Emmanuel Mbogo. Kwa hiyo, mbinu iliyoonekana kufaa ni mbinu ya majadiliano ya vikundi ambayo tuliamini kupitia mijadala hiyo tunaweza kupata data za kutosha kwa sababu mbinu hiyo humpa uwezo mtafitiwa wa kujadili na kujieleza kuhusu kile kinachojadiliwa. Kwa hiyo sehemu ifuatayo inajadili kwa kina kuhusu mbinu ya majadiliano ya vikundi na jinsi ilivyotumika katika utafiti huu.

### 3.5.3 Mbinu ya Majadiliano ya Vikundi

Mbinu hii ni mbinu ambayo mwongozo wa majadiliano yanafanywa baina ya kundi la watu kati ya sita hadi kumi ambao huwa na sifa na uzoefu unaofanana (Girbich, 1999). Jilala (2008) anasema kuwa majadiliano ya vikundi chini ya msimamizi mmoja yanaongozwa kiasi kwamba ingawa washiriki wanahamasishwa kuwa huru katika majadiliano lakini lazima kuwepo na mambo ya msingi yanayojadiliwa. Kwa hiyo, msimamizi wa majadiliano hujikita katika mambo mahususi. Mbinu hii ni bora kwa sababu inampa mtafiti taarifa nyingi haraka na kwa muda mfupi. Vile vile ni mbinu muafaka katika kuibua imani, mawazo, maoni na mtazamo ndani ya jamii. Aidha, kwa kutumia mbinu hii wahojiwa katika makundi yao huweza kubadilishana uzoefu kuhusu jambo hilo. Kwa hiyo, sababu ya kutumia mbinu hii ni kwamba tuliamini kuwa ni mbinu ambayo inaweza kutupatia data nyingi kwa muda mfupi. Aidha, kupitia majadiliano ya wahojiwa tutaweza kupata data za kutosha ili kukidhi malengo ya utafiti wetu.

Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi, tuliwagawa wanachuo wanaosoma kozi ya Fasihi ya Kiswahili katika makundi ya wanafunzi watano kwa kila kundi. Mjadala wa makundi hayo ulifanyika kwa siku mbili ambapo kila siku kulikuwa na mjadala wa makundi mawili ambayo yalifanya mjadala kwa muda tofauti. Kwa kila kundi mtafiti alifanya majadiliano ya dakika thelathini hadi dakika arobaini. Katika majadiliano hayo mtafiti alilenga kupata maoni, mitazamo na mielekeo juu ya matumizi ya mbinu ya mwingilianomatini katika tamthiliya za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Kwa ujumla mbinu hii ilitusaidia kupata data kama ambavyo tulikusudia katika utafiti huu.

## 3.6 Zana za Utafiti

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia zana zifuatazo:

### 3.6.1 Shajara

Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI (2013), shajara ni kitabu cha kuwekea kumbukumbu za kila siku. Zana hii ilitumika kuhifadhi kumbukumbu za data zilizopatikana katika utafiti huu. Kwa kutumia zana hii, mtafiti aliandika katika shajara taarifa mbalimbali zilizopatikana wakati wa utafiti.

### 3.6.2 Kompyuta

Kompyuta ni zana ambayo mtafiti aliitumia tangu mwanzo hadi mwisho wa utafiti wake. Kompyuta ni mashine ya kielektroniki inayotumika kuhifadhi na kusarifu taarifa zinazoingizwa ndani yake (BAKIZA, 2010). Mtafiti aliitumia zana hii kuchapa kazi yake ya utafiti, kuhifadhi data, kutafuta machapisho na maandiko mbalimbali yahusuyo utafiti huu yanayopatikana katika tovuti na wavuti mbalimbali.

### 3.6.3 Simu ya Mkononi

Simu ni chombo kinachopokea na kupeleka taarifa sehemu mbalimbali kutokana na mitambo yake ilivyosukwa kitaalamu. Pia simu hutumika kurekodi mazungumzo, kuandika ujumbe, kupiga picha na kufanya kazi nyingine mbalimbali hata za mahesabu. Katika utafiti huu, simu ilitumika kuwasiana na wahojiwa ili kuweka miadi ya muda wa kukutana, muda wa usaili na kufanya usaili. Pia wakati wa usaili na majadiliano ya vikundi simu ilitumika kurekodi data kupiga picha na mtunzi wa tamthiliya lengwa (tazama kiambatisho namba 3).

## 3.7 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data kwa mujibu wa Kothari (2013), ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo itasaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Wakiunga mkono hoja hii Bagdan na Biklen (1992), wakinukuliwa na Omari (2011), wanaeleza kuwa, hii ni hatua muhimu sana katika kutafuta majibu ya tatizo la utafiti husika. Zipo mbinu mbalimbali za uchambuzi wa data lakini data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya Uchambuzi maudhui.

Kombo na Tromp (2006), wanaeleza kuwa mbinu ya uchambuzi maudhui ni mbinu ambayo huziweka mada kulingana na jinsi zinavyofanana na kuhusiana. Dhana kuu au dhamira kuu hubainishwa na kuwekwa pamoja. Utafiti huu uliitumia mbinu hii kuzisoma tamthiliya za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *FumoLiongo* kwa lengo la kupata uelewa na kubainisha matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya hizo. Sababu ya kuitumia mbinu hii ni kwamba, mbinu hii ni mbinu ambayo imekuwa ikitumiwa na watafiti wengi wa kazi za fasihi na hata tafiti nyingi za sayansi ya jamii

hutumia mbinu hii. Aidha, tuliamini kuwa mbinu hii itatuwezesha kuzibaini na kuzitenga data zinazohusiana katika kundi moja na kusaidia uchambuzi na mjadala wa data hizo.

Wakati wa kukusanya data za utafiti huu, mtafiti aliandaa daftari au shajara maalum kwa ajili ya kudondoa data za utafiti kwa kusoma maandiko na kubaini vipengele vinavyodhihirisha mwingilianomatini. Kwa kutumia mbinu ya uchambuzi, maudhui mtafiti aliweka na kuzipanga katika kundi moja data zilizofanana na kuhusiana. Kwa kufanya hivi, ilisaidia kuchambua na kujadili data za utafiti kulingana na malengo mahususi na maswali ya utafiti. Vile vile ilisaidia kurahisisha zoezi la ulinganishaji na ulinganuzi. Mbinu hii ilionekana kufaa zaidi katika kuchambua data za utafiti na kurahisisha uelewekaji wake kwa msomaji kwani iliwezesha kuzipanga na kuzilinganisha na kuzilinganua data hizo na hivyo kuleta maana kwa data hizo ili kuwezesha mawazo ya jumla kubainika kulingana na malengo ya utafiti.

Vile vile utafiti huu umetumia majedwali katika kuwasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti huu.

## 3.8 Hitimisho

Sura hii imejadili kuhusu mbinu za utafiti. Katika sura hii imejadiliwa kuwa eneo la utafiti lilikuwa ni jiji la Dar es salaam, wakati walengwa wa utafiti huu ni msanii na mtunzi wa tamthiliya lengwa za utafiti huu na wanafunzi wa fasihi ya Kiswahili hususani tamthiliya wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Mbinu za usampulishaji zilizotumika ni mbili yaani; mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalum na mbinu ya

uteuzi rahisi. Sura hii pia imebainisha na kujadili mbinu zilizotumika kukusanya data za utafiti huu ambazo ni; mbinu ya mapitio ya machapisho, usaili na majadiliano ya vikundi. Aidha mbinu iliyotumika kuchambua data za utafiti huu ni mbinu ya uchambuzi maudhui. Baada ya kujadili mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu, sura inayofuata inawasilisha, kuchambua na kujadili data na matokeo ya utafiti huu.

# SURA YA NNE

# 4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha, kuchambua na kujadili data kutoka katika vyanzo mbalimbali vya data zinazohusu utafiti huu. Sehemu ya kwanza imeelezea usuli wa mtunzi, sehemu ya pili imewasilisha mihtasari ya tamthiliya teule na sehemu ya tatu hadi ya tano inawasilisha, kuchambua na kutoa matokeo ya data za utafiti huu.

### 4.1.1 Emmanuel Mbogo ni Nani?

Profesa Emmanuel Yakobo Mbogo ni mtunzi na mwandishi wa tamthiliya za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Ni msomi na Profesa wa sanaa za maonyesho na Fasihi ya Kiswahili. Wakati wa usaili na msanii huyu, tuliweza kupata usuli wa maisha yake na utunzi kwa ujumla. Kutokana na maelezo yake, Emmanuel Mbogo alizaliwa tarehe 01/03/1947 katika wilaya ya Kongwa, mkoa wa Dodoma. Alisoma katika shule ya msingi Mpwapwa na kuhitimu darasa la nane mwaka 1963. Baadaye alijiunga na masomo ya sekondari katika shule ya sekondari Indian (kwa sasa inajulikana kama Shule ya Sekondari Dodoma) na kuhitimu mwaka 1967. Wakati akisubiri matokeo yake, ya mtihani wa Sekondari alifanya kazi ya ukarani katika Wizara ya Kilimo, mkoani Dodoma. Baada ya kufaulu mwaka 1968, alijiunga na Chuo cha Ualimu Morogoro kwa ajili ya mafunzo ya Ualimu daraja la IIIA na kuhitimu mwaka 1969. Akiwa chuoni hapo, ndipo alipogundua kipaji chake cha uandishi. Hii ni baada ya kuandika hadithi aliyoiita *James I Die of Love* (1968) katika jarida la chuo lililokuwa linaitwa *Morani*, hadithi hiyo iliwavutia wasomaji na kusifiwa sana na mwalimu wake wa Fasihi ya Kiingereza na wanachuo wenzake.

Hadithi hii ndiyo iliyomtanabaishia uwezo wake wa kutunga hadithi na kumpa hamasa na ari ya kuingia katika ulimwengu wa sanaa na utunzi.

Mwaka 1970, alipangiwa kufundisha katika shule ya msingi Mwitikira iliyopo mkoani Dodoma. Akiwa anaendelea kufanya kazi, alijiunga na Chuo cha Rapid Results College kilichopo nchini London kwa mfumo wa elimu masafa, na kusomea masomo ya Kiswahili na Jiografia kwa lengo la kuongeza alama zitakazomwezesha kujiunga na masomo ya stashahada. Wakati huohuo akiwa katika shule hiyo, alitunga tamthiliya yake ya kwanza aliyoiita *Mama Tamasha* (1970). Mwaka 1971 alihamia katika shule ya msingi Nara. Akiwa katika shule ya msingi Nara, aliufanyia mazoezi mchezo huo na wanafunzi wake darasani, lengo likiwa ni kusikiliza namna unavyosikika katika mazungumzo na vitendo. Mchezo huo uliigizwa mwaka 1972 alipokuwa akifundisha shule ya Msingi Bwigiri. Wakati huo yeye na kundi lake la waigizaji ambao ni wanafunzi wake, walitembea na kuigiza mchezo huo katika vijiji na shule mbalimbali kwa kutumia usafiri wa magari yaliyokuwa yanahamishia watu kwenye kijiji vya ujamaa. Mchezo huu aliubadili jina na kuuita *Watoto Wetu* (1972).

Mwaka 1973 alijiunga na masomo ya stashahada ya ualimu na sanaa za maonyesho katika Chuo cha Ualimu Chang'ombe, kilichopo jijini Dar es Salaam na kuhitimu mwaka 1974. Baada ya kumaliza mafunzo ya stashahada, alipangwa kufundisha katika Chuo cha Ualimu Katoke, ambapo alifundisha hadi Juni 1976, alipojiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kusomea shahada ya kwanza na ya pili katika Sanaa za Maonyesho (B.A in Theatre Arts na M.A in Theatre Arts). Akiwa chuoni hapo, alitunga tamthiliya yake ya pili iliyoitwa *Tone la Mwisho* (1981). Akiwa bado

mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam alitunga tamthiliya nyingine iliyoitwa *Giza Limeingia* (1977), ambayo ilivutia na kuonyesha uwezo na kipaji chake. Yeye ndiye alikuwa mwongozaji wa tamthiliya hiyo iliyoigizwa katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Mbogo, alihitimu masomo yake ya shahada ya Sanaa za maonyesho mwaka 1981. Mwaka 1982 alijiunga na Chuo Kikuu cha Humboldt kilichopo mjini Berlin nchini Ujerumani, kwa masomo ya shahada ya tatu katika sanaa za Maonyesho (PhD in Theatre Arts) na kuhitimu mwaka 1984.

Baada ya kumaliza masomo yake alirudi nchini Tanzania na kufanya kazi katika Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), ambayo kwa sasa inatambulika kama Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI), iliyopo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hadi mwaka 1989. Mwaka 1990, alikwenda nchini Kenya na kufundisha katika Chuo Kikuu cha Moi hadi mwaka 1991. Mwaka 1992 alihama na kwenda kufundisha katika Chuo Kikuu cha Maseno kilichopo Kisumu hadi mwaka 2002, kisha mwaka 2003 alihamia Chuo Kikuu cha Kenyata ambapo alifundisha hadi mwaka 2006. Baada ya hapo mwaka 2007 alikwenda nchini Rwanda na kufundisha katika Chuo Kikuu cha Kigali kwa muda wa mwaka mmoja. Mwaka 2008 alirudi nchini Tanzania na kujiunga na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, ambapo yupo hadi sasa akiwa ni mhadhiri chuoni hapo.

Mtunzi ameshatunga vitabu kadhaa vya riwaya na tamthiliya. Tamthiliya alizokwishatunga na kuzichapisha ni *Watoto Wetu (1972), Giza Limeingia (1980), Tone la Mwisho (1981), Ngoma ya Ng'wanamalundi (1988)*, *Morani (1993), Fumo Liongo (2009), Sundiata (2011), Sadaka ya John Okelo (2014) na Nyerere na safari*

*ya Kanaani (2015).* Vilevile ametunga tamthiliya iitwayo *Tunuafrika-Wangari Maasai (haijatoka)* Pamoja na tamthiliya hizo, ametunga pia riwaya kama vile *Watoto wa Mama Ntilie* (2002), *Vipuli vya Figo* (2008) na *Siri ya Maisha* (2010). Katika utafiti huu tulichagua tamthiliya zake mbili za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo* kama ilivyojadiliwa katika sura zilizotangulia. Kwa hiyo mjadala wetu utajikita katika tamthiliya hizo mbili.

### 4.1.2 Muhtasari wa Tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*

Utafiti huu ulibaini kuwa *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ni tamthiliya inayozumguzia masuala ya matabaka katika jamii, hasa juu ya unyonywaji na unyanyaswaji wa wananchi unaofanywa na tabaka tawala (Chidama ambaye ni mchawi) dhidi ya tabaka tawaliwa (Vizuu). Msanii anatumia dhana tatu katika kurejelea uchawi na uganga. Dhana hizi ni dhana ya 'uchawi', 'vizuu' na 'uganga' kurejelea mbinu ya ukombozi. Dhana ya uchawi inarejelea tabaka tawala, vizuu linarejelea tabaka tawaliwa na uganga ni ukombozi. Kwa kutumia dhana hizo msanii anaonyesha jinsi tabaka tawala linavyowanyonya, kuwanyanyasa, kuwakandamiza na kuwadhulumu wananchi wakati huo huo wakijilimbikizia mali kutokana na jasho la wanyonge. Hata hivyo, mtunzi anaonesha jinsi harakati za ukombozi zinavyofanyika kwa kufanya mapinduzi dhidi ya unyonyaji, ukandamizaji na dhuluma ya tabaka tawala. Mwandishi anahitimisha kwa kuonesha daima uovu huangushwa na nguvu ya umma katika kujikomboa.

Kwa kutumia mbinu ya mapitio ya maandiko na majadiliano ya vikundi utafiti huu ulibaini kuwa msanii ametumia sitiari ya ngoma. Ngoma hizo zipo za aina tatu, yaani

ngoma ya Chidama, ngoma ya Ng'wanamalundi na ngoma ya harusi. Kila ngoma imetumika kisitiari kurejelea maisha ndani ya jamii. Kwa mfano ngoma ya Chidama, inahusisha taasisi ya uchawi na misukule[1], inarejelea mbinu za ukandamizaji na unyonyaji unaofanywa na tabaka tawala. Ngoma ya Ng'wanamalundi, ambayo inahusisha uganga wa mganga maarufu aitwaye Ng'wanamalundi, Nyamiti, Chibupa na Seche inarejelea mbinu na harakati za ukombozi dhidi ya dhuluma, unyonyaji na ukandamizaji. Ngoma ya arusi, ambayo inahusisha maandalizi ya ndoa kati ya Nyamiti na Chibupa na mpambe wao Seche, imetumika kuashiria nafasi ya vijana katika harakati za ukombozi wa jamii. Mwandishi ametumia mandhari ya uchawi na uganga kuibua na kuwasilisha dhamira ya unyonyaji na harakati za ukombozi. Tukirejelea nadharia ya Mwingilianomatini tunaona kuwa katika utunzi huu msanii ameathiriwa na falsafa ya Kiafrika kuhusu uchawi na uganga na hivyo kutumia falsafa hiyo kisanii kwa kutumia ubunifu, kuiwasilisha uhalisia ndani ya jamii. Aidha, msanii anaingiza vipengele vya fasihi simulizi na falsafa ya Kiafrika katika ujenzi wa dhamira.

Hoja hii inashadidiwa na maelezo ya msanii wakati wa usaili ambapo alikiri kuathirwa na mapokeo simulizi ya jamii ya Ubena Zomozi kuhusu mzee mchawi aliyefuga misukule katika himaya yake. Mzee huyo, aliwachukua watu kichawi na kuwaharibu bongo zao na kuwafanya wasijitambue wala kujielewa ili aweze kuwatumikisha, kuwanyonya na kuwadhulumu jasho lao. Mtunzi alibainisha kuwa, aliathiriwa na masimulizi hayo na aliuona uchawi kama mbinu ya ukandamizaji, unyonyaji na dhuluma ambayo inajikita katika uchumi na uhai, kwamba mtu

[1] Misukule ni jina linalotumika kurejelea pia vizuu

anadhulumiwa uhai wake na kupotezwa katika maisha halisi na kuelekezwa katika udhahania. Wakati wa majadiliano ya vikundi wahojiwa walibainisha uwepo wa aina hiyo ya uchawi katika jamii za kitanzania. Kwa mfano, kwa Wasukuma kuna sehemu inaitwa Gamboshi, ambako ni kijiji dhahania cha uchawi, watu wote wanaokufa kwa njia ya uchawi hupelekwa kuishi katika kijiji hicho na kutumikishwa. Mfano mwingine ni Pemba ambapo kuna sehemu inaitwa Giningi[2] ambayo imejitokeza katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* (19) ya Mohmmed S. Mohammed. Kwa hiyo, mtunzi alikiri kutumia masimulizi hayo ili kuibua suala la utabaka, uonevu, unyonyaji, ukandamizaji na aina fulani ya utumwa katika masimulizi ya jamii hiyo.

Aidha, wakati wa usaili, mtunzi alithibitisha kuwa hupenda kutunga kazi za fasihi zinazoibua matatizo ya jamii ili kuwaamsha na kuwaelimisha wananchi ndani ya jamii kuhusu namna ya kujikomboa kutokana na unyonyaji na ukandamizaji ndani ya jamii. Pamoja na mapokeo simulizi ya kisa ya Ubena Zomozi, msanii alikiri kuathirwa na mapokeo simulizi ya kisakale cha jamii ya Wasukuma kuhusu Ng’wanamalundi ambaye alikuwa na sifa za ushujaa na miujiza ya kiganga ambayo aliitumia kupambana na wachawi na kutibu watu walioathiriwa na uchawi. Mtu huyu katika kisakale hicho anasimuliwa kama mkombozi wa jamii. Kwa hiyo, tamthiliiya yake hii ni matokeo ya athari ya mapokeo simulizi ya jamii mbili. Moja ikiwa inawasilisha ukandamizaji na nyingine ikiwa inahusisha ukombozi. Visakale hivi ndivyo vilivyomuathiri mtunzi na kuamua kutumia sanaa na ubunifu wa kisanii kuwasilisha na kuibua hali ya ukandamizaji katika jamii na harakati za ukombozi.

[2] Maelezo haya yanathibitishwa na Jilala (haijachapishwa) katika majadiliano aliyoyafanya na wanafunzi wa MA Kiswahili Pemba (August, 2015)

### 4.1.3 Muhtasari wa Tamthiliya ya *Fumo Liongo*

Kwa kutumia mbinu ya mapitio ya maandiko, utafiti huu ulibaini kuwa, tamthiliya ya *Fumo Liongo* inawasilisha masuala ya uongozi mbaya wa tabaka tawala chini ya Mfalme Daudi Mringwari, dhidi ya tabala tawaliwa. Mfalme huyo aliitawala Pate kwa imla na hofu iliyotokana na umaarufu wa nduguye Fumo Liongo, aliyekuwa shujaa vitani, aliyependwa na watu, malenga stadi na mkosoaji wa siasa za Mfalme Daudi Mringwari. Hivyo, ubabe, vitisho, ukatili, unyonyaji na unyanyasaji vilikuwa ni sehemu ya utawala huo. Chini ya uongozi wa Mfalme Mringwari, wananchi hawakuwa na fursa ya kutoa mawazo yao hata kama yalikuwa ni mazuri na yenye tija kwa jamii. Aliyethubutu kufanya hivyo aliishia kuuawawa kwa amri ya Mfalme, kama ilivyokuwa kwa waziri Msheki, aliyeonyesha msimamo wa kumtetea Fumo Liongo kwamba ni mzalendo anayeipenda na kuitetea nchi yake. Kwa kusema hivyo, Msheki alionekana ni msaliti anayepingana na Mfalme, hivyo iliamriwa auawe na kutupwa baharini.

Kutokana na uongozi huo kandamizi wa Mfalme, Fumo Liongo anatokea kuwa ndiye mtetezi wa wananchi na mkosoaji wa siasa na uongozi mbaya wa Mfalme dhidi ya wananchi wanyonge wa Pate. Wananchi wanatokea kumpenda sana, hali ambayo inamtia wasiwasi Mfalme na kujenga chuki ya wazi dhidi yake. Hali hiyo inamfanya Mfalme kuanza kuweka mbinu na mikakati ya kumuangamiza Fumo Liongo. Hatimaye Mfalme Mringwari anafanikiwa kumuua Fumo Liongo, baada ya kuibukua siri yake ya uhai na ufu kupitia kwa mwanaye wa kambo, Zahidi.

Tamthiliya hii inadhihirisha mawazo ya nadharia ya mwingilianomatini ambapo tunabaini kuwa, jina la (kitabu) tamthiliya yake ya *Fumo Liongo,* ni athari aliyoipata msanii katika utendi wa "Fumo Liongo" na kuchukua jina la mhusika wa kwenye utendi na kumtumia kwenye tamthiliya yake. Hoja hii inathibitishwa na maelezo ya mtunzi wakati wa usaili ambaye anaeleza kuwa, aliamua kutunga tamthiliya hiyo ili kuendelea kuihifadhi historia ya Pate na shujaa wa Kiafrika, Fumo Liongo katika utanzu huu wa fasihi. Mtunzi alifafanua kuwa, historia za watu maarufu wa Afrika walioishi kale zinapotea na jamii ya sasa haitatambua uwepo wake kama hakutakuwa na juhudi za kuzihifadhi. Hivyo yeye kama mtunzi mwenye mapenzi na historia za jamii mbalimbali, ameamua kwa vitendo kuanza kuzihifadhi. Hata hivyo, wakati wa usaili mtunzi alikiri kuwa utunzi wake wa tamtiliya ya *Fumo Liongo* ni matokeo ya athari aliyoipata kwa kusoma utenzi wa "Fumo Liongo" uliotungwa mwaka 1913, TUKI (1999) na kuamua kutumia mbinu za kisanii na ubunifu kutunga tamthiliya ya *Fumo Liongo*.

## 4.2 Matumizi ya Mwingilianomatini katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*

Mojawapo ya malengo mahsusi ya utafiti huu lilikuwa ni kubainisha matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo.* Katika kufikia lengo hili, utafiti huu ulitumia mbinu ya mapitio ya maandiko kwa kusoma, kuchunguza na kuchambua tamthiliya hizo ili kubainisha matumizi ya mwingilianomatini yanavyojitokeza katika utunzi wa tamthiliya hizo. Hivyo basi, kwa kutumia mbinu hiyo, utafiti huu uliweza kubainisha mwingilianomatini matini

katika tamthiliya hizo. Aidha, utafiti huu ulitumia mbinu za usaili na majadiliano ya vikundi ili kujaziliza na kufafanua zaidi data za utafiti huu.

Vilevile data zilizokusanywa kwa mbinu ya mapitio ya maandiko, usaili na majadiliano ya vikundi zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi maudhui. Kwa kutumia mbinu hii mtafiti aliandaa mwongozo wa kuchambulia data ambapo matini zinazofanana ziliwekwa pamoja ili kurahisha uchambuzi na uwasilishaji wake, kwa mfano matini ambazo zilibainika kuwa ni mtindo wa fasihi simulizi kama vile nyimbo, ushairi, hadithi ziliwekwa katika kundi moja[3]. Ili kuchambua matini zilizotumika katika utunzi na Emmanuel Mbogo, tumezigawa katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni mwingilianomatini katika utunzi wa tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na sehemu ya pili ni mwingilianomatini katika utunzi wa tamthiliya ya *Fumo Liongo.* Kwa hiyo, sehemu ifuatayo inawasilisha matumizi ya mwingilianomatini kwa kubainisha matini zilizomo katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*.

### 4.2.1 Mwingilianomatini katika utunzi wa *Ngoma ya Ng'wanamalundi*

Utafiti huu ulibaini kuwa utunzi wa *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ni matokeo ya athari ya mapokeo simulizi ambayo yalimuathiri mtunzi na kuyatumia masimulizi hayo kuzalisha tamthiliya hii. Aidha, utafiti huu pia ulibaini kuwepo na mwingilianomatini katika kazi hii ya fasihi ambapo kuna matini zilizotumika katika mapokeo simulizi

[3] Katika utafiti huu fasili za matini za mbinu ya mwingilianomatini zilizotumika na zinazojitokeza katika tamthiliya zote mbili, zitatolewa pale matini inapoelezwa kwa mara ya kwanza katika tamthiliya ya kwanza ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Matini hiyo itakapokuwa inaelezewa katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* haitatolewa fasili yake tena. Katika tamthiliya ya pili ya *Fumo Liongo* fasili itatolewa kwa matini ile tu ambayo haikujitokeza katika tamthiliya ya kwanza ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*

zinajitokeza pia katika tamthiliya hii. Kwa ujumla, sehemu hii inabainisha matumizi ya mwingilianomatini kwa kubainisha matini zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Utafiti huu ulichunguza matumizi ya mwingilianomatini kwa kubainisha matini zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na kudhihirisha mwingilianomatini katika tamthiliya hiyo. Kwa kutumia mbinu ya mapitio ya maandiko mtafiti alibainisha matini zifutazo kama zinavyojitokeza kwenye jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.1 Matini zilizotumika katika utunzi wa *Ngoma ya Ng'wanamalundi***

| **Na.** | **Aina ya matini iliyojitokeza** |
|---|---|
| 1. | Hadithi |
| 2. | Ngoma |
| 3. | Nyimbo |
| 4. | Majigambo |
| 5. | Wahusika wa fasihi simulizi |
| 6. | Ushairi |
| 7. | Nguvu za sihiri |

Chanzo: Data za Utafiti katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (Juni, 2015)

Jedwali namba 4.1 linaonyesha matini mbalimbali ambazo zinadhihirisha matumizi ya mwingilianomatini katika katika utunzi wa tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi.* Data hii haikuwa tofauti na data zilizobainishwa na wahojiwa wakati wa majadiliano ya vikundi na pia wakati wa usaili msanii aliweza kuzitolea ufafanuzi vipengele hivyo kama matokeo ya athari ya kazi tangulizi za fasihi simulizi. Sehemu ifuatayo inajadili matini hizo kwa mifano na jinsi zinavyodhihirisha mwingilianomatini katika utunzi wa tamthiliya ya Ngoma ya Ng'wanamalundi

#### 4.2.1.1 Matumizi ya Hadithi

Kwa mujibu wa TUKI (2013), hadithi ni habari za mambo yaliyotukia, mtungo wa habari, kisa, ngano, masimulizi, hekaya. Utafiti huu ulibaini kuwa, mwandishi ametumia matini ya hadithi kujenga tamthiliya yake. Tamthiliya hii ni matokeo ya masilumilizi ya hadithi mbili za jamii mbili kisa cha Ubena Zomozi na kisakale cha Mwanamalundi. Wahojiwa walidhihirisha kuwa mwingilianomatini unajitokeza katika hadithi hizo ambazo zinadhihirisha athari ya matini moja kujitokeza ndani ya matini nyingine. .

Katika mahojiano na mtunzi wa tamthiliya hii, utafiti huu ulibaini kuwa msingi wa kutungwa tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ni kisakale kinachopatikana katika kabila la Wasukuma kuhusu mtu maarufu na mwenye miujiza mingi, aliyeitwa Mwanamalundi, na masimulizi ya kisa cha kweli kuhusu mzee mmoja aliyekuwa mchawi wa misukule aliyekuwa akiishi katika kijiji cha Ubena Zomozi kilichoko Chalinze, mkoani Pwani.

Wakati wa usaili, mtunzi alieleza kuwa ameathiriwa na kisakale hicho baada ya kukisikia, na kikamvutia akitumie katika utunzi wa tamthiliya hii. Vilevile utafiti ulibaini kuwa, masimulizi au habari ya kisakale hicho cha Wasukuma, imewahi kuandikwa na Boaz (1974). Maandiko au masimulizi hayo ya hadithi yanamhusu mtu aliyewahi kuwa maarufu katika historia ya Wasukuma aitwaye Mwanamalundi. Huyu alizaliwa mwaka 1892 katika Wilaya ya Kwimba mkoani Mwanza. Mwanamalundi alikuwa mcheza ngoma hodari mwenye, uwezo wa kufanya miujiza mingi, hasa baada ya kupewa dawa na bibi kizee aliyekuwa mganga maarufu. Baadhi ya miujiza hiyo ni pamoja na kuwa na uwezo wa kuikausha miti iliyokuwa karibu

yake kwa kuinyooshea kidole au kuishika na kuwa na hirizi aliyokuwa anaitupia baharini, na akishaitupa maji hujitenga na kuacha nchi kavu katikati kama njia iliyomwezesha yeye na kijakazi wake kupita katikati ya bahari kutoka sehemu moja kwenda ng'ambo ya pili.

Katika masimulizi ya kisa cha kweli cha Ubena Zomozi, mtunzi alieleza kuwa alikwenda katika kijijini hicho kumtembelea rafiki yake. Alipofika kijijini hapo, alikuta kuna baadhi ya nyumba zimebomolewa, ikiwemo ya mzee mmoja aliyekuwa anamfahamu. Rafiki yake alimueleza kuwa mzee huyo aliamua kukihama kijiji hicho kwa aibu iliyompata, baada ya kufichuliwa kama ni mchawi wa misukule na watu wanaojiita Konikoni, ambao hufichua wachawi kwa nguvu za dawa zao. Ilibainika kuwa misukule hao walikuwa wanatumikishwa na mzee huyo katika kumzalishia mali mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kumlimia mashamba yake na shughuli nyinginezo. Hivyo kisa hiki kilimvutia mtunzi na kupata wazo la kutunga tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, linaloelezea kuhusu utabaka, utumikishaji, ukandamizaji na unyonyaji wa baadhi ya watu dhidi ya watu wengine.

Kupitia usaili uliofanywa kwa mtunzi, utafiti huu ulibaini kwamba, mwandishi ametumia sifa za masimulizi ya mzee mchawi wa Ubena Zomozi na misukule wake na kujenga taswira ya kisanaa iliyowakilisha vema mawazo ya uovu aliokuwa akiufanya mzee huyo kwa kutumia uchawi wake huo. Katika tamthiliya hii, Chidama amejengwa kama mwonevu, mnyanyasaji na mkandamizaji anayetumia nguvu za kichawi kutimiza adhima yake kwa kuharibu ubongo wa watu na kuwaweka katika milki yake isiyoonekana kwa nguvu za macho ya kibindamu. Kwa hiyo utafiti huu

umebaini kuwa, dhamira za tamthiliya hii ni matokeo ya athari ya masimulizi ya kisa cha kweli ambayo yalimuathiri mtunzi na kutumia matini ya hadithi hiyo kujenga tamthiliya yake kwa kutumia mbinu na mtindo wa kisanii.

Vilevile mwandishi ametumia sifa za Mwanamalundi wa kutoka katika kisakale cha jamii ya Wasukuma na kuongeza mbinu za kisanii na ubunifu wake, ili kujenga taswira ya ukombozi na harakati za ukombozi wa wanyonge dhidi ya tabaka tawala.Ng'wanamalundi katika tamthiliya, amejengwa kama shujaa, mtoa elimu na mafunzo ya uokovu dhidi ya viongozi wachache wabadhilifu kama Chidama. Ni mpenda haki na usawa anayewasaidia vizuu kukomboa mali zao kutoka kwa Chidama na kuzirudisha mikononi mwao.

Aidha, utafiti huu umebaini kuwa mwandishi anatumia sifa za mhusika Ng'wanamalundi katika kisakale cha jamii ya Wasukuma na kumvika mhusika Ng'wanamalundi katika tamthilya yake. Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa msanii amemhamisha Ng'wanamalundi wa kisakale na kumhamishia katika kazi yake ya fasihi. Mbinu hii inadhihirisha msingi wa nadharia ya mwingiliano matini ambao unasema kuwa mtunzi huchota matini za kazi moja ya fasihi na kuihamishia katika matini nyingine ya fasihi (taz. Wamitila, 2003; Senkoro, 2011) .

Aidha, mbali ya kutumia hadithi kujenga kazi yake ya fasihi kama matokeo ya athari ya mapokeo simulizi. Mwingiliano matini unajitokeza katika matumizi ya hadithi ndani ya tamthiliya hii. Msanii ametumia usimulizi wa hadithi ndani ya tamthiliya yake. Tazama mfano katika dondoo ifuatayo kuthibitisha hoja hiyo.

(1) "…Si mganga tu bali ni mtu wa ajabu. Alizaliwa kimiujiza na atajakufa kimiujiza. Ngano zinaeleza kuwa: baba yake Ng'wanamalundi aliambiwa na mganga wake kuwa utazaa mtoto mmoja tu wa kiume na wewe kama dume la nyuki, utaiaga dunia. Kweli. Mara baada ya mkewe kutunga mimba yake Ng'wanamalundi aliiaga dunia. Siku alipozaliwa Ng'wanamalundi mvua kubwa ya mawe ilinyesha nchi nzima. Mito ikafurika, radi za mvua zikachana na kuunguza mibuyu na mikuyu. Tetemeko la ardhi lilirindima toka mashariki ya dunia hadi magharibi. Na ghafla mchana wa jua la utosini ukakumbwa na giza nene. Lakini mkunga aliukata mnyororo wa kitovu cha mtoto yule mchanga, akakirusha juu! Kikapaa kikanata mawinguni – na akakirusha juu! Kikapaa kikanata mawinguni – Na tazama: ghafla giza likatoweka na jua likaangaza tena katikati ya upindi wa mvua…." (Uk.27-28)

Chanzo: Data za Utafiti katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (Juni, 2015)

Mwandishi ameyaweka masimulizi yanayomhusu Ng'wanamalundi katika mtindo wa usimulizi wa hadithi za kijadi, lakini bila kuwa na kianzio wala kimalizio kilichozoeleka katika hadithi za kijadi. Mwandishi anatudondolea historia ya Mwanamalundi tangu utabiri wa kuzaliwa kwake, maajabu yaliyotokea siku ya kuzaliwa kwake, safari yake ya kwenda kutafuta dawa ya kuchezea ngoma, kukutana kwake na Bi kizee na yaliyotokea mwituni na jinsi alivyotakiwa kuacha kucheza ngoma kwa kujifurahisha tu bali kucheza ngoma mpya, ngoma itakayowakomboa wanyonge wote duniani ambako giza limetamalaki. Mwandishi ameonyesha upeo wa hali ya juu kwa kutumia matini ya hadithi katika tamthiliya yake, ili kudokeza na kuelezea chimbuko la harakati za ukombozi dhidi ya unyonyaji na ukandamizaji wa Chidama.

Wakati wa usaili, utafiti huu umebaini kuwa, mtunzi ameathiriwa na masimulizi ya kimapokeo ya kisakale cha Wasukuma na masimulizi ya tukio la kweli kuhusu uchawi wa misukule. Hivyo tamthiliya hii imechota maudhui toka katika masimulizi hayo na hivyo kuleta uhusiano wa kimaudhui na wahusika baina ya masimulizi hayo

na tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Ubunifu huu wa kuchota malighafi za kutungia tamthiliya kutoka katika masimulizi ya kweli yaliyowahi kutokea katika jamii, unaonyesha ukomavu wa hali ya juu katika utunzi wa E. Mbogo.

Nadharia ya Mwingilianomatini kama inavyowasilishwa na Kristeva (1980), inasisitiza kuwa utunzi wa aina hii unadhihirisha uathiriano na uhusiano wa matini za kifasihi, kwamba mbinu za uteuzi wa matini za kifasihi hutokana na muathiriano wa kazi za kifasihi zilizotangulia na kusaidia katika uashiriaji wa kazi za baadaye. Kristeva anaitazama dhana hii kama jumla ya maarifa na mbinu zinazoifanya matini kuwa na maana. Maana ya matini hapa inaangaliwa kama inayoitegemea matini nyingine. Hapa tunaona uhusiano uliopo kati ya hadithi na tamthiliya, na jinsi mwandishi alivyomudu kutumia hadithi katika tamthiliya yake.

**4.2.1.2 Matumizi ya ngoma**

Kwa mujibu wa TUKI (2013), neno ngoma lina maana mbili kama ifuatavyo. Kwanza, ni ala ya muziki inayotengenezwa kwa kuwambwa ngozi kwenye mzinga. Halikadhalika ni mchezo wa kufuata mdundo wa ala hiyo. Utafiti huu ulibaini kuwa mwingiliano matini katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi,* unajidhihirisha katika matumizi ya Ngoma.

Wakati wa usaili, mtunzi alibainisha kuwa, ametumia ngoma katika utunzi wa tamthiliya yake hii ili kuingiza na kuonyesha thamani ya Uafrika na kuleta upya katika utunzi wa tamthiliya hii na kuipa vionjo vya Kiafrika. Sambamba na hilo, Aidha, ngoma ni moja ya sifa ya jamii ya Wasukuma na Ng'wanamalundi katika kisakale alitumia ngoma na alicheza ngoma na kutumia mbinu mbalimbali za

kushinda ngoma. Kwa hiyo, utafiti huu umebaini kuwa matumizi ya ngoma yanadhihirisha mwingiliano matini ambapo msanii amechota mbinu za utunzi kutoka katika masimulizi ya kisakale na kuyatumia katika kwa ubunifu na usanii kujenga maudhui ya tamthiliya yake. Hoja hii pia iliungwa mkono na wahojiwa wakati wa majadiliano ya vikundi kuwa matumizi ya ngoma yanadhihirisha mwingilianomatini katika tamthiliya ya Ngoma ya Ng'wanamalundi.

Wakati wa uchambuzi wa matini ya tamthiliya hii na matokeo ya majadiliano ya vikundi, utafiti huu umebainisha ngoma za aina tatu zilizotumiwa na msanii katika kuwasilisha maudhui ya tamthiliya ya ngoma ya Ng'wanamalundi. Ngoma hizo ni; ngoma ya arusi/ Nyamiti, ngoma ya Chidama na ngoma ya Ng'wanamalundi.

Kupitia majadiliano ya vikundi iligundulika kuwa, ngoma ya arusi ina wahusika vijana ambao ni Nyamiti, Chibupa, Seche. Ngoma hii ilionekana inachezwa wakati wa maandalizi ya arusi ya Chibupa na Nyamiti.  Ngoma za aina mbalimbali zilichezwa katika siku hii muhimu kama anavyotubainishia Seche, "Nakwambia leo, usiku ngoma aina kwa aina. Wenye kupenda hii, wenye kupenda ile. Ili mradi…" uk 5. Katika Afrika ngoma za arusi huchezwa katika kumuandaa bi arusi kuingia katika hatua ya utu uzima na kuchukua jukumu la kumtunza mume. Vilevile ngoma hizo huchezwa kwa madhumuni ya kufurahisha na kunogesha sherehe za arusi. Dondoo lifuatalo linashadadia hoja hii:

(2) NYAMITI: (*mirindimo ya ngoma ya arusi inaongezeka Sasa tunasikia wanabadili mapigo na tunasikia mirindimo ya sindimba. Nyamiti anaruka kwa furaha*.) Ee! Sindimba – unyago! Wote huko arusini wanachemka - mie tu. (*Mirindimo ya sindimba inaongezeka*)

Chanzo: Data za Utafiti katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (Juni, 2015)

Wakati wa majadiliano ya vikundi wahojiwa walibainisha kuwa ngoma hii inaashiria dhima na wajibu wa vijana katika maendeleo na ujenzi wa jamii. Hata hivyo harakati hizo za ujenzi wa jamii unakwamishwa na viongozi ambao hawapo tayari kuona ukombozi na maendeleo ya vijana Vijana. Kwa mfano Chidama anaonekana kudhurumu na kuingilia nguvu ya vijana kwa kudhurumu uhai wa Nyamiti na kummiliki kwa nguvu zake. Hatimaye, vijana wanaamua kuutafuta ukombozi wa kweli dhidi ya dhuluma.

Utafiti huu ulibaini pia kuwepo kwa ngoma ya Chidama. Wakati wa majadiliano katika vikundi watafitiwa walibainisha kuwa, ngoma hii ina wahusika wanne ambao ni Chidama, Melo, Mahube na Vizuu wa Chidama. Ngoma hii imetumika kama sitiari inayorejelea mbinu za ukandamizaji na unyanyasaji. Mtunzi anaitumia sitiari hii kisanii kwa kuionesha ngoma hii kama mbinu ya kuwahadaa na kuharibu ubongo wa watu ili kurahisisha ukandamizaji na unyonyaji kwa manufaa ya wachache. Dondoo lifuatalo linabainisha madhumuni ya ngoma ya Chidama:

> (3) CHIDAMA: …Siku zote nimekwambia lazima wacheze dansi ya Chidama. Ngoma ya kuwafanya wakakamavu wa mwili lakini mazimbwezimbwe wa roho na bongo. Dansi ya kutia mbolea nyongo ya unyonge wao. Dansi ya kurutubisha nidhamu katika kazi yao.
>
> Chanzo: Data za Utafiti katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (Juni, 2015)

Wakati wa usaili, mtunzi alikiri kuwa mbinu ya ngoma ni ubunifu alioingiza ili kuwasilisha masimulizi aliyopokea kuhusu mzee mchawi wa Ubena zomozi ili kuelezea taasisi kandamizi ya uchawi wa misukule, ambapo vizuu hufanyishwa kazi za uzalishaji mali bila malipo wala kujali afya zao, kwa faida ya mchawi husika. Mtunzi alifafanua kuwa mawazo haya ya kutumia ngoma ya Chidama aliyabuni

baada ya kupata tukio la kweli la uchawi wa misukule uliokuwa ukifanywa na mzee mmoja aliyekuwa anaishi Ubena Zomozi.

Utafiti huu ulibaini kuwa, msingi mkuu wa ngoma ya Chidama ulikuwa ni unyonyaji, unyanyasaji, ukandamizaji, udhalilishaji na uzalishaji mali kwa gharama ndogo yenye kuleta faida kubwa kwa Chidama. Hivyo wachezaji walihitajika kukomaza maungo zaidi na kuleta nidhamu ya woga katika kazi.

Ngoma ya tatu iliyobainishwa na utafiti huu ni ngoma ya Ng'wanamalundi. Ngoma hii ina wahusika Ng'wanamalundi, Dude, Sango na Vizuu wa Ng'wanamalundi. Baadaye walijiunga Seche na Chibupa. Tofauti na ngoma ya Chidama, wahojiwa walibainisha kuwa ngoma hii ni ngoma ya ukombozi ambayo wachezaji hufundishwa jinsi ya kuicheza kwa utaratibu maalum na kwa madhumuni maalum, kwani ni ngoma ya kivita inayochezwa kwa kutumia silaha za jadi na mikuki. Ngoma hii inapingana na ngoma ya Chidama. Dondoo lifuatalo linatubainishia madhumuni ya ngoma ya Ng'wanamalundi:

> (4) NG'WANAMALUNDI: Nimewaonya tangu mwanzo kuwa haya si mapambano ya binafsi dhidi ya udhalimu. Sio wewe peke yako unayetiririka machozi ya damu hapa kijijini. Watu wengi wamewapoteza ndugu zao kwa mavumba haya ya zongo. Jukumu la ngoma ya Ng'wanamalundi ni kuleta ukombozi kwa masikini wote. uk 43,

Chanzo: Data za Utafiti katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (Juni, 2015)

Katika majadiliano ya vikundi na mapitio ya maandiko, utafiti huu ulibaini kuwa, msingi mkuu wa ngoma hii ni ukombozi dhidi ya ukandamizwaji na unyonyaji. Halikadhalika, tofauti na ngoma ya Chidama, utafiti umegundua kuwa, hii ni ngoma inayochezwa kwa kufuata utaratibu maalum uliofundishwa kwa wahusika wake wote. Uchezaji wake ni wenye lengo la kukomboa tu, na haichezwi kwa madhumuni ya kujiburudisha au jambo jingine lolote. Dondoo lifuatalo linabainisha hayo:

(5) NG’WANAMALUNDI: Njoni tuanze kucheza. (*Vizuu wanaingia kila mmoja ana mkuki, hata Duda naye ana mkuki wake)*
NG’WANAMALUNDI: (*anapaza sauti*) SASA WAKATI UMEFIKA WA KUCHEZA NGOMA YA NG’WANAMALUNDI. (*Vizuu na wengine wanaitikia. Sasa Ngoma inapamba moto. Wanacheza hadi wanapagawa hasa wale vizuu…)*
NG’WANAMALUNDI: Yuko wapi adui!
KIZUU 1: Yuko wapi adui!
NG’WANAMALUNDI: Ua Chidama!Ua!
KIZUU 1: Ua Chidama! Ua!
NG’WANAMALUNDI: Ua Chidama! Ua!
KIZUU 2: Ua Chidama! Ua!
NG’WANAMALUNDI: Damu! Damu! Damu!
KIZUU 3: Damu! Damu! Damu! Uk 41

Chanzo: Data za Utafiti katika *Ngoma ya Ng’wanamalundi* (Juni, 2015)

Utafiti huu ulibaini kuwa ngoma ya Ng’wanamalundi ndiyo iliyoleta ukombozi kwa kukomboa njia zote kuu za uchumi kutoka kwa Chidama. Katika utafiti huu, kupitia majadiliano ya vikundi, ngoma ya Ng’wanamalundi ilielezewa kuwa ni kiwakilishi cha Azimio la Arusha lililokata mirija yote ya unyonyaji na kurudisha njia zote kuu za uchumi mikononi mwa wananchi.

Hata hivyo, utafiti huu umebaini pia kuwa, kutumika kwa ngoma katika kuwasilishia maudhui ya tamthiliya hii ni athari ya mwingilianomatini inayotokana na kisakale cha kabila la Wasukuma kuhusu shughuli aliyokuwa anaifanya Mwanamalundi ya kucheza ngoma za asili. Ngoma ni utanzu mmojawapo wa fasihi simulizi. Kwa hiyo, msanii ametumia utanzu huu wa fasihi simulizi katika kujenga riwaya yake. Matumizi ya utanzu wa ngoma katika tamthiliya yanadhihirisha mwingilianomatini wa matini ya utanzu wa ngoma katika kujenga maudhui ya tamthiliya. Kwa hiyo, sifa na matendo ya Ng’wanamalundi katika kisakale yameathiri utunzi wa Emmanuel Mbogo na hivyo kutumia ubunifu wake kujenga maudhui ya kazi yake ya fasihi.

Matumizi ya sifa na matendo ya mhusika katika kisakale yanadhihirisha mwingilainomatini katika tamthiliya hiyo.

#### 4.2.1.3 Matumizi ya Nyimbo

Matini nyingine iliyobainishwa wakati wa utafiti huu ni nyimbo. Mutembei (2012), anaeleza kuwa nyimbo zinazotumiwa katika kazi za fasihi za Kiafrika huwa ni sehemu ya kazi hiyo ya fasihi na huwa ni kipengele muhimu katika kujenga maana nzima ya simulizi katika kazi hiyo ndani ya kazi yenyewe. Katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, utafiti huu ulibaini matumizi ya wimbo ambayo yalidhihirisha mwingilianomatini, mfano ni wimbo unaoimbwa katika maandalizi ya harusi ya Chibupa na Nyamiti. Tazama mfano ufuatao:

(6) SECHE (*anaimba*)
Leo mambo mtaona
Leo mambo mtaona
Tumembadili kijana!
Tumembadili kijana! Uk 5

Chanzo: Data za Utafiti katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (Juni, 2015)

Wakati wa majadiliano ya vikundi, wahojiwa walibainisha kuwa, ngoma ya harusi ni ishara ya harakati na nafasi ya vijana katika kuleta mapinduzi ya mfumo kandamizi wa tabaka la wanyonge ambalo ndiyo walio wengi, dhidi ya tabaka tawala. Kwa hiyo harusi hapa ni ishara ya harakati za ukombozi.

Aidha, wakati wa usaili mtunzi alielezea kuwa, katika utunzi wa tamthiliya hii ametumia matini za fasihi simulizi kama mbinu ya utunzi ili kuingiza ujumi wa Kiafrika na kutumia utajiri wa tanzu za fasihi simulizi kama mbinu za utunzi wa tamthiliya hii. Utafiti huu ulibaini kuwa, matumizi ya nyimbo yanaonesha namna mtunzi anavyoingiza matini za fasihi simulizi katika tamthiliya. Mbinu hii

inadhihirisha mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo. Matumizi ya nyimbo kama utanzu wa fasihi simulizi katika tamthiliya, ni mwingilianomatini unaodhihirisha kuathiriana na kuingiliana kwa tanzu za kifasihi katika mbinu za utunzi, kwa lengo la kuchangizana na kutegemeana ili kukamilishana kimaana, kama anavyobainisha Kristeva katika nadharia yake ya mwingilianomatini.

#### 4.2.1.4 Matumizi ya Majigambo

Wamitila (2003) anafasili majigambo kuwa ni aina ya maghani (sifo) yanayohusu kujisifu au sifa, aghlabu kuhusu kutongoa utungo wa kujisifu kuhusiana na kitendo fulani cha ushujaa, urijali au matendo muhimu (tazama pia Samwel, 2012; Mulokozi; 1996). Katika utafiti huu, tulibaini matumizi ya majigambo katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Majigambo ni mmoja wa utanzu wa fasihi simulizi, kwa hiyo ujitokezaji wa majigambo katika tamthiliya unadhihirisha mwingilianomatini wa fasihi simulizi katika tamthiliya.

Aidha, utafiti huu ulibaini kuwa mbinu ya majigambo katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* inajidhihirisha katika nyanja mbili ambazo ni; majigambo ya tabaka tawala na mjigambo ya tabaka tawaliwa. Majigambo ya tabaka tawala yanawasilishwa na Chidama wakati akimtumia Ng'wanamalundi joka la vichwa saba, ili liende likamfundishe adabu na heshima. Tazama mfano ufuatao:

(7) CHIDAMA: …Joka la vichwa saba
Lakini ni joka moja tu
moja katika saba na saba katika moja,
Ewe mtambaa chini,
Mwenye meno ya sumu
Mwenye kinywa kilichojaa misumari na miiba ichomayo
na kurarua bila huruma, bila kusita…
Haya nawende, nakutuma:

> Nenda ukatumbukize ukucha wako wa chuma ubavuni mwake,
> Ukamfutue na kumfumua matumbo yake
> Ukumzingire na kumzingara figo zake
> Umkamue anye na kujinyea
> Umminye akojoe na kujikolea.
> Ajue kuwa Chidama ni Chidama kweli
> (*Anamtemea mate kichwani kisha 'anamrusha' nje kupitia dirishani*). Uk 15-16.

Chanzo: Data za Utafiti katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (Juni, 2015)

Wahojiwa katika majadiliano ya vikundi walieleza kuwa, msanii amemtumia Chidama kisitiari ili kuwakilisha tabaka tawala, tabaka ambalo lina nguvu kiuchumi. Kwa hiyo, mbinu hii ya majigambo imetumika kulianika tabaka tawala linavyotumia uwezo na nguvu zao katika kupambana na harakati za ukombozi zinazofanywa na tabaka tawaliwa.

Aidha, utafiti ulibainisha pia majigambo ya tabaka tawaliwa yanayowasilishwa na shujaa mtetezi wa wanyonge, Ng'wanamalundi. Tazama dondoo lifuatalo:

NG'WANAMALUNDI: Najua aliyekutuma

> Lakini huyo si *mulume* sawasawa.
> Wewe ni *tonga*, hujawa *tui* bado. Huchochote bali garasa, shushu la nyoka mgonjwa, (*anamtemea mate yule nyoka*).
> Lakini nakutambua wewe U nani.
> Najua ndiye wewe yule **anukae damu ya maskini**.
> Huwezi kunizuga na mavazi uliyovaa. Kwani sabuni na manukato havitoshi kutoharisha nuksi iliyoko ndani ya kichwa, roho na matendo yako. Kwani nani hajui kuwa wewe ni mchawi wa msukule?...(uk.34)

Chanzo: Data za Utafiti katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (Juni, 2015)

Kupitia majigambo hayo, utafiti huu umebaini kuwa, nguvu ya umma haiwezi kuzoroteshwa na nguvu ya wachache. Msanii kupitia Ng'wanamalundi anasema, "Najua ndiyo wewe yule anukae damu ya masikini. Huwezi kunizuga na mavazi uliyovaa. Kwani sabuni na manukato havitoshi kutoharisha nuksi iliyoko ndani ya

kichwa, roho na matendo yako" Hii ina maana kuwa, tayari jamii inatambua mbinu za tabaka tawala na haiwezi kushindana na haja ya mapinduzi.

Wakati wa majadiliano ya vikundi utafiti huu ulibaini kuwa, mwandishi ametumia majigambo haya ya mahasimu wawili, Chidama, ambaye ni mnyonyaji anayedhulumu mali za wanayonge na Ng'wanamalundi ambaye ni mtetezi wa wanyonge, kusawiri mapambano ya watawala na watawaliwa. Hoja hii inathibitishwa na Ng'wanamalundi anapozumngumza na nyoka, "Lakini: sasa wakati umefika wa kucheza ngoma ya Ng'wanamalundi" uk.34. Hii ina maana kuwa, wakati wa mapinduzi dhidi ya dhuluma, uonevu, unyanyaswaji, ukandamizwaji na utumikishwaji umefika. Na ukombozi huo utapatikana kupitia ngoma ya Ng'wanamalundi.

Utafiti huu ulibaini kuwa, mtunzi ametumia mbinu ya majigambo kama mbinu ya kisanii, ili kuingiza ujumi wa Kiafrika katika kazi za sanaa na kuleta uhalisia wa maisha ya shujaa wa Kiafrika, ambaye hujisifu kwa jambo kubwa alilofanya. Mbinu hii inabainisha mwingilianomatini kwa kudhihirisha jinsi fasihi simulizi za Kiafrika zinavyoathiri ubunifu na utunzi wa fasihi andishi ya Kiswahili.

#### 4.2.1.5 Matumzi ya wahusika wa fasihi simulizi

Utafiti huu umebaini kuwa, mtunzi ametumia wahusika kutoka katika fasihi simulizi, mfano matumizi ya Joka la vichwa saba. Majigambo ya tabaka tawala yanawasilishwa na Chidama wakati akimtumia Ng'wanamalundi joka la vichwa saba, ili liende likamfundishe adabu na heshima. Rejea mifano ya 4.2.1.4 hapo juu.

#### 4.2.1.6 Matumizi ya Ushairi

Mulokozi (1996) anaeleza kuwa, shairi ni utungo wa kisanaa unaotumia lugha teule na mpangilio fulani wa maneno wenye kusawiri hisi, wazo, hali, kitu au tukio fulani na papo hapo kuvuta au kuathiri hisia zetu badala ya kutumia lugha nathari. Utafiti huu ulibaini kuwa, mwingilianomatini unajitokeza katika tamthiliya ambapo msanii ametumia ushairi na kuuingiza kama mbinu ya utunzi wa tamthiliya yake. Tazama mfano ufuatao:

(8) Ewe mtabaa chini
Ewe kifutu wangu, mfutua watu
Ewe chatu wangu, mvunja mbavu
Ewe koboko wangu, mkoboa watoto
Ewe Songwe wangu, msokomeza wana
Ewe swila wangu, mvimbisha matumbo
Ewe kipiri wangu, wa mate ya pilipili
Ewe moma wangu, mmogoa miamba… uk 15

Chanzo: Data za Utafiti katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (Juni, 2015)

Mfano huo unadhihirisha mwingilianomatini ambapo msanii anaingiza utanzu wa ushairi katika tamthiliya. Mbinu hii ni miongoni mwa mbinu ambazo msanii alizielezea kuwa alizitumia ili kuingiza vionjo vya fasihi simulizi ya Kiafrika katika utunzi wa tamthiliya. Aidha, utafiti huu ulibaini kuwa, msanii ametumia ushairi kwa kutumia lugha yenye mpangilio maalum wa mapigo na baadhi ya vina vya kati vinavyofanana ambavyo ni "-ngu" pia tunapata neno linalojirudiarudia ambalo ni "wangu" likitupa hisia na taswira ya nyoka anayeaminiwa sana na Chidama, ambaye ni tegemeo lake pekee na mwenye uwezo wa hali ya juu wa kuangamiza.

Wakati wa majadiliano walielezea matumizi ya nyoka katika matini hii kuwa ni athari ya fasihi simulizi ya Kiafrika ambapo wanyama, mizimu, majoka, miti na mawe hutumika kama wahusika wa kazi za fasihi. Wahusika hawa hupewa sifa ya kibinadamu ya kutenda na kuona. Mbinu hii inadhihirisha mwingilianomatini ambao

unatokana na msanii kuathiriwa na fasihi simulizi na hata kuchota vipengele vya fasihi simulizi na kuvitumia katika utunzi wake.

Wakati wa usaili ilibainika kuwa, matumizi ya ushairi ni matokeo ya kuathiriana na kuingiliana kwa matini za kifasihi kwa lengo la kuchangizana na kutegemeana katika kukamilishana kimaana, kama inavyobainishwa na nadharia ya mwingilianomatini katika Wamitila (2002).

#### 4.2.1.7 Matumizi ya Nguvu za Sihiri

Utafiti huu umebaini kuwa, nguvu za sihiri ni matini ambayo imetumiwa na msanii katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Nguvu za sihiri katika matini hiyo, zinajidhihirisha katika matumizi ya nguvu za kichawi na kiganga. Kwa mfano, mhusika Chidama amepewa nguvu za uchawi kama mbinu ya ukandamizaji na unyonyaji na kwa upande mwingine Ng'wanamalundi amepewa nguvu za uganga kama mbinu ya ukombozi na mapinduzi ya jamii ya wanyonge. Tazama mfano ufuatao;

> (9) MELO:..Ni pumzi za roho ngapi alizokwisha zinasa katika ile tunguri yake bwana wangu? Ebu: Toka mwezi juzi, kila siku kizuu mmoja. Wa kuvua samaki kumi. Wa kupalilia ishirini. Wa kuvuna mazao mbalimbali arobaini. Shughuli za nguruwe na kuku…uk 10-11

**Chanzo: Data za Utafiti katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (Juni, 2015)**

Katika majadiliano ya vikundi, utafiti huu ulibaini kuwa, mbinu ya nguvu za sihiri imetumika kisanii kama mbinu ya kisitiari ili kuwakilisha tabaka tawala na misingi ya unyonyaji, udhalimu, ukandamizaji na udhalilishaji inayotumiwa dhidi ya wananchi (vizuu). Chidama anawakilisha viongozi ambao ni tabaka tawala,

wanaojali nafsi zao, wanaojilimbikizia mali bila kujali wanyonge walio wengi na wanaotumia vibaya madaraka waliyonayo kwa faida yao. Wakati wa usaili na mtunzi, alieleza kuwa, mbinu hii inaruhusu mtunzi kuelezea jambo lolote lile, hata kama ni la kufikirika na linalomhusu mtu yeyote yule. Mwandishi alifafanua katika usaili huo kuwa:

> (10) "Uchawi, uganga na ndoto zinafanana kidogo, kwa maana kwamba inategemea unabuni nini, kwani vinawezesha ubunifu wa vitu ambavyo wakati mwingi havipo na wakati mwingine vinakuhusu wewe mwenyewe. Vipengele hivi vinaruhusu ubunifu katika kiwango chochote kile, mtu atake asitake anaweza kukubali, kwa sababu huwezi kusema kwamba tukio hili katika hali halisi halitokei. Hata kama katika hali halisi halitokei, lakini kwenye kubuni unaweza kulifanya litokee. Kwa hiyo uchawi, uganga na ndoto, kama mtu anajua jinsi ya kuvitumia vizuri vinaimarisha na kuboresha kazi ya sanaa, iwe ushairi, tamthiliya au riwaya. Hivyo, uchawi, uganga na ndoto ni kama kitunguu katika mboga. Ukitumia uchawi, uganga au ndoto unaweza kuwa na mada nyingi. Watu huanza kusema hapana anasema hivi, hapana ni hivi. Hivyo ukishaona watu wanatoa tafsiri tofautitofauti ujue kazi hiyo imefaulu, kwani inakuwa na sura nyingi katika tafsiri".

Chanzo: Data za utafiti kutokana na usaili kwa mtunzi, uliofanyika 24/6/2015

Wamitila (2002) akimrejelea Kristeva, anabainisha kuwa, mwingilianomatini sio urejelezi wa kazi fulani katika kazi nyingine tu, bali pia ni ule uingiliano wa mitindo ya kiuashiriaji. Hivyo mtunzi kwa kutumia uchawi na ushirikina kama mtindo na mbinu ya mwingilianomatini katika uashiriaji, ameweza kuibua masuala nyeti aliyokusudia kuyafikisha kwa hadhira.

### 4.2.2 Hitimisho

Sehemu hii imejadili kuhusu usuli wa mtunzi, muhtasari wa tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo* na kubainisha mbinu ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi.* Imebainika kuwa, mtunzi ametumia matini nane zinazodhihirisha mwingilianomatini katika utunzi wake. Mbinu hizo ni;

hadithi, ngoma, nyimbo, ushairi, majigambo, wahusika wa fasihi simulizi na nguvu za sihiri. Utafiti huu ulibaini kuwa utunzi wa *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ni matokeo ya athari ya mapokeo simulizi ambayo yalimuathiri mtunzi na kutumia masimulizi hayo kuzalisha tamthiliya hii. Aidha, utafiti huu pia ulibaini kuwepo na mwingilianomatini katika kazi hii ya fasihi ambapo kuna matini zilizotumika katika mapokeo simulizi zinajitokeza pia katika tamthiliya hii. Matumizi ya mbinu hizo yamedhihirisha kuwa, mtunzi ameathiriwa na kazi za fasihi simulizi na mapokeo simulizi katika utunzi wa tamthiliya yake hii.

### 4.2.3 Mwingilianomatini katika utunzi wa *Fumo Liongo*

Utafiti huu ulichunguza matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Fumo Liongo.* Katika utafiti huu, imebainika matini sita ambazo zinadhihirisha mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo. Jedwali lifuatalo linabainisha matini hizo:

**Jedwali 4.2 Matini zilizotumika katika utunzi wa *Fumo Liongo***

| **Na.** | **Aina ya matini iliyojitokeza** |
|---|---|
| 1. | Utendi |
| 2. | Ngoma |
| 3. | Nyimbo |
| 4. | Majigambo |
| 5. | Ushairi |
| 6. | Nguvu za sihiri |

Chanzo: Data za Utafiti katika *Fumo Liongo* (Juni, 2015)

Jedwali namba 4.2 linawasilisha mbinu ambazo zinadhihirisha ujitokezaji wa mwingilianomatini katika utunzi wa tamthiliya ya *Fumo Liongo*. Sehemu zifutazo zinajadili na kutoa ufafanuzi kwa mifano jinsi mbinu hizo zimejitokeza katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*.

#### 4.2.3.1 Matumizi ya Utendi

Mulokozi (1996) anafasili tendi kama utungo wenye kusimulia matukio ya kishujaa katika ngazi ya kijamii au kitaifa. Matukio yanayosimuliwa huweza kuwa ya kihistoria au huchanganya na visakale au visasili. Utafiti huu umegundua kuwa, tamthiliya ya *Fumo Liongo* ni matokeo ya mwingilianomatini ambapo mtunzi aliathiriwa na mapokeo simulizi ya utendi wa "Fumo Liongo" na hivyo kutunga tamthiliya ya *Fumo Liongo* Utendi huu unaelezea mambo yaliyowahi kutokea katika historia ya mji wa Pate. Utendi huo uliandikwa mwaka 1913 na Muhamadi bin Abubakar bin Omari al-Bakry aliyejulikana zaidi kwa jina la Muhamad Kijumwa. Inasadikiwa kuwa Kijumwa aliandika utendi huo baada ya kupata hadithi ya mapokezi simulizi yanayomhusu mtu maarufu katika historia ya Pate, aliyeitwa Fumo Liongo, anayeaminika kuwa aliishi katika karne ya 13 hadi 14, (TUKI, 1999).

Utafiti ulibaini kuwa, utendi wa "Fumo Liongo" unaelezea mgogoro uliokuwepo kati ya Fumo Liongo na kaka yake Mfalme wa Pate aliyeitwa Daudi Mringwari. Mgogoro huo ulitokana na hofu iliyokuwa imemtawala mfalme Daudi Mringwari, kuhusu kunyang'anywa ufalme wake na nduguye Fumo Liongo, ambaye alitokea kuwa mwenye nguvu, shujaa, jasiri, manju na malenga hodari aliyependwa na wananchi wa Pate. Hofu hiyo ya mfalme ilijenga chuki na fitina kali dhidi ya Fumo Liongo, kiasi cha mfalme kutafuta mbinu mbalimbali za kutaka kumuua. Fumo Liongo aligundua mipango hiyo ya ndugu yake ya kutaka kumuua, akaamua kuondoka Pate na kwenda kuishi nyikani na Wasanye, Wadahalo, Waboni na Watwa.

Hata hivyo, hila za mfalme zilifanikiwa na Fumo Liongo alikamatwa akiwa anacheza ngoma na kutiwa gerezani. Akiwa gerezani iliamriwa kuwa auawe, ila alipewa ruhusa ya kutoa ombi lake la mwisho kabla ya kuuawa. Liongo aliomba apigiwe ngoma ya mwao na gungu. Wakati ngoma ikiandaliwa, alimtuma kijakazi wake Saada, akamwambie mama Liongo kuwa, atengeneze mkate wa wishwa (pumba) na katikati aweke tupa. Ujumbe huo ulikuwa wa kishairi. Mama alitekeleza ujumbe huo na kumpa Saada mikate hiyo ampelekee Liongo gerezani. Ngoma zilipoanza, Liongo aliutumia muda huo kukata minyororo aliyofungwa kwa kutumia tupa iliyoletwa na Saada ndani ya mkate, kisha alivunja lango la jela na kutoroka kurejea nyikani.

Mfalme alipoona jaribio la kumuua Liongo limeshindwa, aliamua kutumia mbinu nyingine ya kumshawishi mtoto wa Liongo ili ampeleleze baba yake kuwa, ni kitu gani kinaweza kumuua. Mtoto huyo aliahidiwa kupewa uwaziri na kumuoa binti mfalme. Kijana huyo alikwenda kwa baba yake huko Shaka na kumuuliza kuwa ni kitu gani kinaweza kumuua. Liongo alibaini kuwa mwanae alikuwa ametumwa na adui zake, lakini aliamua kumweleza ukweli kuwa yeye hafi isipokuwa tu atakapochomwa sindano ya shaba kitovuni. Mwanae huyo alirudi kwa mfalme na kumweleza siri hiyo. Mfame akaandaa sindano ya shaba na kumpa zawadi nyingi sana kijana huyo huku akimtaka arudi akamuue baba yake. Kijana alikubali na alifanikiwa kumchoma baba yake sindano ya shaba kitovuni akiwa usingizini. Liongo alifariki baada ya kuchomwa sindano hiyo.

Wakati wa majadiliano ya vikundi na usaili, utafiti huu ulibaini kuwa, mapokezi simulizi ya hadithi ya utendi huo, yanafanana kwa kiasi kikubwa na tamthiliya ya

*Fumo Liongo.* Hii inaonyesha jinsi mtunzi alivyoathiriwa na mapokeo simulizi ya utendi huo. Wamitila (2003) anaeleza kuwa, kazi za fasihi huathiriana kiasi cha athari hizo kuonekana moja kwa moja katika kazi nyingine ya fasihi, hata kama watunzi wake ni tofauti na wana uzoefu tofauti. Vilevile kufanana huko kunadhihirisha mawazo ya Kristeva katika nadharia yake ya mwingilianomatini inayoeleza kuwa, katika kazi za fasihi kuna kuhusiana na kutegemeana, hivyo si rahisi kuzungumzia uasili au upekee wa kazi ya fasihi, kwani kwa vyovyote vile itakuwa inatokana na kazi za fasihi zilizotangulia au zilizopo. Sehemu ifuatayo imebainisha baadhi ya maeneo ya utendi wa "Fumo Liongo" yaliyoathiri utunzi wa tamthiliya ya *Fumo Liongo*.

#### 4.2.3.2 Wahusika

Utafiti huu uligundua kuwa mtunzi wa tamthiliya ya *Fumo Liongo* ameathiriwa na utendi wa "Fumo Liongo" katika uteuzi wa majina ya wahusika. Mhusika mkuu wa tamthiliya ya *Fumo Liongo* amepewa jina la Fumo Liongo anayezungumziwa katika utendi wa Fumo Liongo. Vile vile, majina ya wahusika wengine kama vile; Mbwasho na Sada ambayo ni majina ya wahusika wanaojitokeza katika utendi wa "Fumo Liongo." Athari nyingine iliyobainiwa na utafiti huu ilijitokeza katika visa na matukio. Mifano ifuatayo inabainisha hoja hii.

#### 4.2.3.3 Kisa

Utafiti huu ulibaini kuwa mtunzi wa tamthiliya ya *Fumo Liongo* amehamisha matukio yaliyomo katika Utendi wa "Fumo Liongo" na kuyatumia katika kazi yake ya tamthiliya. Athari hii inajidhihirisha katika kisa cha Wagala kutaka mbegu ya

Fumo Liongo katika kabila lao. Tazama dondoo lifuatalo kutoka kwenye tamthiliya ya *Fumo Liongo*:

ZAHIDI: Mama ana mtoto.

> MBWASHO: Nimesikia. Mtoto gani baba?
> LIONGO: Madi unakumbuka mwaka jana ulipokuja ule ujumbe wa Mfalme wa Gala kumwomba Mringwari nikubali kutoa mbegu ya simba?
> MADI: Nakumbuka sana. Uk 17

Chanzo: Data za Utafiti katika *Fumo Liongo* (Juni, 2015)

Mfano huo unadhihirisha jinsi Wagala walivyohitaji mbegu ya Fumo Liongo kwa ajili ya vizazi vyao kutokana na ujasiri, ushujaa, ushupuvu na matendo yake. Sifa hizi zinajitokeza katika matumizi ya sitiari 'simba' iliyotumika kumrejelea Fumo Liongo. Kisa hiki kinajitokeza pia katika Utendi wa "Fumo Liongo" ambapo Wagala wanaomba wapatiwe mbegu ya Fumo Liongo ili apate kuwazalia watoto wenye sifa kama zake. Kisa hicho kinapatikana katika utendi wa "Fumo Liongo" ubeti wa 41. Tazama dondoo ya ubeti huo.

(11) "Twaitaka mbeu yake
nasi kwetu tuipeke
kwa furaha tumuweke
apate kutuzaliya". Uk 29

Chanzo: Data za utafiti katika *Tenzi Tatu za Kale* (Juni, 2015)

Katika mfano huo tunaona kuwa mahitaji ya kupata mbegu ya Fumo Liongo kwa ajili ya vizazi vya jamii nyingine yanajitokeza pia katika utunzi wa Emmanuel Mbogo katika tamthiliya yake ya *Fumo Liongo*. Hii inadhihrisha kuwa mtunzi aliathiriwa na utendi huo na kuchota maudhui ya utendi huo katika utunzi wake. Aidha utafiti huu ulibaini kuwa mtunzi anatumia pia mbinu na mtindo wa kisanii katika kuwasilisha maudhui hayo mfano ni matumizi ya sitiari 'simba' katika tamthiliya yake.

### 4.2.3.4 Uchu wa Madaraka

Utafiti huu ulibaini kuwa mtunzi ametumia tukio la Mfalme kuwa na hofu ya kunyang'anywa ufalme wake na Fumo Liongo, na kujenga chuki ya wazi kwake. Hii inajidhihirisha katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* anaposema.

> (12) MRINGWARI: Mbwa huyu, japokuwa anilindia nyumba na mali yangu dhidi ya wanyang'anyi, lakini nahofia meno yake yanayozidi kuchongeka kila uchapo. Uk 8.

Chanzo: Data za Utafiti katika *Fumo Liongo* (Juni, 2015)

Mfano huo unawasilisha maneno ambayo yanadhihirisha hofu ya mfalme kupokonywa madaraka na mali zake. Tukio hili ni matokeo ya athari ambayo mtunzi ameipata kutoka katika utendi wa Fumo Liongo ubeti wa 93.Tazama mfano huu:

> (13) "Anipoke ufalume
> kisa chanda nikiume
> kheri yangu mwanamume
> kumuuwa mara moya" uk 37

Chanzo: Data za utafiti katika *Tenzi Tatu za Kale* (Juni, 2015)

Data hiyo inadhihirisha jinsi mtunzi alivyoathiriwa na maudhui yanayohusu uchu wa madaraka katika utendi wa "Fumo Liongo" na kuchota maudhui hayo na kutumia tamthiliya kuwasilisha maudhui ya utendi huo. Hii inadhihirisha kuwa mwingiliano matini katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* haujitokezi katika fani tu bali mtunzi pia amechota maudhui ya utendi huo na kuyawasilisha kwa kutumia tamthiliya. Kwa hiyo, maudhui ya utendi wa Fumo Liongo yameathiri utunzi wa tamthiliya ya *Fumo Liongo* ambayo utafiti huu umebaini kuwa ni matokeo ya athari ya kifani na kimaudhui aliyoipta mtunzi kutokana na kusoma utendi wa Fumo Liongo[4].

---

[4] Hoja hii inathibitishwa na mtunzi ambaye wakati wa usaili alikiri kuwa utendi wa Fumo Liongo umemuathiri kwa kiasi kikubwa katika utunzi wake wa tamthiliya ya Fumo Liongo.

#### 4.2.3.5 Usaliti

Utafiti huu umegundua kuwa, maudhui ya usaliti ambayo yanasababisha kifo cha Fumo Liongo katika utendi yamejitokeza pia katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* . Hii inajitokeza katika kisa cha mtoto wa kambo wa Liongo kurubuniwa na Mfalme ili akapeleleze siri ya kifo cha Liongo na pia amuue. Tazama mfano huu kutoka katika tamthiliya ambao unashadadia hoja hiyo:

(14) ZAHIDI: Nilimwuliza, "Baba mpenzi ni kitu gani kiwezacho kukuua?"…
Unataka kuniua? Aliniuliza Liongo, nikamwambia. Hata baba. Mimi nakuuliza tu, Sina nia kama hiyo. (*Kimya*). Akasema "Zahidi mwanangu, mimi ni Fumo Liongo. Simba wa Pate. Hakuna mwingine yeyote ajuaye siri ya uhai na ufu wangu ila mimi na yeye Muumba Wangu". (*Kimya kidogo*). "Mwanangu Zahidi. Mimi mkuki hauniui, mimi mshale hauniui, mimi kisu hakiniui.
Kitu chochote mimi hakiniui. Ila ukitaka kuniua mimi fanya bidii utafute sindano ya shaba…
ZAHIDI: "Uchukuwe sindano ya shaba; kwa sindano ya shaba unichome nayo kitovuni. Ukinichoma nayo kitovuni basi mie nitakufa." (*Kimya*). Uk 38

Chanzo: Data za Utafiti katika *Fumo Liongo* (Juni, 2015)

Dondoo hapo juu linawasilisha kisa cha usaliti wa mtoto kwa baba yake. Kisa hiki kimechotwa kutoka katika utendi wa "Fumo Liongo" kuanzia ubeti wa 133 hadi 144. Tazama mfano ufuatao:

(15) "Kikuuwacho ni n'ni
nami niyuwe yakini
nina hamu ya moyoni
atakuweka Jaliya. Uk 44

Chanzo: Data za utafiti katika *Tenzi Tatu za Kale* (Juni, 2015)

Pamoja na kufahamu kuwa mwanaye amesharubuniwa na Mfalme ili abaini siri yake ya kifo ili aje amuue, Liongo aliamua kumweleza ukweli wa kile kinachoweza kumuua. Tazama ubeti wa 143 hadi 144:

"Nisikiya wangu baba

Liniuwalo ni haba

Ni msumari wa shaba
Kitovuni nitikiya.

"Jamii silaha piya
Haziniuwi swabiya
Ila nimezokwambiya
Ni ya kweli yot'e piya. Uk 45

Chanzo: Data za utafiti katika *Tenzi Tatu za Kale* (Juni, 2015)

Mifano katika beti hizo inazungumzia juu ya kisa cha mtoto wa Fumo Liongo alivyomsaliti baba yake. Kisa hiki kimejitokeza katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* kama ilivyobainishwa hapo juu. Kwa ujumla utafiti huu umebaini kuwa msanii wa tamthiliya ya *Fumo Liongo* ameathiriwa na mapokeo simulizi yanayojitokeza katika utendi wa "Fumo Liongo" kuhusu kisakale cha Fumo Liongo. Athari hii ni athari ya moja kwa moja ya kifasihi ambapo msanii huchota vipengele vya kifani na kimaudhui kutoka katika kazi moja ya fasihi na kuvitumia katika utunzi wa kazi nyingine ya fasihi. Athari hii inadhihirisha mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo

Hata hivyo, utafiti huu umegundua kuwa, pamoja na kuathiriwa kifani na kimaudhui, mtunzi pia ameingiza ubunifu wake kwa kudhihirisha mbinu mbalimbali za kimtindo katika utunzi wa kazi yake ya fasihi. Hili linadhihirishwa na matumizi ya ndoto, methali mafumbo na semi, kuwa mtunzi huwa na uhuru wa kujibainisha kimtindo wakati wa kuchota vipengele vya kifani na kimaudhui kutoka katika kazi zingine za fasihi, kama matokeo ya athari aliyoipata kwa kusoma kazi zao. Hivyo, Emmanuel Mbogo katika utunzi wake ameonyesha ubunifu wake kisanii kwa kutumia mbinu za kimtindo katika kuwasilisha matukio hayo kwa kutumia mbinu na mtindo tofauti kwa mfano matumizi ya sitiari, tashibiha, methali, mafumbo na ishara.

Msanii pia katika maudhui ya kazi ya fasihi ameongeza matukio ambayo hayapo katika utendi. Kwa mfano, kitendo cha Fumo Liongo kuota ndoto inayotabiri kifo chake, hotuba ya Fumo Liongo na tukio la wananchi kwenda kumlaki Fumo Liongo aliyekuwa anatoka vitani. Kuongezwa kwa matukio hayo kunadhihirisha hoja ya kwamba, pamoja na kuwa mtunzi huathiriwa na kazi za fasihi simulizi na kuchota malighafi ya kutungia kazi yake, bado mtunzi huyo hutumia mbinu na ubunifu wake katika utunzi wa kazi husika ya kifasihi. Hivyo, mwandishi E. Mbogo, ameonyesha usanii katika utunzi wa tamthiliya hii ya kihistoria ya *Fumo Liongo*, yenye kuhifadhi historia ya mji wa Pate na shujaa wake Fumo Liongo.

Hoja hizo zinathibitishwa na maelezo ya mtunzi wakati wa usaili ambapo alikiri kuathiriwa na fasihi simulizi ya utendi wa "Fumo Liongo". Hii inadhihirisha misingi ya nadharia ya mwingilianomatini, kuwa tanzu za fasihi huathiriana, huhusiana, hutegemeana na huingiliana katika kukamilishana. Kwa hiyo, utunzi wa Emmanuel. Mbogo ni matokeo ya athari ya fasihi simulizi ya tendi za Kiafrika.

#### 4.2.3.6 Matumizi ya Ngoma

Utafiti huu uliabini kuwa mwingilianomatini katika utunzi wa tamthiliya ya *Fumo Liongo* unajidhihirisha katika matumizi ya ngoma. Ngoma kama moja ya kiperea cha fasihi simulizi inajitokeza katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*. Wakati wa majadiliano ya vikundi wahojiwa walieleza kuwa moja ya dhima ya ngoma ni kustarehesha na kuburudisha. Ngoma hufanyika katika matukio ya kijamii kama vile; kipindi cha mavuno, harusi, na sherehe mbalimbali za kijamii. Dhima hii ndiyo inayojitokeza katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* ambapo ngoma imetumika kuonyesha furaha ya wananchi wa Pate katika sherehe ya kumpokea shujaa wao Fumo Liongo, ambaye

alikuwa amerejea kutoka katika vita vya kuikomboa nchi yao dhidi ya uvamizi wa *Wabuu* wa Sango Vere. Hii inamaanisha kuwa miongoni mwa dhima zilizojitokeza katika ngoma hizo ni pamoja na kuburudisha wanajamii katika sherehe hizo. Kielelezo kifuatacho kinashadadia hoja hiyo:

> (16) MKE: Hao! (*Anaruka*) Hao! Mume wangu, hao! (*Anapiga vigelegele huku akifunga kibwaya chake vizuri*). Sikubali! Nakwambia sikubali. Leo na miye nitapenya lufufu ya watu hadi niyaguse manyoya ya Simba wa Pate. Niwapiku wenzangu kulisakata goma la Liongo.…(*Anaimba wimbo wa kumsifu Liongo wakati huohuo wanangoma wanaingia na wote wanacheza kwa pamoja*) uk 3
>
> Chanzo: Data za Utafiti katika *Fumo Liongo* (Juni, 2015)

Mfano katika dondoo hiyo unadhihirisha dhima ya ngoma katika jamii ya Pate. Aidha, wakati wa majadiliano ya vikundi utafiti huu uliabini kuwa, ngoma imetumika kama mbinu ya kisanii ili kuibua Uafrika na tamaduni za Kiafrika. Mtunzi ametumia ngoma katika tamthiliya hii ili kusadifu uhalisia wa jamii ya Kiafrika ya watu wa Pate, kwa kuingiza ujumi wa Kiafrika ili kuleta vionjo vya Kiafrika. Utafiti huu ulibaini kuwa, matumizi ya ngoma ni matokeo ya athari ya mapokeo simulizi ya utendi wa "Fumo Liongo", katika utendi huo tunabainishiwa kuwa Fumo Liongo alikuwa ni manju na malenga stadi katika uimbaji na uchezaji ngoma. Haya yanadhihirishwa na ubeti wa 79 katika uk.35

> (17) Liongo nikwambiao
> Shaha wa gungu na mwao
> tena ni mkuu wao,
> huwashinda wut'e piya

Chanzo: Data za utafiti katika *Tenzi Tatu za Kale* (Juni, 2015)

Tukirejelea nadharia ya mwingilianomatini, inaaminika kuwa, matini huchukua au hufaidi kutokana na matini nyingine (Wamitila, 2002). Hii ina maana kuwa kuwepo kwa matini katika kazi ya fasihi ni kuwepo kwa matini nyingine katika kile kinachoitwa mwanda wa kimwingilianomatini, katika kukamilishana na kujengana ili

kuleta maana. Hivyo matini ya ngoma imekamilisha na kuleta maana katika tamthiliya hii, kwani imesaidia kuwasilisha kile mwandishi alichotaka kukieleza na kukifikisha kwa hadhira wake kupitia matini hiyo.

#### 4.2.3.7 Matumizi ya Nyimbo

Utafiti huu umebaini kuwa, mwingilianomatini unajitokeza katika matumizi ya wimbo. Wimbo ni utanzu wa fasihi simulizi ambao msanii ameutumia katika utunzi na uwasilishaji wa maudhui ya tamthiliya yake. Katika tamthiliya hii mwandishi ametumia wimbo wa kumsifu Liongo baada ya kurejea kutoka vitani ambapo aliongoza mapambano dhidi ya Wabuu wa Sango Vere na kupata ushindi. Haya yanabainika katika mfano ufuatao.

(18) MUME: Umesikia! (*Akisisitiza*.) Simama twende mwanamke! (*Wanapita watu wanne ama watano hivi wakiimba*.) Liongo!Simba! Liongo! Simba! (*Kisha wanatoka*.) Uk 1.

Chanzo: Data za Utafiti katika *Fumo Liongo* (Juni, 2015)

Mfano huo unadhihirisha matumizi ya wimbo katika matini ya tamthiliya. Matumizi ya wimbo yanadhihirisha mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* ambapo mtunzi ameingiza utanzu wa fasihi simulizi katika tamthiliya yake.

Aidha, wimbo mwingine unajitokeza katika tukio la Liongo alipokuwa gerezani wakati akimpa Sada maagizo ya kumpelekea mama yake, Bi Mbwasho, ili amtengenezee mkate na katikati aweke tupa. Kielelezo kifuatacho kinabainisha wimbo huo:

(19) LIONGO: Ebu imba tena nikusikie Kijakazi wangu mwema.
SADA: *(Anaimba.)*
*Ewe Kijakazi na kutuma uwatumika,*
*Kamwambie mama, ni mwinga siyalimika,*
*Afanye mkate, kati tupa kuweka,*

*Nikeze pingu na minyoo ikinyooka,*
*Ningie ondoni ninyinyirikeja mana nyoka,*
*Tatange madari na makuta kuno kumeta.* Uk 25 -26
Chanzo: Data za Utafiti katika *Fumo Liongo* (Juni, 2015)

Mfano hapo juu unatudhihirishia kuwa nyimbo katika jamii za Afrika hutumika katika nyakati mbili; wakati wa furaha na wakati wa shida ama huzuni[5]. Kwa hiyo, wimbo huu wa Liongo umetumika wakati wa shida Utafiti huu umebaini kuwa, wimbo huo ni athari ya moja kwa moja ya utendi wa "Fumo Liongo" katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*. Mwandishi ameuchukua wimbo huo kutoka katika utendi wa "Fumo Liongo" uk 58, na kuutumia katika utunzi wa tamthiliya yake.

(20) Ewe kijakazi nakutuma hujatumika
Kamwambie mama ni muyinga hajalimuka
Afanye mkate pale kati tupa kaweka
Nikeeze pingu na minyoo ikaniuka
Nitatage kuta na madari yakiyekuka
Niuwe rijali wake wana nikiwateka
Katokeze nde kama kozi nikatotoroka
Panu kakunduwa mandakozi yuu karuka
Yuu la konde jangwa pwani kitiririka
Ningie ondoni ninyepee ja mwana nyoka
Ningie mwituni ningurume ja samba buka
Nali mti pweke nimeziye katika nyika
Si nduu si mbasi mimeziye kuwakupuka
Nduu ali mame uwasiye kinda kuitika uk 58
Chanzo: Data za utafiti katika *Tenzi Tatu za Kale* (Juni, 2015)

Mfano hapo juu unadhihirisha kuwa wimbo unaojitokeza katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* ni matokeo ya utendi wa "Fumo Liongo". Wamitila (2002) anafafanua kuathiriana huko kwa kusema kuwa matini za awali zinasaidia uelewekaji wa kazi za baadaye. Hapa tunaona jinsi wimbo wa utendi ulivyosaidia uelewekaji wa tamthiliya

[5] Wazo hili linajidhihirisha katika jamii za Kiafrika tunaona nyimbo zikiimbwa wakati wa sherehe, harusi, mikusanyiko ya furaha. Katika kipindi hiki nyimbo za kupongezana na kufurahiana huimbwa kwa furaha na vifijo Nyimbo pia huimbwa wakati wa msiba kwa ajili ya kuwaliwaza wafiwa na kumuombea marehemu na hata waliobaki.

hii katika kile kilichowasilishwa na wimbo huo, na hivyo kusaidia kujenga maana ya tamthiliya nzima.

Halikadhalika, utafiti huu umebaini wimbo mwingine wa maombolezo uliodokezwa ukiimbwa, bila kuainishwa maneno yake. Wimbo huo unaimbwa na watu waliokuwa wamebeba maiti ya Fumo Liongo. Haya yanabainishwa na mwandishi katika dondoo lifuatalo:

> *(21)* WATU: Motoooo!!! Choma Mringwari, uwa! (*Radi na ngurumo mvua*
> *inaanza kunyesha …Watu wanaondoka mbio wakilia. Moto! Moto! Moto! Motooo! Sekunde zinapita. Wanawake na wanaume kadhaa wanabeba maiti ya Fumo Liongo wanatoka, Mbwasho akifuata nyuma. Sambamba wimbo wa maombolezo unasikika ukiimbwa taratibu. Polepole mwanaga unafifia*.) uk 48

Chanzo: Data za Utafiti katika *Fumo Liongo* (Juni, 2015)

Mfano huo unathibitisha kuwa matumizi ya wimbo ni matokeo ya athari ya fasihi simulizi ya Kiafrika na falsafa ya Kiafrika ambapo wimbo hutumika kama mbinu ya faraja kwa jamii iliyokumbwa na huzuni. Hii inathibitishwa na matokeo ya utafiti huu wakati wa majadiliano ya vikundi na wakati wa usaili ambapo wahojiwa walielezea matumizi ya wimbo na utamaduni wa jamii ya Kiafrika ambao umebeba falsafa yao. Utafiti huu ulibaini kuwa, wimbo huu wa maombolezo umedokezwa tena na Machaka na Mwanamke, bila kubainishwa maneno yake baada ya mauaji ya watu yaliyofanywa na mazabania wa mfalme Mringwari uk 51. Tazama dondoo lifuatalo:

> (22) …Ila sasa wakati wa kuwakafini na kuwasitiri
> Kwa maji ya mazchozi yetu
> Hawa waliolala sasa umewadia
> [*anapiga rimba, akiimba wimbo wa maombolezo pamoja na mwanamke*
> *Aliyekuwa analia…Polepole taa zinafifia*]

Chanzo: Data za Utafiti katika *Fumo Liongo* (Juni, 2015)

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa, wimbo wa maombolezo na ule wa kuburudisha katika sherehe za mapokezi ya Liongo kutoka vitani, zinatokana na ubunifu wa mtunzi, hazimo katika utendi. Hivyo mwandishi katika tamthiliya hii, ameonyesha dhima tatu za nyimbo ambazo ni kuburudisha, kuelimisha na kuombeleza. Hii imebainika kulingana na mazingira na matukio ambamo nyimbo hizo zimetumika. Wakati wa mahojiano na mtunzi, utafiti huu ulibaini kuwa, matumizi ya nyimbo katika tamthiliya hii, yamekusudia kuingiza ujumi wa Kiafrika na kutumia utajiri ulioko katika fasihi simulizi ya Kiswahili. Matumizi ya nyimbo katika tamthiliya yanabainisha kuathiriana kwa matini za kifasihi kwa lengo la kuchangizana na kutegemeana.

#### 4.2.3.8 Matumizi ya Majigambo

Mbinu nyingine inayodhihirisha mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* ni matumizi ya Majigambo. Majigambo hayo yanajitokeza wakati Liongo akiongea na mama yake, Mbwasho:

(23) LIONGO: Unanijua mama, unanijua. Lakini wakati mwingine nadhani unanisahau: Unasahau kuwa mimi si mwanao tu bali pia mimi ni Liongo! Fumo Liongo Mama. Liongo Simba wa Pate ninayeweza kuunguruma na kuleta *zilizala* kwa watakao kunichezea, Liongo! Ala! He! …. Uk16.

Chanzo: Data za Utafiti katika *Fumo Liongo* (Juni, 2015)

Mfano huo unaonesha majigambo ambayo mhusika Liongo anayatumia kujigamba juu ya uwezo wake wa nguvu alizonazo. Katika majigambo hayo mhusika huyo anatumia sitiari kuelezea uwezo wake na nguvu zake kwa kuonesha sifa za shujaa wa Kiafrika. Hata hivyo, utafiti huu ulibaini kuwa mbinu hii ya majigambo haikujitokeza katika utendi wa Fumo Liongo bali ni mwingilianomatini ambao mtunzi anatumia mbinu za fasihi simulizi ya Kiafrika katika utunzi wa tamthiliya.

Kwa kutumia ubunifu huu msanii anachota sifa za mhusika Fumo Liongo kutoka katika utendi wa “Fumo Liongo” na kutumia mbinu za kisanii kumvisha sifa hizo mhusika wa tamthiliya yake. Hii inatokana pia na mtunzi kuathiriwa na mapokezi simulizi kuhusu mashujaa wa Kiafrika.

#### 4.2.3.9 Matumizi ushairi

Matumizi ya ushairi katika utunzi wa tamthiliya ya *Fumo Liongo*, yamebainishwa na utafiti huu pia. Haya yanabainika uk. 4 na uk 9 ambapo mtunzi ametumia lugha yenye mpangilio maalum wa mapigo na baadhi ya vina vinavyofanana mwishoni mwa mistari, ambavyo ni –“mbo” na” –“no”. Mfano wa matini yenye lugha hiyo ni hii ifuatayo:

> (24) WENA: Waziri Kiongozi: Maneno yako barabara, lakini huyu mtu si mtu,
> bali jini! Ukimnasa kwa uli<u>mbo</u>, atajinasua kwa fi<u>mbo</u> tu, Ukimkomea kwa ma<u>mbo</u> atajikwamua kwa nyi<u>mbo</u> tu, ukimng’ata kwa me<u>no</u>, yeye atajing’atua kwa mane<u>no</u> tu. Uk 4

Chanzo: Data za Utafiti katika *Fumo Liongo* (Juni, 2015)

Imebainiwa na utafiti huu kuwa, mwandishi ametumia tena lugha yenye mpangilio maalum wenye vina vinavyofanana katika hotuba ya Liongo aliyoitoa wakati wakiwa kwa Mfalme Mringwari baada ya kurudi vitani. Lugha ya hotuba hiyo ilikuwa na vina vya mwisho wa sentensi ambavyo ni ” –ao.” na “-ko” Dondooo lifuatalo linabainisha hayo:

> (25) LIONGO:…Hiyo ndio kaifa ya kondo mtukufu Mfame Mringwari, shwari na amani vimerejea tena Pate. Raia wema Wabajuni sasa waitulize mioyo y<u>ao</u>, warudi nyumbani watazame wana na migunda y<u>ao</u>. Wanaovua samaki wachukuwe ndoana z<u>ao</u>. Wenye kuzitaka ngoma wafunge vibwaya vy<u>ao</u>. Na wewe Mfalme uwatazame watu wa<u>ko</u>. Wakipatwa na kiu uwachimbie visima vy<u>ao</u>, zikipungua pembejeo, wagawie watumwa wa<u>ko</u>. Wakipatwa madonda, yaguse kwa vidole vya<u>ko</u>. W<u>ao</u> wakulinde wewe na wewe uwalinde w<u>ao</u>. … uk 9.

Chanzo: Data za Utafiti katika *Fumo Liongo* (Juni, 2015)

Utafiti umebaini kuwa, kwa kutumia lugha hiyo, mwandishi amedokeza masuala mazito yanayohitaji hadhira wayatafakari kwa kina ili kupata alichokikusudia. Lugha hiyo imemsaidia mwandishi kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa. Wakati wa mahojiano na mtunzi, ilibainika kuwa mtunzi ametumia matini ya shairi ili kuifanya kazi yake iwe bora na yenye kudumu kwa muda mrefu, kwa kuingiza ujumi wa Kiafrika, ambapo tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili hutumika. Matumizi ya ushairi katika tamthiliya hii, yanabainisha muathiriano na kuingiliana kwa matini za kifasihi kwa lengo la kuchangizana na kutegemeana katika kukamilishana kimaana.

#### 4.2.3.10 Matumizi ya Sihiri

Utafiti huu umebaini pia kuwa, mwandishi wa tamthiliya hii ametumia mbinu ya sihiri kumchora mhusika Fumo Liongo. Amemuonyesha kuwa, Fumo Liongo ni mtu wa ajabu, mwenye nguvu za sihiri ambaye hawezi kufa kwa njia yoyote zaidi ya siri ya uhai na ufu wake ambayo ilikuwa iko kitovuni. Haya yanabainishwa uk.38 Zahidi akimweleza Mfalme Mringwari kuhusu maongezi yake na baba yake, Fumo Liongo. Kutokana na majadiliano ya vikundi, ilibainika kuwa huo ni muujiza wa nguvu za sihiri.

Pamoja na hayo kutokana na nguvu zake na miujiza yake, mitego anayotegwa huitegua na anafahamu kila kinachoendelea kumhusu yeye. Hali hii inasababisha waziri Wena kumwambia Waziri Kiongozi kuwa "maneno yako barabara lakini huyu si mtu, bali jini." uk 4. Watu walijenga imani kuwa Liongo si mtu wa kawaida bali ni jini. Miujiza iliyotokea siku ya kufa kwake nayo inakazia zaidi kuwa alikuwa na nguvu za ziada zitokanazo na ushirikina au mizimu. Haya yanabainishwa uk. 44. Rejea mazungumzo ya Mwanamke 1 hadi 3. Hata hivyo, kwa mujibu wa Mulokozi

(1999), anafafanua kuwa, sifa mojawapo ya shujaa chasili katika tendi za Kiafrika ni kuwa na nguvu za ziada za sihiri. Akiorodhesha sifa za shujaa chasili anasema kuwa, shujaa wa utendi anakuwa na sifa zifuatazo:

> (29) "-Nguvu. Hapa zinazungumziwa nguvu za kimwili yaani ubabe na mabavu nguvu za kiume na kidume, yaani urijali, nguvu za kiakili na nguvu za kivita.
> -Uganga au nguvu za sihiri.
> -Mshikamano na kundi au jumuiya fulani inayomuunga mkono". Uk 11

Chanzo: Data za utafiti katika *Tenzi Tatu za Kale* (Juni, 2015)

Akiendelea kueleza anasema kuwa, nguvu za mwili au silaha pekee bila sihiri hazitoshi, maana mapambano ya shujaa na hasimu wake si mapambano ya silaha bali kwa kiwango fulani ni mapambano ya sihiri; mwenye uganga kuntu zaidi ndiye anayeshinda. Sifa zote hizi alikuwa nazo pia Fumo Liongo mhusika mkuu wa tamthiliya hii. Sifa za mhusika na suala la sihiri ni mwingilianomatini ambapo matini za fasihi simulizi zinatumika kujenga tamthiliya. Mwingilianomatini unajitokeza katika matumizi ya nguvu za sihiri ambazo zinasadifu sifa za shujaa wa Kiafrika kama anavyosawiriwa kwenye fasihi simulizi za Kiafrika hususani ngano na visakale. Matumizi ya nguvu za sihiri pia ni matokeo ya athari ya utendi wa "Fumo Liongo" kwa mwandishi. Mwandishi anachota sifa za mhusika Fumo Liongo wa kwenye utendi na kuzihamishia kwenye tamthiliya ya *Fumo Liongo.*

Wakati wa usaili, utafiti huu ulibaini kuwa, mtunzi ameathiriwa na utendi wa "Fumo Liongo" kuhusu nguvu za sihiri. Kwa hiyo, amechota vipengele na sifa zinazojitokeza katika utendi wa "Fumo Liongo" na kuzitumia katika kazi yake. Wamitila (2002) akimrejelea Kristeva katika nadharia yake ya mwingilianomatini anabainisha kuwa, mwingilianomatini sio urejelezi wa kazi fulani katika kazi nyingine tu, bali pia ni ule uingiliano wa mitindo ya kiuashiriaji. Hivyo mtunzi kwa

kutumia sihiri kama mtindo na mbinu ya mwingilianomatini katika uashiriaji, ameweza kuibua masuala nyeti aliyokusudia kuyafikisha kwa hadhira.

## 4.3 Hitimisho

Sehemu hii imejadili matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa, matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* yanajidhihirisha katika ujitokezaji wa matini za; nyimbo, ushairi, ngoma, majigambo kwa upande wa tamthiliya ya Fumo Liongo mwingilianomatini unajitokeza katika matumizi ya matini za utendi, ngoma, nyimbo, ushairi, majigambo na nguvu za sihiri.

Vilevile matumizi ya mbinu za mwingilianomatini katika tamthiliya hizi, yanadhihirisha kuathiriana, kuingiliana, kuhusiana na kutegemeana kwa matini au tanzu za kifasihi katika utunzi wa kazi za fasihi, kwa lengo la kuchangizana na kutegemeana ili kukamilishana kimaana. Hivyo uteuzi na matumizi ya matini zilizobainishwa katika tamthiliya hizo, umechangia katika uibuaji wa maana ya kazi hizo za fasihi.

Aidha, utafiti huu umebaini kuwa, utunzi wa Emmanuel Mbogo ni matokeo ya athari ya mapokeo simulizi ya fasihi simulizi ya Kiafrika. Mtunzi ameathiriwa na masimulizi ya aliyoyapata kuhusu kisakale cha kabila la Wasukuma katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na kuyahusisha na masimulizi ya kisa cha kweli cha Ubena Zomozi kuhusu uchawi na uganga. Kwa upande mwingine, tamthiliya ya *Fumo Liongo* ni matokeo ya athari ya kusoma utendi wa "Fumo Liongo" unaohusu kisakale cha

Fumo Liongo. Athari hii inajidhihirisha katika fani na maudhui ya tamthiliya yake. Msanii amechota maudhui ya visakale hivyo na kuingiza mtindo wake wa kisanaa katika kuwasilisha maudhui ya visakale hivyo. Kwa hiyo, utafiti huu umebaini kuwa, katika utunzi wa tamthiliya hizo kuna ujitokezaji wa mwingilianomatini ambao unajidhihirisha katika fani na maudhui. Aidha, data za utafiti huu zinadhihirisha kuwa, pamoja na kuathiriwa na matini za fasihi simulizi, mtunzi pia ametumia ubunifu na mbinu za kisanii kujenga na kuibua maudhui ya tamthiliya.

## 4.4 Ulinganishaji wa Matumizi ya Mwingilianomatini Baina ya tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*

Lengo mahsusi la pili la utafiti huu lilikuwa ni kulinganisha na kulinganua matumzi ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Utafiti huu ulijiuliza je, kuna kufanana ama kutofautiana katika matumizi ya mwingiliano matini baina ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*? Hivyo basi, baada ya kuchunguza, kuchambua na kubainisha matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya zote mbili, utafiti huu ulifanya ulinganishaji na ulinganuzi wa namna mwingilianomatini unavyojitokeza katika tamthiliya hizo. Lengo lilikuwa ni kubaini ni kwa jinsi gani mbinu za kisanii zilizodhihirisha mwingilianomatini katika tamthiliya hizo zinafanana na kutofautiana. Je, huu ndio upekee wa mtindo wa utunzi wa Emmanuel Mbogo katika kazi zake za fasihi? Sehemu ifuatayo inawasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti huu.

### 4.4.1 Kufanana kwa Matumizi ya mwingilianomatini katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*

Baada ya kuchunguza na kuchambua data zilizopatikana katika mapitio ya matini zote mbili, usaili na majadiliano ya vikundi, utafiti huu umegundua kuwa tamthiliya hizi zina mfanano zaidi kuliko kutofautiana. Kufanana kwa tamthiliya hizo kunajibainisha katika matumizi ya matini zifuatazo. Tazama jedwali lifuatalo;

**Jedwali 4.3 Matini zinazojitokeza katika *Ngoma ya Ngw'anamalundi* na *Fumo Liongo***

| **Na.** | **Aina ya matini iliyojitokeza** |
|---|---|
| 1. | Ushairi |
| 2. | Nyimbo |
| 3. | Ngoma |
| 4. | Nguvu za Sihiri |
| 5. | Majigambo |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (Juni 2015)

Jedwali namba 4.3 hapo juu linaonesha kuwa, msanii ametumia matini kama vile ngoma, nyimbo, majigambo, ushairi, na nguvu za sihiri katika tamthiliya zake zote mbili zilizofanyiwa uchunguzi katika utafiti huu. Matumizi ya matini hizo yametumika kama mbinu za kisanii katika kuibua maudhui ya kazi hizo.

Utafiti huu ulibaini pia kuwa, mwandishi ametumia matini hizo ili kuingiza Uafrika katika utunzi wa tamthiliya teule, ili kuleta upya na mvuto wa kipekee katika ujumi wa tamthiliya hizo katika kutumia mazingira na fasihi simulizi ya Kiafrika. Hivyo, tunaweza kusema kwamba, tamthiliya zote mbili, zimetumia uchotarishaji kwa kuingiza vipengele vya fasihi simulizi katika utunzi wake. Kwa maana hiyo,

tamthiliya hizi zimekengeuka mbinu za utunzi wa tamthiliya zilizozoeleka ambazo zinafuata misingi ya utunzi wa Aristotle.

Utafiti huu ulibaini pia kuwa, tamthiliya zote mbili ni matokeo ya athari ya masimulizi ya kimapokeo ya fasihi simulizi ya Kiafrika. Katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* mtunzi amethiriwa na masimulizi ya kisakale cha kabila la Wasukuma, kinachohusu habari za kweli za mtu maarufu katika kabila la Wasukuma aliyeitwa Mwanamalundi, aliyewahi kuishi mwaka 1892 hadi 1934. Kwa upande wa *Fumo Liongo* ni matokeo ya masimulizi ya utendi wa Kiafrika wa "Fumo Liongo" unaohusu habari za kweli za mtu shujaa na jasiri aliyeitwa Fumo Liongo, aliyeishi katika karne ya 13 hadi 14 katika mji wa Pate nchini Kenya. Uthibitisho wa athari hizo unajidhihirisha katika fani na maudhui ya tamthiliya hizo.

### 4.4.2 Kutofautiana kwa Mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*

Utafiti huu umegundua tofauti kadhaa zinazojitokeza katika tamthiliya hizi. Tofauti ya kwanza ni matini ambazo ndio msingi wa kutungiwa tamthiliya hizo. Kupitia mbinu ya mapitio ya maandiko ya tamthiliya hizo, usaili na majadiliano ya vikundi, imethibitika kuwa malighafi ya kutungia tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi,* imetokana na masimulizi ya kisakale cha kabila la Wasukuma na masimulizi ya kisa cha kweli kilichowahi kutokea katika jamii ya kijiji cha Ubena Zomozi, kuhusu mzee mmoja aliyekuwa ni mchawi anayefuga misukule, kama ilivyoelezwa katika sura ya nne. Kwa upande wa *Fumo Liongo* msingi wake ni masimulizi ya utendi wa "Fumo

Liongo" ambamo ndimo mwandishi kwa kiasi kikubwa amechota malighafi ya kutungia tamthiliya hiyo.

Tofauti nyingine iliyobainishwa na utafiti huu, ni matumizi ya matini mbalimbali katika utunzi wa tamthiliya teule. Katika *Fumo Liongo* mtunzi ametumia matini ya utendi ambayo haijitokezi katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Vile vile hadithi ni matini ambayo inajitokeza katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* lakini haijitokezi katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*. Ilibainika kuwa, sababu ya tofauti hizi imetokana na masimulizi yaliyopelekea utunzi wa tamthiliya hizi. Hivyo mtunzi alitumia matini kama alivyozipokea katika masimulizi na kuzitumia katika utunzi wa tamthiliya zake.

Aidha, utafiti huu ulibaini kuwa, katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* mtunzi ametumia matini za aina tatu za ngoma zenye dhima tofauti. Kwa upande wa *Fumo Liongo* ngoma imetumika katika kuwasilisha dhima ya furaha, kwa mfano ngoma iliyochezwa kuonyesha furaha ya Wabajuni tu.

Tofauti nyingine inajibainisha katika matumizi ya nyimbo. Tofauti hii inajidhihirisha katika dhima ya nyimbo kwa jamii husika. Kwa mfano katika *Fumo Liongo*, msanii ametumia nyimbo za aina tatu zenye dhima tofauti kama vile kuburudisha, kutoa maagizo na kuomboleza. Tofauti na matini ya *Fumo Liongo*, msanii katika matini ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ametumia wimbo mmoja tu ambao una dhima ya kuonyesha ukomavu na ujasiri.

Halikadhalika tofauti nyingine inajitokeza kwa upande wa wahusika. Katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* mtunzi ametumia matini ya wahusika wa fasihi simulizi wakati ambapo katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* hakuna wahusika wa fasihi simuli waliotumika.

Wakati wa majadiliano ya vikundi, wahojiwa walionesha kuwa, tofauti za matumizi ya matini hizo hutokana na mtindo wa usanii na dhamira zinazowasilishwa na matini hizo katika kujenga maudhui ya kazi za sanaa.

### 4.5 Hitimisho

Utafiti huu ulibaini kuwa, tamthiliya za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo* zinafanana kwa sababu zote ni matokeo ya mwingilianomatini unaotokana na athari ya utanzu wa fasihi simulizi katika utunzi wa tamthiliya. Tamthiliya zote mbili ni matokeo ya mapokeo simulizi ya visakale vya fasihi simulizi ya Kiafrika. Hii inathibitishwa na mbinu ya mwingilianomatini ilivyojitokeza katika tamthiliya zote mbili, ingawa zimetungwa na mtunzi mmoja katika vipindi tofauti vilivyopishana kwa takribani muongo mmoja. Mbinu za mwingilianomatini zilizotumika katika tamthiliya zote mbili nyingi ni zile zile isipokuwa tu zinatumika kutegemeana na mazingira na dhamira zinazowasilishwa. Hii inatuthibitishia kuwa, mtunzi ameendelea kufumbata mbinu ya mwingilianomatini katika utunzi wa kazi zake za fasihi, na hivyo tunaweza kuchukulia pia kama ndio mtindo wake katika uandishi wa kazi za fasihi.

Kutokana data za utafiti huu, matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha kuwa, utunzi wa Emmanuel Mbogo ni matokeo ya athari ya fasihi simulizi na historia ya jamii.

Pamoja na athari ya kifasihi, mtunzi huyu huingiza mbinu za kimtindo katika kuwasilisha mapokeo aliyoyakusudia. Aidha, utunzi wake umedhihirisha kuwa, mtunzi anatumia mtindo wa kisanii katika kuikosoa jamii kwa kuhusisha na mapokeo ya fasihi simulizi. Kwa hiyo, msanii huyu hatungi kazi zake nje ya jamii, mazingira yake na muktadha wa jamii yake.

### 4.6 Dhamira zinazowasilishwa na mbinu ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*

Utafiti huu ulilenga kubainisha dhamira zinazojitokeza kutokana na matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo.* Utafiti huu ulibaini kuwa, matumizi ya mwingilianomatini yanaibua dhamira mbalimbali katika matini hizo. Sehemu zifuatazo inabainisha dhamira zinazowasilishwa na matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wamalundi Fumo Liongo*.

#### 4.6.1 Dhamira zinazojitokeza katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*

Utafiti huu ulibaini kuwa, mbinu zinazodhihirisha mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* zinaibua dhamira za matini hiyo. Jedwali lifuatalo linaonyesha dhamira zilizowasilishwa na mbinu ya mwingilianomatini katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi*.

**Jedwali 1.4 Mwingilianomatini na Uibuaji wa Dhamira katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi***

| Na. | Matini | Dhamira iliyoibuliwa |
|---|---|---|
| 1. | Ngoma ya Ng'wanamalundi | Ukombozi, nafasi ya mwanamke na elimu chanya |
| 2. | Ngoma ya Chidama | Ukandamizaji, unyonyaji na elimu hasi |
| 4. | Nyimbo | Elimu na harakati za mapinduzi |
| 5. | Nguvu za Sihiri | Unyonyaji, ukandamizaji |
| 3. | Ushairi | Ukandamizaji na harakati za mapinduzi |
| 4. | Majigambo | Nguvu za unyonyaji na utawala, nguvu za ukombozi na mapinduzi |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (Juni 2015)

Jedwali namba 4.4 linawailisha dhamira zinazoibuliwa na mwingilanomatini katika tamthiliya ya Ngoma ya Ng'wanamalundi. Sehemu ifuatayo inawasilisha mjadala wa dhamira hizo.

#### 4.6.1.1 Ukombozi

Utafiti huu ulibaini kuwa, kwa kutumia ngoma mtunzi anaibua dhamira ya harakati za ukombozi na mapinduzi ya jamii. Kupitia ngoma ya Ng'wanamalundi, mwandishi anatuonyesha jitihada za vizuu kutaka kujikomboa. Ukombozi wa vizuu unabainishwa pale Ng'wanamalundi anaposema "Jukumu la ngoma ya Ng'wanamalundi ni kuleta ukombozi kwa masikini wote" Uk 43. Kielelezo kifuatacho kinabaisha hayo:

(30) NG'WANAMALUNDI: Usisahau kuwa: tendo huzaa fikra. (*anapaza sauti)* SASA WAKATI UMEFIKA WA KUCHEZA NGOMA YA NG'WANAMALUNDI: Yuko wapi adui! Yuko wapi adui!
KIZUU 1: Yuko wapi adui! Yuko wapi adui!
NG'WANAMALUNDI: Ua Chidama Ua!
KIZUU 2: Ua Chidama Ua!
NG'WANAMALUNDI: Damu! Damu! Damu!
KIZUU 3: Damu!Damu! Damu! Uk 41

Chanzo: Data kutoka katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (Juni 2015)

Data hiyo inadhihirisha harakati za ukombozi kupitia ngoma ambayo ilitumika kama mafunzo ya mbinu na harakati za ukombozi. Msanii anaonyesha kuwa, kwa kutumia ngoma ya Ngw'anamalundi vizuu wanafanikiwa kujikomboa na kurudisha njia zote kuu za uchumi mikononi mwao. Kwa ujumla mwandishi anatuelimisha kuwa, jamii yoyote ile inayotawaliwa, kunyonywa na kukandamizwa hainabudi kupewa urazini kuhusu adui wanayepambana naye ili kuweza kuweka mikakati thabiti ya kupambana naye. Kupitia mbinu ya ngoma mwandishi amefanikiwa vema kufikisha dhamira ya ukombozi kwa hadhira wake.

#### 4.6.1.2 Ukandamizaji

Utafiti huu umebaini pia matumizi ya ngoma katika kuibua dhamira ya ukandamizaji. Msanii anaichora jamii ambayo inatawaliwa na Chidama katika nyanja zote kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Chidama amechorwa kuwa ni kiwakilishi cha tabaka tawala ambalo ni tabaka kandamizi. Mtunzi anatumia ngoma ya Chidama kuwasilisha mbinu za utawala na ukandamizaji. Kwa kutumia ngoma ya Chidama vizuu wanashindwa kujitambua na hawana uwezo wa kusema lolote, zaidi ya kupokea amri kutoka kwa Chidama. Chidama anadhihirisha hayo kwa kusema:

> (31) "…Jambo kubwa hapa ni kuyateka na kuyafuga mawazo ya watu wako… Na hawawezi kusema lolote la maana kwani tayari uwezo wao wa kufikiri umeuchukuwa umo mikononi mwako. Hivyo ndivyo sisi watu wenye ujuzi tunavyofinyanga udongo ili kuumba vijakazi na vitwana vyetu. Uk 22

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, Juni 2015

Mwandishi anatufafanulia kuwa uonevu na udhalimu wanaofanyiwa wananchi sio majaliwa yao toka kwa muumba, bali ni tabia ya watu wachache ambao hujiona ni bora zaidi kuliko wenzao, hivyo huamua kuwafanya wenzao watwana na watumwa wao. Mwandishi anatuhakikishia kuwa hali hiyo huweza kuondolewa endapo tu

wananchi (vizuu) wataelimishwa vema jinsi ya kupambana na adui yao huyo anayewanyonya na kuwadhulumu.

#### 4.6.1.3 Elimu

Mbinu ya mwingilianomatini ya ngoma imebainishwa na utafiti huu katika kuwasilisha dhamira ya elimu. Katika utafiti huu, kwa kupitia maandiko ya tamthiliya hii na majadiliano ya vikundi imebainika kuwa, mwandishi anatuonyesha dhana mbili za elimu. Dhana hizo ni Elimu Chanya na Elimu Hasi.

##### 4.6.1.3.1 Elimu Chanya

Wakati wa majadiliano ya vikundi utafiti huu umebaini kuwa, elimu chanya ni ile iliyowasilishwa na ngoma ya Ng'wanamalundi. Elimu hii imetumika kama chombo cha ukombozi kwa kuwa inajenga fikra za kujikomboa kwa wananchi (vizuu) wanaokandamizwa na tabaka tawala. Elimu hiyo inatumika kuwakomboa wananchi kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.

Lengo kuu la elimu hii ni ukombozi kama ambavyo Ng'wanamalundi anatueleza kuwa "Jukumu la ngoma ya Ng'wanamalundi ni kuleta ukombozi kwa masikini wote…" Uk 43. Hivyo elimu hii imesaidia jamii kujikomboa katika nyanja zote. Elimu ni chombo muhimu kwa jamii yoyote ile, hivyo ni haki ya kila mtu katika jamii kupata elimu ili kuleta ukombozi wa kweli na kujenga jamii iliyo sawa na huru. Kwa kutumia elimu, wananchi watatambua haki zao na njia bora za kutatulia matatizo yao. Hivyo wanajamii hawanabudi wapate elimu bora itakayowawezesha kupambana na mazingara yao.

Hata hivyo mwandishi anaikumbusha jamii kujifunza yale tu yaliyo muhimu na yenye kuleta faida kwa jamii husika. Anatukumbusha hayo kwa kusema kuwa, "Kama dunia hii watu wangesema na kusoma yaliyo muhimu tu, wakatenda yaliyo muhimu tu basi dunia hii ingebadilika na kuwa peponi" uk 41. Hivyo ni vema mipango ya elimu inapoandaliwa wapangaji wakabainisha mambo machache lakini yenye umuhimu kwa jamii husika na kwa wakati husika. Matini ya ngoma imewezesha kuwasilisha vema dhamira ya elimu na kueleweka kwa hadhira iliyokusudiwa.

#### 4.6.1.3.2 Elimu Hasi

Ngoma ya Chidama ni mbinu iliyobainishwa na utafiti huu kuwa inaibua dhamira ya elimu hasi. Mtunzi anatuonyesha elimu inayotumika vibaya kama chombo cha ukandamizaji. Hii ni elimu iliyowasilishwa na ngoma ya Chidama kwa wananchi. Ngoma hii inajenga fikra za kunyonywa, kunyanyaswa, kunyenyekea na kuheshimu tabaka tawala. Elimu hii inawafanya wananchi wanaoipata (vizuu), waamini kwamba, wao wameumbwa kwa ajili ya kuwatumikia na kuwanyenyekea watu wa tabaka tawala, kwa kuwa tu wao ni wa tabaka la chini, wanyonge na hawana nguvu za kiuchumi wala njia za kujikomboa. Wanaamini kuwa kila wanachofundishwa kupitia elimu hiyo hasi ni sahihi na ndio majaliwa yao, hata kama ni kibaya na kinawaumiza, wao hufurahia tu. Haya yanabainishwa katika dondoo lifuatalo:

(32) CHIDAMA: Dansi ya Tilantiki?
MAHUBE: Dansi?
CHIDAMA: (*Anakasirika na kumgonga konzi*) kima we!
Siku zote nimekwambia lazima wacheze dansi ya Chidama. Ngoma ya kuwafanya wakakamavu wa mwili lakini mazimbwezimbwe wa roho na bongo. Dansi ya kutia mbolea nyongo ya unyonge wao. Dansi ya kurutubisha nidhamu katika kazi zao. Unayajua hayo au umesahau?
MAHUBE: Nakumbuka mzee. Uk. 17.

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, Juni 2015

Dondoo hilo linatuthibitishia kuwa, elimu hiyo kandamizi inatolewa kwa vizuu ambao ni kiwakilishi cha wananchi wa tabaka la chini, ambao wao huamuriwa tu nini wafundishwe hata kama hakiwafai au hawakihitaji, ili mradi tu kina faida na maslahi kwa tabaka tawala.

#### 4.6.1.4 Mvutano wa Kitabaka

Utafiti huu umebaini matumizi ya matini ya majigambo kuibua dhamira ya mvutano wa kitabaka. Wakati wa majadiliano ya vikundi utafiti huu ulibaini kuwa, mwandishi ametumia majigambo haya ya mahasimu wawili, Chidama, ambaye ni kiwakilishi cha tabaka tawala, mnyonyaji anayedhulumu mali za wanayonge na Ng'wanamalundi ambaye ni kiwakilishi cha tabaka tawaliwa, mtetezi wa wanyonge, kusawiri mapambano ya tabaka tawaliwa dhidi ya tabaka tawala. Hoja hii inathibitishwa na Ng'wanamalundi anapozumngumza na nyoka, "Lakini: sasa wakati umefika wa kucheza ngoma ya Ng'wanamalundi" uk.34. Hii ina maana kuwa, wakati wa mapinduzi dhidi ya dhuluma, uonevu, unyanyaswaji, ukandamizwaji na utumikishwaji umefika. Ukombozi huo dhidi ya tabaka tawala utapatikana kupitia ngoma ya Ng'wanamalundi.

#### 4.6.1.5 Usawiri wa Mwanamke

Utafiti umebaini dhamira ya usawiri wa mwanamke ikiwasilishwa kwa kutumia mbinu ya ngoma. Mwandishi anamsawiri mwanamke katika dhana kadhaa kama inavyobinishwa hapo chini:

#### 4.6.1.5.1 Mwanamke kama jasiri, shujaa na mwanamapinduzi

Dhana mojawapo ambayo imebainishwa na utafiti huu kupitia matini ya ngoma, inamuonyesha mwanamke kuwa ni jasiri, shujaa na ni chanzo cha ukombozi katika jamii. Hapa tunamrejelea Nyamiti, ambaye alimtumwa na Ng'wanamalundi akawafundishe vizuu wenzake kucheza ngoma ya Ng'wanamalundi ndani ya himaya ya hasimu wa Ng'wanamalundi, Chidama. Nyamiti aliifundisha ngoma hiyo kwa ujasiri mkubwa na hatimaye ikafanikiwa kuleta ukombozi kwa vizuu wote. Kazi ya kuwafundisha vizuu ngoma ya Ng'wanamalundi ilikuwa yenye changamoto nyingi. Haya yanabainishwa na Nyamiti kwa kusema kuwa " …nilipoanza kuwafundisha …Nilikuwa karibu kukata tama, maana maendeleo yalikuwa mwendo wa kobe." Uk 51. Baadaye Nyamiti anakuwa ni chachu ya ukombozi, kwani anashiriki kikamilifu katika kuhitimisha ukombozi na kurejesha njia zote kuu za uchumi mikononi mwa wananchi.

Seche ni mwanamke mwingine ambaye anachorwa kama shujaa na jasiri pia. Seche anajitoa muhanga na kutembea usiku wa giza nene peke yake kwa ajili ya kufuatilia kifo cha somo yake Nyamiti. Hii ni baada ya kusikia minong'ono ya wazee kuhusu kifo cha Nyamiti. Mzee mmoja alisema "Wamekwisha mchezea mtoto." Mzee wa pili akaongezea "Baadaya siku tatu atajiunga na wadudu wenzake kulima mashamba." Seche anakuwa chokochoko wa kumshawishi Chibupa waende kwa Ng'wanamalundi kufuatilia kifo cha somo yake Nyamiti. Ushawishi wake huo ndio unaoibua mafanikio ya kuleta ukombozi kwa jamii nzima (vizuu wote) dhidi ya tabaka tawala (Chidama) kupitia ngoma ya Ng'wanamalundi.

#### 4.6.1.5.2 Mwanamke kama mwenye kuthamini utu wake na mwenye kujiheshimu.

Aidha imebainika kupita utafiti huu kuwa, kupitia matini ya ngoma, mwandishi amemjenga mwanamke akiwa ni mwenye kujiheshimu na kuthamini utu wake. Haya yabainishwa kupitia matini ya ngoma ya harusi ambapo mwandishi anamsawiri Nyamiti akiwa katika maandalizi ya harusi yake na Chibupa. Nyamiti anamweleza Seche jinsi alivyokataa kuolewa na Chidama kwa kurubuniwa kwa fedha. Nyamiti anasema, "…Nimemshinda yule aliyetaka kunichukua kama sarafu. Aliyetaka kuninunua kama gunia la chumvi – anioe!...Kuuza penzi kwa mali ni kuunadi utu na nafsi yako…" uk 2. Ngoma ya harusi ni kiashiria cha ukomavu na harakati za kupinga ukandamizaji na uonevu wa tabaka tawala. Hivyo Nyamiti kukataa kununuliwa ni kuonyesha ukomavu katika harakati za kuleta mabadiliko katika jamii.

Halikadhalika kutokana na usawiri huo wa mwanamke, mwandishi anabainisha na kuikumbusha jamii kuhusu suala la wasichana kupewa uhuru na nafasi ya kuchagua wachumba wanaowataka. Kwa ujumla, anaikumbusha jamii kutomdharau mwanamke na kumuona ni kiumbe duni kisicho na thamani, faida au uwezo wa kutenda lolote katika jamii. Mwanamke pia ni kiumbe anayejitambua na kuujali utu wake, hivyo hanabudi kuthaminiwa na kheshimiwa kama wanaume.

#### 4.6.1.5.3 Mwanamke kama Chombo cha Starehe cha Mwanaume

Utafiti huu umebainisha pia dhana inayoonesha ya udhalilishaji wa mwanamke mwandishi amemsawiri mwanamake katika hali dhalili. Msanii amemsawiri mwanamke kama chombo cha kumstarehesha mwanaume. Chidama amechorwa

akiwadhalilisha wanawake kwa kuwatumia kama chombo cha kutimiza haja zake za starehe za kimwili. Haya yanabainishwa katika mazungumzo ya Nyamiti na Seche kama ifuatavyo:

(33) SECHE: Mjini amejaza wanawake tele wa kumtimizia haja zake.
NYAMITI: Na hapa shamba kafuga wengine wa kutaga na kuatamia mayai yake. Uk.4.

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, Juni 2015

Vilevile utafiti huu umebaini kuwa, Nyamiti pia alidhalilishwa kwa kufanywa chombo cha starehe baada ya kuwa kizuu. Mwandishi anatubainishia haya kupitia mazungumzo ya Nyamiti na Chidama. Chidama anamwambia Nyamiti huku akimfuata kwa uchu "Mtoto! Ule moto uliokuwa ukiwaka katikati ya miguu yangu nashukuru sasa utauzima na kuniondolea mateso yangu" uk 20.

#### 4.6.1.5.4 Mwanamke kama chombo cha Uzalishaji mali

Halikadhalika katika utafiti huu imebainika kuwa, Chidama anaoa wanawake wengi kwa ajili ya kuwatumikisha katika miradi yake. Haya yanabainika katika ngoma ya Chidama kupitia Melo, ambaye analalamika kwa kuzidiwa na kazi za kusimamia miradi ya mumewe Chidama na kusema kuwa, "Kila jambo linanihesabu mimi…" uk 11. Halikadhalika baada ya Nyamiti kufanywa kizuu, naye alidhalilishwa kwanza na kisha kuanza kutumikishwa. Mwandishi anatukumbusha kuwa mwanamke naye ni binadamu, anahitaji kuthaminiwa, kuheshimiwa na kushirikishwa katika shughuli mbalimbali za kijamii, badala ya kumchukulia kuwa ni kiumbe duni chenye kazi ya kutumikishwa tu na mwanaume, bila kufaidi kikamilifu matunda ya uzalishaji mali unaofanywa na wao.

Kwa ujumla mwandishi amesawiri hali mbalimbali zinazowakumba wanawake katika maisha yao ya kila siku katika jamii. Anawakumbusha wanajamii kwa ujumla kuwa, wanawake nao ni binadamu wanaohitaji kuheshimiwa, kusikilizwa na mwawazo yao kufanyiwa kazi kikamilifu, kwani ukombozi wa mwanamke katika jamii unamtegeme kila mwanajamii husika.

Kwa mujibu wa utafiti huu, dhamira zilizoibuliwa na mbinu ya mwingilianomatini katika tamthiliya hii ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ni Ukombozi, Ukandamizaji, Elimu, Mvutano wa Kitabaka na Usawiri wa Mwanamke. Dhamira hizi zimeibuliwa na kuwasilishwa na matini mbalimbali kama vile ngoma na majigambo.

### 4.6.2 Dhamira zinazojitokeza katika tamthilia ya *Fumo Liongo*

Utafiti huu umebaini kuwa zipo dhamira nyingi zinazojadiliwa na mwandishi kulingana na masuala mbalimbali yanayoibuliwa na kujadiliwa. Katika utafiti huu dhamira tano zimejadiliwa ili kuonyesha jinsi mbinu ya mwingilianomatini ilivyowezesha uwasilishaji wa dhamira hizo. Jedwali lifuatalo linaonyesha dhamira zilizozowasilishwa na matini mbalimbali zilizotumiwa katika mbinu ya mwingilianomatini katika tamthiliya hii.

**Jedwali 4.5 Mwingilianomatini na Uibuaji wa dhamira katika *Fumo Liongo***

| Na. | Matini | Dhamira inayoibuliwa |
|---|---|---|
| 1. | Utendi | Uongozi mbaya, uchu wa madaraka na usariti |
| 2. | Ngoma | Mapinduzi na ukombozi |
| 3. | Nyimbo | Usawiri wa mwanamke |
| 4. | Nguvu za sihiri | Ushujaa |

Chanzo: Data za utafiti katika Fumo Liongo (Juni 2015)

Jedwali Na. 4.5 hapo juu linaonesha matini zilizotumika katika tamthiliya ya Fumo Liongo na dhamira ambazo zimeibuliwa na matini hizo. Sehemu ifuatayo inajadili dhamira hizo kwa mifano kutoka katika tamthiliya husika.

#### 4.6.2.1 Uongozi Mbaya

Katika utafiti huu imebainika kuwa mtunzi ameibua dhamira ya uongozi mbaya kwa kutumia matini ya utendi. Katika matini hii mtunzi anatumia mapokeo ya utendi wa "Fumo Liongo" kuibua dhamira ya uongozi mbaya, uchu wa madaraka na usaliti unaotokana na kufumbata na kung'ang'ania madaraka. Tazama mifano ifuatayo:

(34) MRINGWARI: Mbwa huyu, japokuwa anilindia nyumba na mali yangu dhidi ya wanyang'anyi, lakini nahofia meno yake yanayozidi kuchongeka kila uchapo. Uk 8.

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Fumo Liongo,* Juni, 2015

Mfano huo unawasilisha hofu ya mfalme kupokonywa madaraka na mali zake. Tukio hili ni matokeo ya athari ambayo mtunzi ameipata kutoka katika utendi wa "Fumo Liongo" ubeti wa 93:

(35) "Anipoke ufalume
kisa chanda nikiume
kheri yangu mwanamume
kumuuwa mara moya" uk 37

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Tenzi Tatu za Kale*, Juni, 2015

Data hiyo inadhihirisha jinsi mtunzi alivyoathiriwa na maudhui yanayohusu uchu wa madaraka katika utendi wa "Fumo Liongo" na kuchota maudhui hayo na kutumia tamthiliya kuwasilisha maudhui ya tamthiliya yake.

#### 4.6.2.2 Rushwa na Usaliti

Utafiti huu umegundua kuwa, msanii ameibua dhamira ya rushwa na usaliti ambayo inasababisha kifo cha Fumo Liongo. Usaliti huo umefanywa na mwanae wa kambo kwa kurubuniwa na Mfalme. Dhamira hii ni mwingilianomatini ambao msanii amechota kisa hiki kutoka katika utendi wa”Fumo Liongo” na kuibua dhamira ya usaliti katika jamii. Tazama mfano huu kutoka katika tamthiliya ambao unashadadia hoja hiyo:

> (36) ZAHIDI: Nilimwuliza, “Baba mpenzi ni kitu gani kiwezacho kukuua?... Unataka kuniua? Aliniuliza Liongo, nikamwambia. Hata baba. Mimi nakuuliza tu, Sina nia kama hiyo. (*Kimya*). Akasema “Zahidi mwanangu, mimi ni Fumo Liongo. Simba wa Pate. Hakuna mwingine yeyote ajuaye siri ya uhai na ufu wangu ila mimi na yeye Muumba Wangu”. (*Kimya kidogo*). “Mwanangu Zahidi. Mimi mkuki hauniui, mimi mshale hauniui, mimi kisu hakiniui. Kitu chochote mimi hakiniui. Ila ukitaka kuniua mimi fanya bidii utafute sindano ya shaba…
>
> ZAHIDI: “Uchukuwe sindano ya shaba; kwa sindano ya shaba unichome nayo kitovuni. Ukinichoma nayo kitovuni basi mie nitakufa.” (*Kimya*). Uk 38
>
> Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Fumo Liongo*, Juni, 2015

Dondoo hapo juu linawasilisha kisa cha usaliti wa mtoto kwa baba yake. Kisa hiki kimechotwa kutoka katika utendi wa “Fumo Liongo” kuanzia ubeti wa 133 hadi 144. Tazama mfano ufuatao:

> (37)“Kikuuwacho ni n’ni
> nami niyuwe yakini
> nina hamu ya moyoni
> atakuweka Jaliya. Uk 44
>
> Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Tenzi Tatu za Kale*, Juni, 2015

#### 4.6.2.3 Harakati za Ukombozi

Utafiti huu ulibaini kuwa msanii ameibua dhamira ya harakati za ukombozi kwa kutumia matini ya wimbo. Hapa msanii anaonesha namna Fumo Liongo alivyotumia wimbo katika harakati za kutafuta mbinu za kujikomboa kutoka gerezani. Tazama mfano ufuatao:

(38) LIONGO: Ebu imba tena nikusikie Kijakazi wangu mwema.
SADA: *(Anaimba.)*
*Ewe Kijakazi na kutuma uwatumika,*
*Kamwambie mama, ni mwinga siyalimika,*
*Afanye mkate, kati tupa kuweka,*
*Nikeze pingu na minyoo ikinyooka,*
*Ningie ondoni ninyinyirikeja mana nyoka,*
*Tatange madari na makuta kuno kumeta.* Uk 25 -26

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Fumo Liongo*, Juni, 2015

Mfano hapo juu unatudhihirishia kuwa mbinu ya wimbo ilitumika katika harakati za ukombozi. Mwandishi ameuchukua wimbo huo kutoka katika utendi wa "Fumo Liongo" uk 58, na kuutumia katika kuibua dhamira ya ukombozi katika utunzi wa tamthiliya yake.

#### 4.6.2.4 Dhamira ya Mapinduzi

Utafiti huu ulibaini kuwa, msanii wa *Fumo Liongo* ameibua dhamira ya mapinduzi kupitia matini ya ngoma. Katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*, ngoma imetumika kuonyesha furaha ya wananchi wa Pate katika sherehe ya kumpokea shujaa wao Fumo Liongo, ambaye alikuwa amerejea kutoka katika vita vya kuikomboa nchi yao dhidi ya uvamizi wa Wabuu wa Sango Vere. Hii inamaanisha kuwa miongoni mwa dhima zilizojitokeza katika ngoma hizo ni pamoja na kuburudisha wanajamii katika sherehe hizo. Kielelezo kifuatacho kinashadadia hoja hiyo:

(39) MKE:Hao! (*Anaruka*) Hao! Mume wangu, hao! (*Anapiga vigelegele huku akifunga kibwaya chake vizuri*). Sikubali! Nakwambia sikubali. Leo na miye nitapenya lufufu ya watu hadi niyaguse manyoya ya Simba wa Pate.

> Niwapiku wenzangu kulisakata goma la Liongo.…(*Anaimba wimbo wa kumsifu Liongo wakati huohuo wanangoma wanaingia na wote wanacheza kwa pamoja*) uk 3

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Fumo Liongo*, Juni, 2015

Mfano katika dondoo hilo unadhihirisha dhamira ya mapinduzi ambapo ngoma imetumika kama sherehe ya kupatikana kwa ukombozi kupitia mapinduzi.

#### 4.6.2.5 Usawiri wa Mwanamke

Utafiti huu ulibaini pia dhamira ya usawiri wa mwanamke iliyowasilishwa kwa mbinu ya wimbo. Mwandishi amemsawiri mwanamke katika nafasi bora ambazo ni mwanamke kama jasiri na mwaminifu.

##### 4.6.2.5.1 Mwanamke kama Jasiri

Mbwasho anasawiriwa kama jasiri. Mbwasho alipata maagizo ya Fumo Liongo kupitia kwa Sada, kuhusu kutengeneza mkate na katikati aweke tupa. Maagizo hayo yalitumwa kwa wimbo ambao Liongo alimfundisha Sada ili akamwimbie mama yake. Mama huyo bila kujali wala kuogopa askari alitengeneza mkate huo na kuweka tupa kama alivyoagizwa, ili kumwokoa mwanawe katika mikono ya Mringwari – gerezani. Tupa hiyo ilimsaidia Fumo Liongo kukata minyororo aliyofungwa na kutorokea katika msitu wa kuzimuni, ambako aliishi mpaka Zahidi alipokwenda kumuua.

##### 4.6.2.5.2 Mwanamke kama Mwaminifu

Vilevile mwandishi amemsawiri mwanamke kuwa ni mwaminifu, anayepewa maagizo na kuyafikisha kwa usahihi wake. Sada anafikisha maelekezo kwa Mbwasho, mama wa Liongo, ya jinsi ya kuweka tupa katika mkate. Hata hivyo Sada naye ni jasiri kwani ameweza kupeleka mkate gerezani bila kuogopa wala

kutetereshwa na maaskari wa gerezani. Mkate huo ndio uliokuwa msaada kwa Liongo kwa kupata tupa iliyokuwemo ndani yake na kuweza kujikomboa kwa kutorokea msituni alikoishi kwa amani.

Kwa ujumla mwandishi anaonyesha kuwa, mwanamke anapoamua kufanya jambo lake hulifanya kwa usahihi na bila woga. Hivyo ni vema wanawake nao wakashirikishwa katika mipango na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kimaendeleo katika jamii. Matini ya wimbo imetumiwa vema na msanii kuwasilisha dhamira ya usawri wa mwanamke.

#### 4.6.2.6 Ushujaa

Utafiti huu ulibaini kuwa nguvu ya sihiri imetumika kuwasilisha dhamia ya ushujaa na ujasiri katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*. Katika tamthiliya hiyo mtunzi ametumia matini ya nguvu na sihiri za Fumo Liongo na jinsi nguvu hizo zilivyotumika katika kukomboa jamii yake.

Kwa ujumla, utafiti huu umebaini kuwa mtunzi ametumia mbinu ya mwingilianomatini katika kuibua dhamira za tamthiliya zake za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Matini hizo zimetumika kulingana na dhamira ambayo mwandishi alikusudia kuiwasilisha kwa hadhira. Utafiti huu umebaini kuwa, kwa kutumia mwingilianomatini msanii ameweza kuibua dhamira zaidi ya moja katika matini moja na hivyo kuwa na dhamira changamani katika tamthiliya zake.

## 4.7 Hitimisho

Katika sura hii tumebainisha mbinu ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo.* Katika tamthiliya zote mbili, imebainika kuwa mwandishi ametumia mbinu ya mwingilianomatini kwa kuhusisha matini saba katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na matini sita katika *Fumo Liongo*. Matini tano ambazo ni ngoma, nyimbo, majigambo, ushairi, na nguvu za sihiri zilitumika katika tamthiliya zote mbili.

Hata hivyo ilibainika kuwa tamthiliya zote mbili ni matokeo ya athari ya mapokeo simulizi ya Kiafrika. Hii inatokana na mtunzi kuathiriwa na mapokeo simulizi ya kisakale cha kabila la Wasukuma na mapokezi simulizi ya utendi wa "Fumo Liongo."

Vilevile tumelinganisha na kulinganua mbinu ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Katika utafiti huu ilibainika kuwa, mbinu hizi zimetumiwa kwa kadri ya uhitaji wa kinachowasilishwa na mazingira zinamotumika. Halikadhalika tulibainisha dhamira zinazowasilishwa na mbinu ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo.* Imebainika kuwa mbinu hizi zilitumika kulingana na dhamira ambayo mwandishi alikusudia kuiwasilisha kwa hadhira.

Kwa ujumla, katika sura hii, utafiti ulibaini kuwa tamthiliya za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo* zinafanana zaidi kuliko kutofautiana. Hii inathibitishwa na mbinu ya mwingilianomatini ilivyojitokeza katika tamthiliya zote mbili, ambazo ni zile zile isipokuwa tu zinatumika kutegemeana na mazingira na dhamira zinazowasilishwa. Hii inatuthibitishia kuwa, mtunzi ameendelea kufumbata

mbinu ya mwingilianomatini katika utunzi wa kazi zake za fasihi, ingawa zimetungwa katika vipindi tofauti vilivyopishana kwa takribani muongo mmoja. Hivyo tunaweza kuchukulia kuwa, huu ndio mtindo wa mtunzi katika uandishi wa kazi za fasihi.

# SURA YA TANO

# 50. MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ni sura ya mwisho ambayo ambayo imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza inahusu muhtasari, sehemu ya pili ni hitimisho na sehemu ya tatu ni mapendekezo

## 5.2 Muhtasari

Utafiti huu ulihusu tathmini ya mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo kwa kulinganisha tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kufanya tathmini ya mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo kwa kulinganisha tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988) na *Fumo Liongo* (2009) ili kubaini jinsi mtunzi huyo anavyofumbata mbinu ya mwingilianomatini katika kazi zake za fasihi na namna mbinu hiyo inavyotumika kuibua dhamira za tamthiliya hizo. Utafiti huu ulikuwa na malengo mahsusi matatu ambayo yalijibiwa na maswali matatu. Malengo hayo ni; Kubainisha matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*, kulinganisha na kulinganua matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo* na kubainisha dhamira zinazowasilishwa kutokana na matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo.*

Tatizo la utafiti huu limetokana na uelewa wa mtafiti baada ya kupitia mapitio mbalimbali na kubaini kuwa hakukuwa na utafiti ambao umejikita katika

kuchunguza na kulinganisha kipengele cha mwingilianomatini katika kazi za mtunzi mmoja. Kwa hiyo, tatizo la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo ili kuona ni jinsi gani msanii huyu anaifumbata mbinu ya mwingilianomatini katika kazi zake za fasihi. Kwa kufanya hivyo, tumeweza kuibua kufanana na kutofautiana kwa matumizi ya mwingilianomatini katika kazi za msanii mmoja zinazopishana muongo mmoja, ili kubaini endapo kuna mabadiliko yoyote ya kiubunifu na mtindo wake kisanaa. Kwa hiyo, utafiti huu umelinganisha tamthiliya mbili za mtunzi Emmanuel Mbogo, zilizotungwa katika vipindi tofauti na kupishana takribani muongo mmoja, ambazo ni: *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988), na *Fumo Liongo* (2009), ili kubaini jinsi msanii huyo anavyofumbata mbinu ya mwingilianomatini na jinsi mbinu hiyo ilivyotumika kuibua dhamira. Utafiti huu umetumia nadharia ya mwingilianomatini katika kuchunguza, kuchambua na kujadili data na matokeo ya utafiti huu.

Katika utafiti huu mbinu za utafiti zinajadiliwa kwa kina katika sura ya tatu. Katika sura hiyo, imebainishwa kuwa eneo la utafiti huu lilikuwa ni Dar es salaam. Walengwa katika utafiti huu walikuwa ni mtunzi wa tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi (1988)* na *Fumo Liongo* (2009) Emmanuel Mbogo, huyu aliteuliwa kwa sababu ndiye mtunzi wa tamthiliya hizo. Kundi jingine lilikuwa ni kundi la wanachuo wa Chuo Kikuu wanaosoma kozi ya fasihi ya Kiswahili. Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalumu. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu tatu ambazo ni mbinu ya mapitio ya maandiko, mbinu ya usaili na mbinu ya majadiliano ya vikundi. Mbinu ya mapitio ya maandiko ilikuwa ni mbinu kuu ambayo ilimsaidia mtafiti kuchambua tamthiliya

zote mbili na kubainisha mbinu ya mwingilianomatini ilivyotumika katika tamthiliya hizo. Vilevile mbinu ya usaili na majadiliano ya vikundi zilitumika kama mbinu jazilizi ambazo zilitumika kujaziliza data zilizopatikana kutoka katika mbinu kuu. Uchambuzi wa data za utafiti huu umefanyika kwa kutumia mbinu ya uchambuzi maudhui. Utafiti huu umetumia mbinu zisizo za kitakwmu katika kuwasilisha na kujadili data za utafiti.

Kwa ujumla matokeo ya utafiti huu yametokana na maswali matatu ambayo yalitokana na malengo mahususi. Kwa hiyo matokeo ya utafiti huu ni kama ifutavyo; Swali la kwanza lililenga kubaini matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Utafiti huu umebaini kuwa; mwandishi ametumia matini za; ngoma, nyimbo, majigambo, ushairi, nguvu za sihiri, hadithi, utendi na wahusika wa fasihi simulizi.

Aidha, utafiti huu umebaini kuwa tamthiliya zote ni matokeo ya mapokeo simulizi ambayo msanii aliyapata kuhusu visakale vya fasihi ya Kiswahili. Matini ya ngoma katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, imetumika kama msingi wa kuigawa tamthiliya hii, kwani imejengwa juu ya ngoma tatu zenye dhima tofauti ambazo ndizo zinazoifanya tamthiliya hiyo iweze kueleweka vema kwa hadhira wake. Ngoma hizo ni ngoma ya Chidama inayowakilisha tabaka tawala ambalo ni kandamizi, ngoma ya Ng'wanamalundi ambayo inawakilisha harakati za ukombozi za tabaka tawaliwa dhidi ya tabaka tawala, na ngoma ya arusi inayowakilisha utayari wa vijana katika kuchukua nafasi na majukumu yao katika jamii yao, ikiwemo kushiriki katika mapambano dhidi ya uonevu wa tabaka tawala.

Kwa upande wa tamthiliya ya *Fumo Liongo,* utafiti huu umebaini kuwa nyimbo zimetumika kwa dhima tatu tofauti ambazo ni kuburudisha, kupeleka maagizo na ukombozi.

Swali la pili lililenga kulinganisha na kulinganua matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Utafiti huu umebainisha kuwa, matini zilizotumika zinafanana ingawa zimetumika kwa viwango tofauti. Matini zote zilitumika kwa lengo la kuibua na kusaidia kujenga dhamira za tamthiliya husika kulingana na mazingira inamoibuliwa dhamira hiyo.

Aidha, utafiti huu ulibaini kuwa matini zote ni matokeo ya mapokeo simulizi ya visakale vya fasihi ya Kiswahili. Pamoja na kuwa zote zimetokana na masimulizi lakini matini hizo zinatofautiana katika misingi na kanuni za utunzi. Hii ina maana kuwa, *Fumo Liongo* imetokana na masimulizi ya utendi wa "Fumo Liongo", wakati *Ngoma ya Ng'wanamalundi* msingi wake wa kutungwa ni masimulizi ya kisakale cha kabila la Wasukuma cha mtu maarufu aitwaye Mwanamalundi na tukio la kweli lililowahi kutokea katika kijiji cha Ubena Zomozi, kuhusu mzee mmoja aliyekuwa mchawi wa misukule. Hata hivyo ilibainika kuwa tamthiliya zote mbili ni matokeo ya athari ya mapokeo simulizi ya Kiafrika. Hii inatokana na mtunzi kuathiriwa na mapokeo simulizi ya kisakale cha kabila la Wasukuma na mapokezi simulizi ya utendi wa "Fumo Liongo"

Swali la tatu la utafiti huu lililenga kuibua dhamira zinazowasilishwa na matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo* Swali hili liliweza kujibiwa kwa data zilizopatikana katika utafiti huu kama

ifuatavyo. Utafiti huu umebaini matini zote zilizotumiwa kama mbinu ya mwingilianomatini zinaibua dhamira kuu ya tamthiliya hizo, kwa mfano, katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* msanii ametumia matini ya ngoma kuwasilisha dhamira ya*;* Ukombozi, Elimu, Umoja na Ushirikiano, Uongozi na Usawiri wa mwanamke.

Aidha, dhamira ya ukandamizaji na unyonyaji inawasilishwa kwa kutumia nguvu za sihiri ambapo mchawi anayetumia uchawi anawasilishwa kama kiongozi anayetumia uchawi 'uongozi' wake kukandamiza na kunyonya umma wa jamii nzima. Wakati mganga wa nguvu za sihiri anatumia mbinu na ujuzi wake kama harakati za ukombozi na mapinduzi ya jamii ya tabaka tawaliwa. Kwa upande wa *Fumo Liongo* matini ambazo zinajitokeza kama mwingilianomatini zimetumika kuibua dhamira za tamthiliya hii. Kwa mfano, wimbo, ngoma, ushairi zimetumika kuwasilisha dhamira za Uongozi, Demokrasia, Rushwa, Usawiri wa Mwanamke na Ukombozi. Utafiti huu umebaini kuwa, inatokana na sababu kwamba, tamthiliya zote mbili zimetungwa katika jamii zenye matatizo yanayofanana kimsingi. Vilevile mtunzi wa tamthiliya hizo ni yuleyule mmoja, hivyo ni wazi kuwa mtazamo wake katika kuiangalia jamii yenye matatizo yanayofanana utakuwa ni uleule.

Pamoja na kufanana kwa dhamira hizo, utafiti umebaini kuwa mjadala wa dhamira hiyo unategemea tatizo na mazingira yaliyosababisha dhamira hiyo kuibuliwa na mtunzi. Kwa mfano, katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, dhamira ya Ukombozi inaelezwa tofauti na katika *Fumo Liongo*. Katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi,* ukombozi unaojadiliwa ni wa tabaka la watawaliwa dhidi ya udhalimu, unyonywaji na ukandamizaji wa tabaka tawala. Wakati ambapo katika

*Fumo Liongo* ukombozi unaowasilishwa ni wa aina mbili. Kwanza ni ukombozi wa kuikomboa nchi ya Pate dhidi ya uvamizi wa Sango Vere. Pili ni harakati za Wabajuni kutaka kuleta mapinduzi dhidi ya utawala dhalimu wa Mfalme Daudi Mringwari.

Kwa ujumla utafiti huu uligundua kuwa, tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo* zinafanana zaidi kuliko kutofautiana katika utumizi wa mbinu ya mwingilianomatini na dhamira zinazoibuliwa na mbinu hiyo, pamoja na kuwa zimetungwa kwa mwachano wa takribani muongo mmoja. Sababu kubwa ya mfanano huo ni kuwa katika tamthiliya zote mbili, imebainika kuwa mwandishi ametumia mbinu ya mwingilianomatini kwa kuhusisha matini za fasihi zimulizi katika ujenzi wa utunzi wa tamthiliya.

Aidha, ilibainika pia kuwa tamthiliya zote mbili ni matokeo ya athari ya mapokeo simulizi ya fasihi simulizi ya Kiafrika. Kuathiriana huku kunatokana na mtunzi kuathiriwa na masimulizi ya kisakale cha kabila la Wasukuma na mapokezi simulizi ya utendi wa "Fumo Liongo." Kwa ujumla tamthiliya zote mbili ni tamthiliya zilizochanganya vionjo vingi vya Kiafrika. Vionjo hivyo ni pamoja na matumizi ya nyimbo, majigambo, ngoma, ushairi na nguvu za sihiri.

Halikadhalika tamthiliya hizi zimetungwa na mtunzi yuleyule, hivyo hiyo huweza kuwa ni miongoni mwa sababu zinazoleta mfanano wa karibu kuliko utofautiano. Hii ni kutokana na kuwa mtunzi ameendelea kufumbata mbinu ya mwingilianomatini katika utunzi wake, pamoja na kuwa tamthiliya hizo zina muachano wa muongo

mmoja katika kutungwa kwake. Utafiti huu ulibaini kuwa, mwingilianomatini ni mbinu ya utunzi wa Emmanuel Mbogo kwa sababu mtunzi huyu anatumia matini mbalimbali ndani ya matini nyingine. Aidha, utunzi wake umedhihirisha kuwa ni matokeo ya athari ya mapokeo aliyoyapata kuhusu fasihi simulizi za Kiafrika hususani visakale. Utafiti huu unamtaja Emmanuel Mbogo kama mwanamwingilianomatini ambaye anadhihirishwa na utunzi wa kazi zake za fasihi. Hivyo, mwingilianomatini ndiyo unampa upekee wake na mtindo wake wa usanii.

## 5.3 Hitimisho

Utafiti huu unahitimisha kuwa Emmanuel Mbogo anatumia mwingilianomatini katika utunzi wake kwa kuingiza matini za fasihi simulizi katika utunzi wa tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo* na hivyo kuzifanya ziwe zinafanana zaidi kuliko kutofautiana. Katika tamthiliya zote mbili, mtunzi ameingiza vipengele vya fasihi simulizi ambavyo ni matokeo ya masimulizi na mapokeo ya visakale vya fasihi simulizi ya Kiswahili. Hii imetuthibitishia kuwa, mtunzi ameendelea kufumbata mbinu ya mwingilianomatini katika utunzi wa kazi zake za fasihi, ingawa zimetungwa katika vipindi tofauti, vilivyopishana kwa takribani muongo mmoja. Hivyo tunaweza kuchukulia kuwa, huu ndio upekee wa kimtindo wa mtunzi Emmanuel Mbogo katika uandishi wa kazi zake za fasihi.

Halikadhalika iligunduliwa na utafiti huu kuwa, mtunzi ameathiriwa na mapokeo simulizi ya fasihi simulizi, kwani tamthiliya zote mbili ni matokeo ya athari ya mapokeo simulizi ya Kiafrika. Hii inatokana na mtunzi kuchota malighafi yake ya kutungia tamthiliya hizi kutoka katika masimulizi hayo ya kimapokeo. *Ngoma ya Ng'wanamalundi* inatokana na mapokeo simulizi ya kisakale cha ngano za kabila la

Wasukuma na kisa cha kweli kilichowahi kutokea katika jamii ya watu wa Ubena Zomozi, na *Fumo Liongo* inatokana na mapokezi simulizi ya utendi wa "Fumo Liongo" kama dafina za kutungia tamthiliya zake.

## 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu umefanywa kwa kutumia tamthiliya mbili za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo,* zote za Emmanuel Mbogo ambazo zinapishana kwa takribani muongo mmoja. Utafiti huu unapendekeza kuwa, tafiti zingine zinaweza kufanyika kwa waandishi wengine kwa kutumia kazi zao za fasihi. Tafiti kama hizo zinaweza kutusaidia kuelewa utunzi wa msanii na mbinu zake za utunzi ili kubaini upekee wake katika utunzi. Aidha, utafiti unaweza kufanyika kwa kuchunguza kazi za watunzi tofauti, lengo likiwa ni kufanya utafiti wa kina kuhusiana na mbinu ya mwingilianomatini katika utunzi wa tamthiliya, riwaya au ushairi. Vilevile tafiti nyingine zinaweza kufanyika kwa kina zaidi kuchunguza mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo kwa kutumia vitabu vyake vya awali na vya sasa ili kuweza kutoa hitimisho la upekee wake katika utunzi wa kazi za sanaa.

## MAREJEO


Adam, O.A (2014) "Kuchunguza dhamira za kijamii na kiutamaduni katika riwaya ya Kiswahili: Uchambuzi kifani wa *Kuli* na *Vuta Nkuvute*" Tasnifu ya shahada ya Uzamivu ya Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Allen, G (2000), *Intertextuality*, Routledge, London.

Babbie,E (1992), *The Practice of social Research 6$^{th}$ Ed*., Wadsworth Publishing Company, Calfonia.

BAKIZA (2010), *Kamusi ya Kiswahili Fasaha*, Oxford University Press, East African Limited, Kenya.

Basnett, S (1993), *Comperative Literature: Acritical Introduction*, Oxford, Blackwell.

Boaz, B. Z. (1974), *Mwanamalundi: Mtu Maarufu katika Historia ya Usukuma*, Wizara ya Elimu ya Taifa, Dar es Salaam, Tanzania.

Bryman, A (2004), *Social Research Methods* 2$^{nd}$ Ed. Oxford Univerity Press.

Enon, J.C (1998), *Educational Reseach: Statistics and Measurement 2$^{nd}$ Ed*. Depatment of Distance Education, Makerere University, Kampala.

Fadhil, E (2014) "Dhima ya Mtindo katika Tamthiliya za Kihistoria: Utafiti Linganishi waTamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile*: Tasnifu ya Uzamili ya Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Herman, L (2011) "Dhana ya Mwingilianomatini kwenye Hadithi za Watoto katika Kiswahili" Makala katika Kioo cha Lugha: Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Jilala, H (2008), "The Artist Uses of Metaphors in constructing meaning in new generation songs in Tanzania" M.A Linguistic Desertation, University of Dar es Salaam.

Jilala, H (2014), "Athari za Kiutamaduni katika Tafsiri: Mifano kutoka Matini za Kitalii Katika Makumbusho za Tanzania" Tasnifu ya shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kombo, D.K na Tromp D.L (2006), *Proposal and Thesis Writing and Introduction*, Paulines Publication African, Nairobi.

Kothari, R.C. (2013). *Research Methodology.Methods and Techniques,* 2nd Ed, New Age International (P) Ltd, New Delhi.

Kristeva, J (1980), *Desire in Language: A Semiotic Approach to Literature and Art*, Columbia Universiyy Press, New York.

Lemanster, T (2012) "What is intertextuality", Great World Text: A programme of the centre for Humanities, University of Wisconsin- Madson, Wisconsin.

Mbogo, E (2009) *Fumo Liongo*,Dar es Salaam University Press, Dar es Salaam.

Mbogo, E (1988), *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, Education Services centre Ltd, Dar es Salaam.

Mkuwili, O (2014) "Fani na Maudhui katika ya Ngoma ya Ng'wanamalundi na Kivuli Kinaishi" Utafiti Linganishi: Tasnifu ya shahada ya Uzamili katika Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Macha, N (2013), "Matumizi ya mtindo wa Mwingilianomatini kwenye Tendi" Makala katika chombez.blogspot.de/2013/05/800x600-normal-0-21-false-false-false-23.html?m=1

Malangwa, P.S. (2010), "Handling Technical Translations: The Case of Translations of Computer Programs from English into Kiswahili." Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M (1996), *Fasihi ya Kiswahili*, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania,

Dar es Salaam.

Mutembei, K.A (2012) Korasi katika Kiswahili: Nadharia mpya ya Uhakiki, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

Ndumbaro, E (2013) “Taathira katika Fasihi: Msingi wa kuwepo motifu za aina moja katika Tanzu anuai za Fasihi za mataifa /makabila tofautitofauti ulimwenguni” makala katika chombez.blogspot.de/2013/10/taathira-katika-fasihi.html?m=1 Bubujiko la Maarifa, Ijumaa tarehe 4 October 2013.

Neuman, N.L (2006) *Social Research,6$^{th}$ Edition*, Boston Pearson.

Njogu K & Wafura, (2007) *Nadharia za uhakiki wa fasihi,* Jomo Kenyata Foundation, Nairobi.

Omary, M (2011), “Siasa katika ushairi wa Kezilahabi: Uchunguzi wa *Karibu Ndani* (1988) na *Dhifa* (2008), Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Padgett, D. (2002). *Qualitative Methods in Social Work Research: Challenges and Rewards.* Sage Publications Inc. London.

Ponera, A. S (2014), *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*, Karjamer Printing Technology, Dar es Salaam.

Powell, R, Conway,C and Lynda, R (2004), ”Effects of Student Predisposing Characteristics on Student Success”,Journal of Distance Education,Vol 5, No.1,Page 20-37.

Salem, M (2013) “Maudhui na Fani katika tamthiliya za Kiswahili’: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya ya *Mashetani*na*Kivuli Kinaishi*, Tasnifu ya PhD katika Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Schutt, R. K. (2006). *Investigating the social world: The process and practice of research*. Sage Publications, London.

Senkoro, F.E.M.K (1982) *Fasihi*, Press & Publicity centre, Dar – es – Salaam.

Senkoro, F.E.M.K (2011) *Fasihi: Mfululizo wa Lugha na Fasihi*, KAUTTU, Dar es Salaam.

Spata, A. V (2003) *Research Methods: Science and Diversity*, John Willey & Sons Inc. USA.

Speziale, H.S. and Carpenter D.R (2006), *Qualitative research in Nursing: Advancing the Humanistic Imperative,* Lippincott Williams and Wilkins, Philadelphia.

Totosy de Zepetnek, S (1996a) "Essays in Reader-Oriented Theory,Criticism and Pedagogy", Katika jarida la International Perspectives on Reading, M. Steven Totosy de Zepetnek, Michigan Technology University, Michigan.

Totosy de Zepetnek, S (1998) *Comperative Literature: Theory, Method and Application,* Rodopi, Amsterdam- Atlanta.

TUKI (1999), Tenzi Tatu za Kale: Fumo Liongo, Al – Inkishafi, Mwanakupona, Taasisi Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

TUKI, (2013) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (toleo la 3) Oxford University Press, Nairobi.Walliman, N (2011) *Research Methods: The Bases*, Routledge, London and New York.

Wamitila, K.W (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*, Phoenix Publishers Ltd, Nairobi.

Wamitila, K.W (2003) *Kamusi Fasihi: Istalahi na Nadharia,* Focus Publication Ltd, Nairobi, Kenya.

Wamitila, K.W (2008)Kanzi ya Fasihi: Misingi na Uchambuzi wa Fasihi, Daisy Printers (K) Ltd, Nairobi, Kenya.

## KIAMBATISHO Na. 1

## MWONGOZO WA MASWALI YA USAILI KWA AJILI YA MTUNZI WA TAMTHILIYA YA NGOMA YA NG'WANAMALUNDI NA FUMO LIONGO

Mpendwa Mhojiwa,

Ninafanya utafiti kuhusu Tathmini ya Mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo: Ulinganishaji wa tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza mwingilianomatini katika utunzi wa tamthiliya teule ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988) na *Fumo Liongo* (2009) za Emmanuel Mbogo ili kubaini jinsi mtunzi huyo anavyofumbata mbinu ya mwingilianomatini katika kazi zake za fasihi na jinsi gani mbinu hiyo inatumika kuibua dhamira za tamthiliya hizo teule.

Nitashukuru sana wewe kama mwandishi wa tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumoliongo* kama utaweza kujibu maswali ya usaili kwa makini, uwazi na ushirikiano wa hali ya juu. Kumbuka taarifa zote zitakazotolewa zitahifadhiwa kama siri baina ya mtafiti na mhojiwa na pia zitatumika kwa ajili ya utafiti huu tu na sivinginevyo.

1. Tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo* zinaonyesha visa vyake vimetokana na matukio ya kweli yaliyowahi kutokea katika jamii, je ni nini kilikusukuma kutunga tamthiliya hizo?
2. Tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumoliongo* zinaonyesha zimetumia mbinu ya mwingilianomatini kwa kiasi kikubwa, je nini umuhimu wa kutumia mbinu hiyo?
3. Je, ni mtunzi gani aliyekuathiri katika utunzi wako hasa katika matumizi ya mbinu hiyo ya mwingilianomatini?
4. Unafikiri dhana ya mwingilianomatini inaeleweka vema kwa hadhira wako?
5. Unadhani mbinu ya mwingilianomatini uliyoitumia katika tamthliya zako za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo* imefanikisha kufikisha dhamira ulizokusudia ziwafikie hadhira wako?

**ASANTE KWA USHIRIKIANO**

**KIAMBATISHO Na. 2**

**MWONGOZO WA MASWALI YA MAJADILIANO KATIKA VIKUNDI KWA WANAFUNZI WANAOSOMA FASIHI YA KISWAHILI KUHUSU TAMTHILIYA YA *NGOMA YA NG'WANAMALUNDI* NA *FUMO LIONGO***


Mpendwa Mhojiwa,
Ninafanya utafiti kuhusu Tathmini ya Mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo: Ulinganishaji wa tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza mwingilianomatini katika utunzi wa tamthiliya teule ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988) na *Fumo Liongo* (2009) za Emmanuel Mbogo ili kubaini jinsi mtunzi huyo anavyofumbata mbinu ya mwingilianomatini katika kazi zake za fasihi na jinsi gani mbinu hiyo inatumika kuibua dhamira za tamthiliya hizo teule.

Nitashukuru sana wewe kama mwanafasihi ya Kiswahili utaweza kushiriki katika majadiliano ya vikundi kwa kujibu maswali kwa makini, uwazi na ushirikiano wa hali ya juu. Kumbuka taarifa zote zitakazotolewa zitahifadhiwa kama siri baina ya mtafiti na mhojiwa na pia zitatumika kwa ajili ya utafiti huu tu na sivinginevyo.

1. Je, mmeshawahi kusoma vitabu vya tamthiliya za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*
2. Mnaelewa nini kuhusu mbinu ya mwingilianomatini katika kazi ya fasihi?
3. Je, ni mbinu zipi za mwingilianomatini zinazojitokeza katika tamthiliya za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*?
4. Matini za mbinu ya mwingilianomatini katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo* zimetumikaje?
5. Ni dhamira zipi zinazoibuliwa na kila moja ya matini za mwingilianomatini iliyotumika katika tamthliya za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*?
6. Je, mtunzi amefanikiwa katika kutumia mbinu ya mwingilianomatini ili kufikisha dhamira alizokusudia kwa hadhira wake kupitia *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*

**ASANTE KWA USHIRIKIANO**

## KIAMBATANISHO Na. 3
## PICHA YA PAMOJA YA MTUNZI WA TAMTHILIYA TEULE NA MTAFITI



Pichani kulia mwa msomaji, ni mtunzi wa tamthiliya za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo* Profesa Emmanuel Mbogo, akiwa na mtafiti wa utafiti huu, Bibi Rehema Adam Mningo, katika ofisi ya mtunzi, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam. Picha hiyo ilipigwa baada ya usaili uliofanywa na mtafiti kwa mtunzi, tarehe 24/06/2015.